"Maoni ya Watu 2007" ni utafiti mkubwa kuliko wote uliofanyika Tanzania bara hadi sasa. Watanzania 7,879 wa umri kutoka miaka 7 – 90 kutoka mikoa kumi ya Tanzania Bara waliulizwa maoni yao kuhusu vipengele mbalimbali vya maendelo ya kiuchumi, hali zao za maisha, ubora na upatikanaji wa huduma za uchumi na kijamii na mwelekeo wa utawala bora.

Mambo yaliyomo katika ripoti hii ni pamoja na ustawi wa jamii, umaskini wa kipato, elimu, mawasiliano, barabara, huduma za afya, nishati, maji, njia za kujipatia riziki, uvuvi, kilimo, ushiriki wa wananchi, utawala bora, uwajibikaji, rushwa, uhalifu, ulevi na usalama.

ISBN 978-9987-615-29-2

MAONI YA WATU 2007

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# MAONI YA WATU 2007

**...Watanzania Watoa Maoni Yao...**



# MAONI YA WATU 2007

## WATANZANIA WATOA MAONI YAO KUHUSU:

UKUAJI WA UCHUMI NA UPUNGUZAJI
WA UMASKINI WA KIPATO,
HALI YAO YA MAISHA NA USTAWI WA JAMII,
NA UTAWALA BORA NA UWAJIBIKAJI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MFUMO WA USIMAMIZI WA MKUKUTA:**
KUNDI LA UTAFITI NA UCHAMBUZI NA KUNDI LA WATAALAMU WA MAWASILIANO,
WIZARA YA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI

**DESEMBA 2007**

Maelezo zaidi na nakala za taarifa hii inaweza kupatikana kutoka:

**Sekretariati ya MKUKUTA, Kitengo cha Kupunguza Umaskini,**
Wizara ya Fedha na Uchumi,
S.L.P. 9242, Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 (22) 2113856 / 2124107
Baruapepe: mkukutamonitoring@gmail.com
Tovuti: www.povertymonitoring.go.tz

Pia kutoka Sekretariati ya Kundi la Utafiti na Uchambuzi:
**Research on Poverty Alleviation (REPOA),**
Kitalu 157, Mtaa wa Migombani, Regent Estate,
S.L.P. 33223, Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 (22) 2700083 / 0784 555 655
Baruapepe: repoa@repoa.or.tz
Tovuti: www.repoa.or.tz

Imechapishwa na REPOA kwa niaba ya Kundi la Utafiti na Uchambuzi
© Kundi la Utafiti na Uchambuzi, 2008

**ISBN 978-9987-615-29-2**

Kwa marejeo taja: Kundi la Utafiti na Uchambuzi, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. 'Maoni ya Watu (2007): Watanzania Watoa Maoni Yao kuhusu: Ukuzaji wa Uchumi na Upunguzaji wa Umaskini wa Kipato, Hali Yao ya Maisha na Ustawi wa Jamii, na Utawala Bora na Uwajibikaji.' Dar es Salaam, Tanzania.

Maneno muhimu: Tanzania, utafiti wa maoni, ustawi wa jamii, utawala bora, uwajibikaji, umaskini wa kipato, elimu, mawasiliano ya simu, barabara, wazee, huduma za afya, vijana, nishati, riziki, uvuvi, maji, wafugaji, ushiriki, rushwa, uaminifu, uhalifu, ulevi, usalama, maliasili, watoto.

# YALIYOMO


Orodha ya Majedwali . . . . . . . . . . V
Orodha ya Vifupisho . . . . . . . . . . VII
Shukrani . . . . . . . . . . VIII
**Muhtasari . . . . . . . . . . IX**
**Sura ya 1 Utangulizi na Methodolojia . . . . . . . . . . 1**
1.1 Usuli . . . . . . . . . . 1
1.2 Methodolojia . . . . . . . . . . 2
1.3 Taswira ya ripoti . . . . . . . . . . 4

**SEHEMU YA KWANZA: MKUKUTA KUNDI LA I - Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini . . . 5**

**Sura ya 2 Hali ya Uchumi wa Watu. . . . . . . . . . 7**
2.1 Mwelekeo wa hali ya uchumi wa watu . . . . . . . . . . 7

**Sura ya 3 Kuendeleza Ukuaji Mpana wa Uchumi: Miundombinu . . . . . . . . . . 9**
3.1 Barabara . . . . . . . . . . 9
3.2 Nishati . . . . . . . . . . 10
3.3 Simu . . . . . . . . . . 10

**Sura ya 4 Hali ya Uchumi . . . . . . . . . . 11**
4.1 Gharama za maisha . . . . . . . . . . 11
4.2 Njia za kujipatia riziki mijini na vijijini . . . . . . . . . . 12

**Sura ya 5 Kilimo. . . . . . . . . . . 13**
5.1 Umiliki wa ardhi na teknolojia ya kilimo . . . . . . . . . . 13
5.2 Aina ya mazao yanayolimwa . . . . . . . . . . 13
5.3 Matatizo makuu yanayowakabili wakulima . . . . . . . . . . 14
5.4 Matumizi ya mbolea na pembejeo nyinginezo . . . . . . . . . . 15
5.5 Ushauri wa kitaalamu unaotolewa kwa wakulima . . . . . . . . . . 15
5.6 Masoko . . . . . . . . . . 16
5.7 Mwelekeo wa utoaji wa huduma za kilimo . . . . . . . . . . 16
5.8 Msaada wa serikali kwa wakulima . . . . . . . . . . 17
5.9 Wafugaji na wakulima wanaojishughulisha na ufugaji . . . . . . . . . . 18
5.10 Wavuvi . . . . . . . . . . 20
5.11 Matumizi ya maliasili. . . . . . . . . . . 21

**Sura ya 6 Vyanzo vya Riziki kwa Vijana . . . . . . . . . . 23**
6.1 Hali ya uchumi kwa vijana. . . . . . . . . . . 23
6.2 Mwelekeo wa hali yao ya uchumi . . . . . . . . . . 23
6.3 Matatizo yanayowakabili vijana . . . . . . . . . . 24

**Sura ya 7 Kulinganisha na Matokeo Mengine ya Utafiti wa Mwaka 2003 na 2007 kuhusu Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini . . . . . . . . . . 25**

**SEHEMU YA PILI: MKUKUTA KUNDI LA II - Maisha Bora na Ustawi wa Jamii . . . . . . . . . . 27**

**Sura ya 8 Elimu ya Msingi na Sekondari . . . . . . . . . . 29**
8.1 Kwenda Shuleni . . . . . . . . . . 29

8.2 Vyumba vya madarasa . . . . . . . . . . 29
8.3 Vitabu vya kiada . . . . . . . . . . 30
8.4 Vyoo . . . . . . . . . . 30
8.5 Kompyuta. . . . . . . . . . . 31
8.6 Mahudhurio ya wanafunzi shuleni . . . . . . . . . . 31
8.7 Walimu. . . . . . . . . . . 32
8.8 Utafiti wa 'Maoni ya Watoto' . . . . . . . . . . 33

**Sura ya 9 Afya . . . . . . . . . . 35**
9.1 Hali ya afya na matatizo yanayohusiana nayo . . . . . . . . . . 35
9.2 Huduma za afya. . . . . . . . . . . 35
9.3 Huduma za afya shuleni . . . . . . . . . . 36
9.4 Usalama barabarani . . . . . . . . . . 36

**Sura ya 10 Huduma ya Maji . . . . . . . . . . 39**
10.1 Vyanzo vya maji majumbani na utaratibu wa malipo . . . . . . . . . . 39
10.2 Mwelekeo na matatizo katika utoaji wa huduma ya maji . . . . . . . . . . 39
10.3 Huduma ya maji shuleni . . . . . . . . . . 40

**Sura ya 11 Wazee . . . . . . . . . . 43**
11.1 Vyanzo vya riziki kwa wazee . . . . . . . . . . 43
11.2 Vyanzo vya misaada kwa wazee . . . . . . . . . . 43
11.3 Huduma ya maji kwa wazee . . . . . . . . . . 44
11.4 Huduma za afya kwa wazee . . . . . . . . . . 44
11.5 Huduma zinazotolewa na wazee . . . . . . . . . . 45
11.6 Wasiwasi wa wazee kuhusu mustakabali wao . . . . . . . . . . 45

**Sura ya 12 Kulinganisha na Matokeo Mengine ya Utafiti wa Mwaka 2003 na 2007 kuhusu Utoaji Huduma . . . . . . . . . . 47**

**SEHEMU YA TATU: MKUKUTA KUNDI LA III - Utawala Bora na Uwajibikaji . . . . . . . . . . 49**

**Sura ya 13 Utawala Bora na Uwajibikaji . . . . . . . . . . 51**
13.1 Ushiriki wa wananchi katika masuala ya umma . . . . . . . . . . 51
13.2 Habari na mawasiliano . . . . . . . . . . 53
13.3 Ufahamu na maoni kuhusu sera . . . . . . . . . . 54
13.4 Maoni kuhusu viongozi wa serikali na vyama vya siasa . . . . . . . . . . 55
13.5 Uwajibikaji . . . . . . . . . . 55
13.6 Rushwa. . . . . . . . . . . 56

**Sura ya 14 Uaminifu, Ushirikiano na Usalama . . . . . . . . . . 61**
14.1 Uaminifu. . . . . . . . . . . 61
14.2 Uhalifu na ulevi . . . . . . . . . . 62
14.3 Mshikamano na ushirikiano katika jamii . . . . . . . . . . 64

**Sura ya 15 Hitimisho na Mambo ya Kufanya Kisera . . . . . . . . . . 65**

**Marejeo . . . . . . . . . . 66**

# ORODHA YA MAJEDWALI


Jedwali 1.1 Mgawanyo wa viwango vya umaskini wa mtu mmoja mmoja . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .2
Jedwali 2.1 Maoni ya wananchi kuhusu mabadiliko ya kiuchumi 2004-07 . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .7
Jedwali 2.2 Mabadiliko ya hali ya kiuchumi 2004-07 kwa madaraja ya vipato . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .7
Jedwali 2.3 Mabadiliko katika maisha 2004-07. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .8
Jedwali 3.1 Asilimia ya watu wazima walioripoti hali ya barabara kuwa tatizo kuu . . . . . . . . . . . . . . . . .9
Jedwali 3.2 Maoni kuhusu mabadiliko ya ubora wa barabara 2004-2007. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .9
Jedwali 3.3 Vyanzo vya nishati ya mwanga na ya kupikia. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .10
Jedwali 3.4 Njia za mawasiliano, kwa maeneo. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .10
Jedwali 4.1 Matatizo ya bei ya chakula na bidhaa muhimu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .11
Jedwali 4.2 Kazi / vyanzo vya riziki . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .12
Jedwali 5.1 Asilimia ya wakulima wa mazao makuu ya chakula . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .13
Jedwali 5.2 Asilimia ya wakulima walioripoti kutumia sehemu kubwa ya mazao kwa matumizi ya nyumbani . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .14
Jedwali 5.3 Matatizo makubua yanayowakabili wakulima . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .14
Jedwali 5.4 Matumizi ya pembejeo asilia na za kibiashara katika kilimo . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .15
Jedwali 5.5 Ushauri wa kitaalamu kwa wakulima . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .15
Jedwali 5.6 Mwelekeo wa upatikanaji wa huduma za kilimo, mabadiliko kwa miaka mitatu Iliyopita, kwa kiwango cha umaskini kwa mtu mmoja mmoja . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .16
Jedwali 5.7 Mwelekeo wa upatikanaji wa huduma za kilimo, mabadiliko kwa miaka mitatu Iliyopita . . .17
Jedwali 5.8 Msaada wa serikali kwa wakulima . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .17
Jedwali 5.9 Msaada kutoka serikalini wanaoupendelea wakulima Ili kuongeza uzalishaji katika kilimo . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .18
Jedwali 5.10 Matatizo yanayowakabili wafugaji . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .18
Jedwali 5.11 Msaada wa serikali katika kuboresha shughuli za ufugaji . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .19
Jedwali 5.12 Msaada kutoka serikalini wanaoupendelea wafugaji . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .20
Jedwali 5.13 Msaada kutoka serikalini wanaoupendelea wavuvi kuboresha viwanda vya samaki . . . . . .21
Jedwali 5.14 Matumizi ya maliasili . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .21
Jedwali 6.1 Hali ya uchumi kwa vijana kijinsia . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .23
Jedwali 6.2 Mwelekeo wa hali ya uchumi kwa vijana . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .23
Jedwali 6.3 Mabadiliko ya siku za karibuni katika maisha ya vijana . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .24
Jedwali 6.4 Matarajio ya vijana kiuchumi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .24
Jedwali 6.5 Matatizo yanayowakabili vijana . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .24
Jedwali 7.1 Matatizo makuu kwa madaraja kama yalivyoripotiwa mwaka 2003 na 2007 . . . . . . . . . . .25
Jedwali 8.1 Kwenda shuleni . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .29
Jedwali 8.2 Utoshelevu wa vyumba vya madarasa . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .30
Jedwali 8.3 Mabadiliko ya hali ya vyumba vya madarasa . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .30
Jedwali 8.4 Upatikanaji wa vitabu vya kiada . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .30
Jedwali 8.5 Utoshelevu wa vyoo vya shule . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .31
Jedwali 8.6 Upatikanaji na utumiaji wa kompyuta . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .31
Jedwali 8.7 Sababu zilizotolewa na wanafunzi za kutohudhuria masomo . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .32
Jedwali 8.8 Utoro wa walimu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .32
Jedwali 8.9 Mitazamo ya wanafunzi kwa walimu wao . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .32
Jedwali 8.10 Walimu na utoaji wa adhabu ya viboko . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .33

Jedwali 8.11 Walimu kuhimiza wanafunzi kuuliza maswali ....................................33
Jedwali 9.1 Matatizo ya afya na matumizi ya vyandarua kwa mwaka uliopita ....................35
Jedwali 9.2 Matatizo katika huduma za afya ..........................................36
Jedwali 9.3 Matukio ya vifo na majeraha makubwa (kwa marafiki, ndugu, majirani) kutokana na ajali barabarani ..........................................37
Jedwali 9.4 Chanzo cha vifo au majeraha ..........................................37
Jedwali 10.1 Vyanzo vikuu vya maji ya kunywa ..........................................39
Jedwali 10.2 Utaratibu wa kulipia maji ya kunywa ..........................................39
Jedwali 10.3 Mwelekeo wa utoaji wa huduma ya maji ..........................................40
Jedwali 10.4 Matatizo ya utoaji wa huduma ya maji ..........................................40
Jedwali 10.5 Upatikanaji wa maji shuleni ..........................................41
Jedwali 11.1 Vyanzo vikuu vya wazee kujikimu ..........................................43
Jedwali 11.2 Vyanzo vya misaada kwa wazee ..........................................44
Jedwali 11.3 Ulipiaji wa huduma za afya ..........................................44
Jedwali 11.4 Matatizo yanayowakabili wazee katika kupata huduma za tiba ....................45
Jedwali 11.5 Wasiwasi wa wazee kuhusu mustakabali wao ..........................................46
Jedwali 11.6 Karaha ya kuzeeka ..........................................46
Jedwali 12.1 Matatizo makuu katika huduma za jamii mwaka 2003 na 2007 ....................47
Jedwali 13.1 Uanachama katika vyama vya eneo husika ..........................................51
Jedwali 13.2 Aina za ushiriki katika masuala ya umma. ..........................................52
Jedwali 13.3 Maombi ya kupewa taarifa za umma. ..........................................52
Jedwali 13.4 Maoni iwapo ushirikishwaji wa watu huleta mabadiliko. ..........................52
Jedwali 13.5 Maoni kuhusu iwapo wananchi hawana budi kushirikishwa zaidi katika kufanya maamuzi kwenye masuala ya umma ..........................................53
Jedwali 13.6 Vyanzo vya habari kwa maeneo mbalimbali ..........................................53
Jedwali 13.7 Kupata habari mara kwa mara ..........................................54
Jedwali 13.8 Ufahamu wa wananchi kuhusu MKUKUTA ..........................................55
Jedwali 13.9 Maoni ya watu kuhusu kuwa na mfumo wa chama kimoja au vyama vingi vya siasa .....56
Jedwali 13.10 Ushahidi wa uwajibikaji ..........................................56
Jedwali 13.11 Mwelekeo wa uwajibikaji ..........................................56
Jedwali 13.12 Maoni kuhusu kuenea kwa rushwa ..........................................57
Jedwali 13.13 Maoni kuhusu kiwango cha rushwa katika sekta mbalimbali ......................57
Jedwali 13.14 Kukutana na watoa huduma na utoaji wa rushwa ......................................58
Jedwali 13.15 Maoni kuhusu juhudi za serikali ya sasa katika kupambana na rushwa ...............59
Jedwali 14.1 Kiwango cha uaminifu katika jamii ..........................................61
Jedwali 14.2 Makundi yanayoaminika katika jamii ..........................................62
Jedwali 14.3 Maoni kuhusu uhalifu, vurugu na kukosekana kwa usalama ..........................63
Jedwali 14.4 Mwelekeo wa mshikamano na ushirikiano katika jamii ..........................64

# ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| CBOs | Asasi za Kijamii |
| CSOs | Asasi za Kiraia |
| ESRF | Taasisi ya Utafiti wa Kiuchumi na Kijamii |
| FBO | Asasi za Kidini |
| FGDs | Majadiliano katika Vikundi vya Fokasi |
| MKUKUTA | Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania |
| MMS | Mfumo wa Usimamizi wa MKUKUTA |
| MPEE | Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji |
| NGOs | Asasi Zisiso za Serikali |
| PCCB | Taasisi ya Kuzuia na Kuondoa Rushwa |
| PMS | Mfumo wa Usimamizi wa Umaskini |
| PSSS | Utafiti kuhusu Uridhishaji wa Sera na Huduma |
| RAWG | Kikundi cha Utafiti na Uchambuzi |
| REPOA | Taasisi ya Utafiti wa Kupunguza Umaskini |
| TT | Timu ya Kiufundi |
| TWG | Kikundi cha Kiufundi |
| Tz-PPA | Tathmini Shirikishi ya Umaskini Tanzani |
| VoC | Maoni ya Watoto |
| VoP | Maoni ya Watu |

# SHUKRANI

Utafiti huu unaojulikana kama ‘Maoni ya Watu 2007’, unaripoti matokeo ya utafiti mkubwa uliofanyika chini ya Mfumo wa Kusimamia Umaskini ambao ni sehemu ya MKUKUTA (Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini Tanzania). Utafiti pamoja na ripoti yake ulisimamiwa na Kikundi cha Utafiti na Uchambuzi kwa ushirikiano na Kikundi cha Ufundi Mawasiliano cha Mfumo wa Usimamizi wa Umaskini cha MKUKUTA. Wakati mradi huu ukiendelea, Laston Msongole ambaye ni Mkurugenzi wa Kitengo cha Uchumi Mkuu katika Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, alikuwa mwenyekiti wa Kikundi cha Utafiti na Uchambuzi. Anna Mwasha, ambaye ni Mkurugenzi wa Kitengo cha Kuondoa Umaskini katika wizara hiyo hiyo, alikuwa mwenyekiti wa Kikundi cha Ufundi Mawasiliano. Taasisi ya Utafiti wa Kupunguza Umaskini (REPOA), ikiwa ndiyo sekretariet ya Kikundi cha Utafiti na Uchambuzi, iliratibu utafiti na kuandaa ripoti, ikisimamiwa na Joseph Semboja.

Utafiti huu unaohusisha Watanzania 7,879 ni mkubwa kuliko tafiti zote za maoni ya wananchi zilizowahi kufanywa Tanzania Bara. Pia ni wa kipekee kwa jinsi ulivyojumuisha wahusika wa umri mbalimbali kuanzia miaka 7 hadi 90. Maoni ya wananchi kuhusu maendeleo yao yanatoa taarifa muhimu kwa ajili ya kupanga mipango na kuunda sera, pia kwa matumizi ya wadau kama vile taasisi za kijamii, watafiti na wahisani. Kwa hiyo ni muhimu taarifa hizi zikatufikia sisi sote ili tuendeleze mijadala inayoeleweka kwa maendeleo ya taifa letu.

Wasomaji wa ripoti hii wanaelekezwa pia kurejea ripoti ya ‘Umaskini na Maendeleo ya Watu 2007’ na ‘Maoni ya Watoto 2007’ – machapisho haya matatu kwa pamoja yanatoa ‘picha’ kamili ya Tanzania ya leo. Serikali inadhamiria kuendeleza mfululizo huu wa tafiti ili kufanya maamuzi yanayoeleweka na kuboresha mijadala ya wazi juu ya masuala muhimu ya maendeleo.

Watu wengi waliochangia utafiti huu pamoja na ripoti iliyotokana nayo, michango yao imepokelewa kwa shukrani. Wale waliofanya kazi katika ngazi mbalimbali za kuandaa utafiti wa ‘Maoni ya Watu’, ukusanyaji wa data, na hatimaye uchambuzi wake na uandishi wa ripoti ni pamoja na: Servus Sagday, Alana Albee, Brian Cooksey, Rose Mwaipopo, Flora Kessy, Blandina Kilama, Cornel Jahari, Jamal Msami, Dennis Rweyemamu, Lucas Katera na Valerie Leach.

Utayari wa wahojiwa pamoja na wajumbe wa kikundi cha fokasi kushiriki katika utafiti huu kumepokewa kwa moyo mkunjufu.

# MUHTASARI

Ripoti hii inawasilisha matokeo ya utafiti wa Maoni ya Watu kuhusu taarifa za vipengele mbalimbali vya maisha ya watu, ikiwa ni pamoja na maendeleo yao ya kiuchumi ya hivi karibuni, mabadiliko ya hali zao kimaisha, na ubora na upatikanaji wa huduma za kijamii na kiuchumi (kama vile upanuzi wa kilimo na ukarabati na utunzaji wa barabara). Utafiti huu pia ulichambua maoni ya watu kuhusu mwelekeo wa shughuli za utawala ikiwa ni pamoja na ushiriki wa wananchi katika masuala ya umma, utungaji sera, na masuala ya rushwa na uaminifu katika jamii.

Utafiti huu ulifanywa mnamo mwezi Machi na Aprili 2007, ukiwashirikisha Watanzania 7,879 wenye umri wa miaka 7 hadi 90 katika mikoa kumi ya Tanzania Bara. Sampuli ya watu walioshiriki katika utafiti huu ilihusisha watoto 512, vijana 1,525, watu wazima 4,987 na wazee 855. Sampuli nyingine ndogo ina takriban watu 1,000 walioshiriki katika utafiti huu kupitia makundi maalumu ya watu yaliyoendesha mijadala ya kina kuhusu hoja mbalimbali. Kwa watoto, utafiti huu ulilenga kuchunguza masuala ya shule, nafasi yao katika jamii na matarajio yao ya baadaye. Kwa vijana, masuala muhimu yalikuwa elimu, maoni yao kuhusu sera, ajira, matatizo binafsi, na matarajio yao ya baadaye. Kwa wazee, lengo kuu la utafiti huu lilihusu ubora na upatikanaji wa huduma zinazohusu ustawi wao na njia zao za kujipatia riziki.

Kama zilivyo tafiti nyingi zinazochunguza maoni ya watu, utafiti huu pia ulikusanya maoni ya watu kuhusu utendaji wa taasisi za umma na wadau mbalimbali. Ingawa jambo hili ni la muhimu, ni muhimu vilevile kubainisha kuwa tafiti za maoni ya watu zinaweza kutoa matokeo tofauti na yale ya tafiti zilizozoeleka za kaya hadi kaya, kwani tafiti za maoni ya watu zina mipaka kuhusu aina ya maswali yanayoweza kutumiwa kwa ajili ya kukusanya takwimu za utafiti na vilevile kuhusu kiwango kinachowezekana cha uchambuzi wa takwimu katika mchakato huo. Hata hivyo, kumejitokeza hali ya kufanana kwa maoni ya watu kuhusu maendeleo ya kiuchumi ya hivi karibuni, mabadiliko katika hali za maisha ya watu, ubora na upatikanaji wa huduma za kiuchumi na kijamii, na shughuli za utawala (ikiwa ni pamoja na ushiriki wa wananchi katika masuala ya umma, utungaji sera, masuala ya rushwa na uaminifu katika jamii).

Utafiti huu ulileta taarifa kuhusu viashirio maalumu vya mfumo wa usimamizi wa MKUKUTA. Utafiti ulichambua maoni ya watu kuhusu maendeleo kwa kutumia viashirio vilivyoteuliwa kutoka katika makundi matatu ya MKUKUTA, ambayo hushughulikia: kukuza uchumi na kupunguza umaskini wa kipato, maisha bora na ustawi wa jamii, na utawala bora na uwajibikaji. Hivyo basi, utafiti huu unaarifu jinsi watu wanavyotambua na kuchambua mabadiliko ya sera na jinsi sera zinavyochukuliwa katika suala la kubadili hali ya maisha ya watu.

## Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini wa Kipato

Kwa ujumla, Watanzania wachache mno wenye umri wa utu uzima ndio wanaoona kuwa wanafaidi matunda ya kukua kwa uchumi kulinganisha na wale wanaoona kuwa riziki zao zinazidi kuwa duni. Wakati 24% ya watu wazima waliosailiwa walieleza kuwepo kwa maendeleo katika shughuli zao za kiuchumi kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita, 26% walisema hakukuwa na mabadiliko, na nusu (50%) ya wakazi hao wa mijini na vijijini walieleza kuwepo kwa hali kuzidi kuzorota. Karibu 32% ya vijana waliosailiwa wanadai kulikuwa na kuzorota kwa shughuli zao kiuchumi katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, huku 39% wakiwa hawaoni mabadiliko, na 26% wakiona kuwepo kwa mabadiliko. Hakukuwa na tofauti katika majibu yaliyotolewa na vijana wa kike na wa kiume.

Matokeo makuu ya utafiti huu kuhusu kukuza uchumi na kupunguza umaskini wa kipato yanazungumzia hali ya miundombinu ya kiuchumi na upatikanaji wa fursa za ajira, gharama za maisha (gharama za chakula na mahitaji mengine ya msingi) na masuala mengine maalumu yanayohusu upatikanaji wa nyenzo mbalimbali kwa shughuli za kiuchumi.

## Miundombinu ya Kiuchumi

### Barabara

Kwa wananchi waliosailiwa katika maeneo ya vijijini, hali ya ubovu wa barabara na kutozifanyia matengenezo ni tatizo kuu. 70% ya washiriki hao wa vijijini huchukulia hali ya ubovu wa barabara kuwa ni 'tatizo kuu,' 47% wakidai kuwa hali ilizidi kuwa mbaya katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, huku 26% wakisema hakukuwa na mabadiliko na 28% wakisema kulikuwa na mabadiliko. 57% ya wakazi wa mijini, isipokuwa Dar es Salaam, na 41% ya wakazi wa Dar es Salaam walidai kuwa ubovu wa barabara ni tatizo kuu.

Kuboreshwa kwa hali ya barabara ni suala lililojadiliwa na 56% ya washiriki wa Dar es Salaam na 42% ya washiriki wa miji mingine. Nusu ya washiriki wa vijijini walibainisha kuwa barabara mbovu huwazuia kuyafikia masoko na huduma nyingine mijini, hivyo kutokana na ubovu wa barabara za vijijini, maendeleo ya kiuchumi katika maeneo ya vijijini hudumaa.

### Mawasiliano ya Simu

Umiliki wa simu za mkononi umeongezeka zaidi ya mara nne katika kipindi kisichozidi miaka minne, hali ambayo imesaidia kuboresha mawasiliano. 35% ya washiriki wenye umri wa utu uzima walimiliki simu za mkononi: 65% wakiwa wa Dar es Salaam na 16% wakiwa wa vijijini. Jijini Dar es Salaam, 17% ya washiriki maskini zaidi humiliki simu za mkononi, ikilinganishwa na 86% ya washiriki wenye nafuu kimaisha. Hata hivyo, kuboreka kwa mawasiliano ya simu kunaweza kuwa hakujachangia vya kutosha kuinua hali ya uchumi, kwani karibu 75% ya wamiliki wa simu nchini kote walisema kuwa hutumia simu zao kwa shughuli binafsi, na 25% tu ndio waliosema kuwa huzitumia kwa shughuli za kibiashara.

### Nishati

Chanzo kikuu cha nishati inayotumiwa na washiriki walio wengi katika kupika ni kuni na mkaa - 60% ya washiriki hutumia nishati ya kuni na 35% hutumia mkaa. Matumizi ya mkaa yalitajwa zaidi jijini Dar es Salaam, ambako hutumiwa na 83% ya washiriki. Nishati ya kuni hutumiwa na 87% ya washiriki wa vijijini na 57% ya washiriki wa mijini isipokuwa Dar es Salaam.

Kwa ujumla, umeme ulitumiwa kama chanzo cha mwanga majumbani na 23% tu ya washiriki. Nishati hii ilitumiwa zaidi katika maeneo ya mijini nchini Tanzania - ilitumiwa na 59% ya washiriki wa Dar es Salaam, ikilinganishwa na 43% katika miji mingine na 11% ya washiriki wa vijijini.

### Hali ya Uchumi

Maoni ya watu kuhusu hali yao kiuchumi yalitathminiwa kwa kutumia vigezo kadhaa ambavyo ni pamoja na ajira na njia nyingine za kujipatia riziki, upatikanaji na gharama za ununuzi wa nyenzo za uzalishaji mali na upatikanaji na gharama za ununuzi wa chakula na mahitaji mengine ya msingi. Wakati gharama za maisha - gharama za ununuzi wa chakula na mahitaji ya msingi - zilitajwa kuwa ni tatizo kuu na 67% ya watu wazima, tatizo ambalo huathiri watu wa mijini na vijijini, 47% walisema kamwe hawakukumbwa na tatizo la upungufu wa chakula mwaka uliopita na 63% walisema walikula milo mitatu kwa siku. Karibu 47% ya vijana nao walidai kuwa gharama za ununuzi wa chakula na bidhaa nyingine za msingi ni tatizo kuu. Ingawa watu maskini walikuwa na wasiwasi zaidi kuhusu bei ya chakula na bidhaa nyingine za msingi kuliko watu wenye nafuu kimaisha, karibu 66% ya washiriki wenye hali bora kimaisha nao pia waliliona suala la kupanda kwa gharama za maisha kuwa tatizo kuu. Wakazi wa mijini walisema kuwa walikula nyama au samaki karibu siku tatu kwa wiki ikilinganishwa na washiriki wa vijijini ambao wastani wao ni chini ya siku mbili kwa wiki.

Robo tatu ya washiriki wa Dar es Salaam (78%) walikula milo mitatu kwa siku, ikilinganishwa na theluthi mbili (64%) ya washiriki kutoka miji mingine na 55% tu ya wale wa vijijini. Walipoulizwa iwapo walikumbwa na njaa katika kipindi cha mwaka uliopita, 19% ya wanavijiji walijibu 'mara kwa mara' na wengine 43% walijibu 'wakati mwingine.' Theluthi moja ya washiriki wa Dar es Salaam (32%) nao walisema 'wakati mwingine' walikumbwa na njaa, na 5% walisema 'mara kwa mara.'

Karibu 87% ya washiriki wa vijijini hujishughulisha na kilimo na ufugaji na uvuvi. 52% walisema kuwa hali yao kiuchumi ilikuwa duni kuliko ilivyokuwa miaka mitatu iliyopita, 25% walisema ilikuwa vilevile na 23% walisema imeboreka. Kwa ujumla, hali duni ya uzalishaji katika kilimo kutokana na matumizi madogo ya pembejeo na zana za kilimo ni jambo lililo dhahiri. Karibu 86% ya wakulima wote waliosailiwa hawakutumia mbolea ya kemikali mwaka uliopita, 72% hawakutumia madawa ya kemikali ya kuua wadudu waharibifu, ama sumu ya mimea, na 77% hawakutumia mbegu zilizoboreshwa. Asilimia ya wakulima maskini zaidi ambao hawakutumia mbolea ya kemikali ilikuwa 98.

Zaidi ya 70% ya wakulima walibainisha kuwa bei, upatikanaji, kufaa/ubora wa mbolea na pembejeo nyinginezo ni kikwazo kikubwa zaidi katika shughuli za uzalishaji wa kilimo. Walipoulizwa kuwa serikali inatakiwa kufanya nini ili kuwasaidia wakulima, 42% walitaja kuboreshwa kwa hali ya upatikanaji wa pembejeo na 19% walitaka wapatiwe mikopo. Kulikuwa na tofauti ndogo sana katika majibu yaliyotolewa na wakulima maskini sana na wale wenye nafuu kimaisha.

Wafugaji wengi, 78% waliosailiwa walilalamikia pia gharama za ununuzi wa madawa ya mifugo na 63% walilalamikia kutopatikana kwa huduma za mifugo. Ukame, magonjwa, umbali wa kuyafikia masoko, bei ndogo ya mifugo yao katika masoko, ukosefu wa maeneo ya malisho na ukosefu wa taarifa za masoko yalitajwa pia kuwa ni matatizo makuu na washiriki walio wengi. 40% ya washiriki ambao ni wafugaji walipata ushauri wa kitaalamu katika kipindi cha mwaka uliopita, kiwango ambacho ni cha juu zaidi cha kupata ushauri wa kitaalamu ikilinganishwa na kile walichokipata wakulima. Nusu ya wafugaji waliosailiwa katika utafiti huu walisema hawajawahi kamwe kupata ushauri wa kitaalamu. Wafugaji walio wengi, 76%, walikuwa na maoni kwamba serikali haikuwa ikijishughulisha kwa namna yoyote zaidi ya hiyo. Kuna wachache sana waliosema kuwa serikali ilikuwa ikitoa huduma za ushauri wa kitaalamu, hali inayoonyesha kuwa pengine huduma hizo zilipatikana kwa kiasi kikubwa kutoka kwa wataalamu binafsi. Kuboreshwa kwa hali ya upatikanaji wa chanjo na madawa ya mifugo ni ombi moja na la muhimu zaidi lililotolewa kwa serikali na wafugaji hao.

70% ya wavuvi waliosailiwa walidai kuwa upatikanaji wa samaki ulikuwa ukipungua, huku 16% tu ndio wakisema kuwa upatikanaji wa samaki ulikuwa ukiongezeka. Walipoulizwa ni kwa nini walidhani upatikanaji wa samaki ulizidi kupungua, theluthi moja walisema kulikuwa na wavuvi wadogowadogo wengi kupita kiasi, na kwamba wavuvi hutumia nyavu zenye matundu madogo mno. Karibu 20% ya wale waliosailiwa walitaja pia uvuvi wa kibiashara, ujio wa wavuvi kutoka maeneo mengine, na matumizi ya baruti kama sababu za kushuka kwa mavuno ya wavuvi. Walipoulizwa iwapo wanaweza kunufaika zaidi kwa kuuza samaki nje ya nchi badala ya kuuza katika masoko ya hapa nchini pekee, zaidi ya nusu (53%) walipendelea kuuza nje, ikilinganishwa na 38% waliosema kuwa watanufaika zaidi kwa kuuza katika masoko ya ndani.

Kwa washiriki wa mijini, upatikanaji wa kazi uliripotiwa mara nyingi zaidi kuwa tatizo kubwa kuliko walivyoripoti washiriki wa vijijini. Wakati upatikanaji wa kazi ulikuwa tatizo kuu kwa 55% ya watu wazima waliosailiwa katika maeneo ya mijini, tatizo hili liliripotiwa na 39% ya watu wazima wa maeneo ya vijijini. Tatizo hili ni kubwa zaidi kwa vijana wa mijini na vijijini: 63% ya vijana wote waliosailiwa (65% wakiwa wa mijini, na 61% wakiwa wa vijijini) walichukulia kuwa hili ndilo tatizo kubwa zaidi linalowakabili.

Utafiti huu uliangalia pia njia za kujipatia riziki kwa mtu mmoja mmoja katika hatua mbalimbali za maisha. Miongoni mwa vijana wenye umri wa miaka 15 hadi 24 waliokuwa tayari wamemaliza shule, 35% hawakuwa na ajira / shughuli ya uzalishaji mali, huku 26% walifanya kazi za vijijini na 11% walikuwa wamejiajiri. Karibu 40% ya vijana walisema kuwa walitarajia kuendelea na masomo yao. Kwa ujumla, hapakuwa na tofauti kubwa sana ya maoni kati ya vijana wa kike na wa kiume. Kwa ujumla, vijana wote wa kike na wa kiume walikuwa na matarajio makubwa kwa maisha yao ya baadaye. Walipoulizwa iwapo wanatarajia hali yao kiuchumi kubadilika katika miaka mitatu ijayo, karibu nusu yao walisema itaimarika, 13% ya vijana wa kiume na 38% ya vijana wa kike walisema itabaki vilevile, na 23-30% walisema hawajui.

Wakati wengi wa watu wenye umri wa zaidi ya miaka 60, hususan wanawake, hutegemea ndugu zao wa karibu katika kujikimu kwao, 34% ya wanaume na 20% ya wanawake waliarifu kuwa walikuwa bado wanafanya kazi za kudumu. Takriban 40% ya wazee waliosailiwa walisema walikuwa wakiwalea wajukuu wao, hususan kutokana na kufariki au kuugua kwa wazazi wa watoto hao. Katika kuwalea wajukuu wao, karibu robo tatu walisema kuwa walisaidiwa na ndugu zao wa karibu.

Karibu wazee wote (88%) walisema kuwa ndugu zao wa karibu wanaweza kuwasaidia wakifikwa na tatizo kubwa. Hata hivyo, 75% ya wazee huhofia zaidi kupoteza nguvu za kufanya kazi kwa kadri wanavyozidi kuzeeka, 66% huhofia kukumbwa na njaa na umaskini, na kupoteza uhuru wao shauri ya maradhi. Mashaka haya yanajitokeza sana miongoni mwa wazee wanaume na wazee wanawake.

## Maisha Bora na Ustawi wa Jamii

### Elimu

Wanafunzi na wazazi waliombwa kutathmini hali ya elimu. Karibu 60% ya washiriki walitaja kuwepo kwa ongezeko la vyumba vya madarasa ya shule za msingi, huku washiriki wengi zaidi wa mijini wakibainisha kuwepo kwa mabadiliko kuliko wale wa vijijini. Zaidi ya nusu ya watu hao waliosailiwa walisema pia kuwa vyumba vya madarasa ya shule za sekondari vilitosheleza, ingawa majibu yao yalionyesha kuwepo kwa hali bora zaidi mijini kuliko vijijini. Hata hivyo, uhaba wa vyumba vya madarasa kwa shule za msingi na sekondari uliripotiwa na 22% ya watu waliosailiwa, hali inayoonyesha kuwa baadhi ya shule bado hazina vifaa vya kutosha kwa ajili ya utoaji elimu. Suala la utengenezaji wa madawati lilifanana kama ya ujenzi wa vyumba vya madarasa, ambapo upungufu zaidi uliripotiwa vijijini na katika shule za msingi ikilinganishwa na hali ilivyo mijini na katika shule za sekondari.

Mabadiliko mengine muhimu yalihusu mazingira ya vyumba vya madarasa, na ushiriki wa wanafunzi na walimu katika kazi za darasani. Takriban 54% ya waliohojiwa waliona kuwepo kwa mabadiliko katika hali ya vyumba vya madarasa, huku 34% wakisema hakukuwa na mabadiliko yoyote. Asilimia 60 ya wanafunzi wa shule ya msingi, waliona kuwepo kwa mabadiliko katika mazingira ya vyumba vya madarasa, ikilinganishwa na 48% ya wanafunzi wa shule ya sekondari.

Idadi kubwa zaidi ya wanafunzi wa shule ya msingi na sekondari walioshiriki katika utafiti huu walisema kuwa baadhi au wengi wa walimu wao waliwahimiza kuuliza maswali darasani. Idadi ya wasichana waliosema kuwa walimu waliwahimiza kuuliza maswali ilikuwa ni ndogo zaidi kuliko ya wavulana. Baadhi ya walimu kutohudhuria vipindi ni tatizo lililoripotiwa katika shule 18 kati ya 20 zilizofanyiwa utafiti. Hata hivyo, 59% ya wanafunzi walisema 'kamwe walimu hawakuwa watoro au hali hiyo ilitokea kwa nadra tu.' Kiwango cha utoro kilionekana kuwa juu zaidi vijijini kuliko mijini. Tofauti ya viwango vya utoro kwa kutumia kigezo cha jinsia au kwa kulinganisha shule za msingi na sekondari haikuonekana kuwa kubwa.

Vitabu vya kiada ni pungufu zaidi vijijini kuliko mijini, lakini hata jijini Dar es Salaam, 61% ya wale waliosailiwa hawakuridhishwa na hali ya ugavi wa vitabu vya kiada. Karibu 80% ya watoto waliosailiwa wenye umri wa kati ya miaka 7 na 14 walisema kuwa hakukuwa na vitabu vya kutosha, huku 15% tu ndiyo wakisema kuwa vilikuwepo vya kutosha. Karibu 66% ya wanafunzi wa madarasa ya juu ya elimu ya msingi na sekondari walisema vitabu vya kiada vilikuwa vichache mno na 16% ya wavulana na 19% ya wasichana wa shule za sekondari walidai kuwa walisoma masomo yao bila kutumia vitabu.

Adhabu ya viboko, au hofu ya adhabu hiyo, ni tatizo kubwa kwa watoto wa shule wenye umri mdogo zaidi kwenye shule 18 kati ya 20 zilizofanyiwa utafiti ili kujua matatizo ya watoto. Kwa wanafunzi wakubwa wa shule za msingi na sekondari, 20% tu ndio hawakuitaja adhabu ya viboko. Katika shule 16 zilizofanyiwa utafiti, walimu 'wote au walio wengi' waliripotiwa kutumia adhabu ya viboko kwa wanafunzi wao, zaidi katika shule za vijijini kuliko za mijini.

Watoto waliarifu kuwa huwa hawakosi kuhudhuria masomo shuleni. Zaidi ya 70% walisema kuwa kamwe hawakosi shule au hukosa kwa nadra sana, na 20% tu walisema kuwa wakati mwingine hukosa kwenda shule. Katika shule za msingi na sekondari, kwa kiasi kikubwa sana ugonjwa ndiyo sababu kuu ya wanafunzi kutohudhuria shule, takriban 61%, huku kukiwa na idadi kubwa zaidi vijijini kuliko mijini. Gharama za elimu / ukosefu wa fedha za ada ya shule, zilitajwa na 36% ya wanafunzi kuwa sababu ya kutohudhuria masomo kwa shule za msingi na sekondari. Kuhudhuria harusi au mazishi huwachukulia pia wanafunzi muda wao, kukiwa kumetajwa na 41% ya wasichana wa shule ya sekondari na 31% ya wavulana.

Matumizi ya kompyuta shuleni yalitajwa kuwepo kwa kiwango kidogo sana, hata katika shule za sekondari. Zaidi ya nusu ya shule za sekondari zilizofanyiwa utafiti, 55%, hazikuwa na kompyuta, na kwa shule zenye kompyuta, nyenzo hizo zilikusudiwa zaidi kwa shughuli za kiutawala na si kwa ajili ya kutumiwa na wanafunzi.

**Huduma za Afya**

Utafiti huu ulitafuta taarifa kuhusu hali ya jumla ya afya za watu na maoni yao kuhusu upatikanaji, ubora na gharama za huduma za afya zinazotolewa na serikali, na iwapo huzifikia huduma hizi. 66% ya watu wazima waliosailiwa waliarifu kuwa waliugua malaria katika kipindi cha mwaka uliopita; wakati 60% waliugua kikohozi, homa na mafua, na 32% walishikwa na ugonjwa wa kuhara mara moja au zaidi. Ugonjwa wa malaria uliripotiwa zaidi jijini Dar es Salaam, huku ugonjwa wa kuhara ukitokea zaidi katika maeneo ya vijijini. Takriban robo tatu, 73%, ya wananchi waliosailiwa waliarifu kuwa walitumia vyandarua, vingi kati ya hivyo vikidaiwa kuwekewa dawa. Kiwango cha matumizi ya vyandarua kilikuwa juu zaidi mijini kuliko vijijini.

Walipoulizwa kuhusu mambo muhimu zaidi ya kuangaliwa katika huduma za afya, 32% ya watu wazima waliosailiwa walitaja suala la ubora / upatikanaji wa huduma, 16% walitaja umbali, 13% walitaja upatikanaji wa madawa na 10% walitaja gharama zake. Zaidi ya robo ya watu waliosailiwa hawakuwa na jibu lolote kwa swali hili.

Kwa watu wazima walioarifu kuwa hutumia huduma za afya, 62% walisema kuwa gharama kubwa za matibabu na ununuzi wa madawa lilikuwa tatizo kubwa. Upatikanaji wa madawa na muda mrefu wa kusubiri huduma yalitajwa pia, hususan na wakazi wengi wa mijini, kuwa ni matatizo makuu. Wananchi wachache tu walilalamikia tabia ya upole wa wahudumu wa afya, ukosefu wa huduma za uzazi na chanjo, na suala la usafi katika utoaji huduma.

Miongoni mwa wazee, karibu 65% walisema walikuwa na matatizo ya afya yanayohitaji uangalizi wa mara kwa mara, mengi kati ya matatizo hayo yakihusiana na utembeaji wao na kwa idadi kubwa kidogo yakiwakumba zaidi wanawake kuliko wanaume. Karibu 66% ya wazee walitafuta huduma za tiba katika kipindi cha miezi mitatu kabla ya utafiti huu, 70% wakiwa wazee wanawake na 60% wazee wanaume. Kwa waliotafuta tiba, 35% walijilipia wenyewe, 27% walilipiwa na familia zao, 15% walipata tiba bure, na 14% hawakupata tiba. Karibu nusu ya watu wenye umri wa zaidi ya miaka 60 (48%) walikiri kutofahamu kuwa wanayo haki ya kupata tiba bure katika hospitali za serikali, 42% wakiwa wanaume na 58% wanawake. Takriban moja ya tano, 18%, ya wazee waliosailiwa walisema kuwa walinyimwa huduma za tiba kwenye hospitali za serikali kwa sababu hawakuwa na uwezo wa kulipia huduma hizo, na 13% walidai kuwa walinyimwa huduma za bure za tiba kwa kushindwa kuthibitisha umri wao.

Watoto wadogo wa shule walioshiriki katika utafiti huu waliarifu kuwa hufundishwa masuala ya afya kama sehemu ya mtaala, lakini shule zao hazina uwezo wa kuwapatia mambo mbalimbali yahusuyo tiba ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi. Nusu ya shule zilizokuwa katika sampuli ya utafiti huu ndizo zilizokuwa na namna fulani ya tiba inayoweza kuitwa huduma ya kwanza. Katika shule nyingine, mwanafunzi anapougua hupelekwa kwenye hospitali au zahanati ya karibu.

Lishe na mpangilio wa ulaji hujulikana kwa kuathiri ufanisi wa watoto shuleni. Licha ya ukweli huo, idadi kubwa zaidi ya wanafunzi, 85%, hula wanaporudi nyumbani kutoka shuleni. Shule tatu tu kati ya ishirini zilizokuwa kwenye sampuli ya utafiti ndizo zina utaratibu wa kuwapa watoto chakula - moja ikiwa na watoto wa wazazi wenye kipato cha juu na nyingine mbili zikiwa na watoto wa wazazi wenye kipato cha kati - na hata katika shule hizi mbili, taarifa zilionyesha kuwa utaratibu huo ulikuwa umesitishwa wakati utafiti huu ukifanywa. Katika shule nyingine mbili (moja ya Arusha na nyingine ya Dar es Salaam), chakula huuzwa kwenye maduka yaliyo jirani na shule. Walipoulizwa kuhusu mpangilio wao wa ulaji, karibu 30% tu ya wanafunzi wa kundi la umri wa miaka 15 na kuendelea walioshiriki katika utafiti ndio waliosema kuwa kila mara hula kabla ya kwenda shule, idadi hiyo ikianzia 26% kwa wanafunzi wa vijijini hadi 48% kwa Dar es Salaam. Vilevile idadi ndogo ya wanafunzi, 15%, walisema hula vyakula vidogovidogo wakati wa mapumziko shuleni.

### Maji

Kati ya 80% na 90% ya watu wazima waliosailiwa hupata maji ya kunywa kutoka kwenye vyanzo vinavyomilikiwa na jamii au na majirani. Wakati 73% ya watu wazima vijijini hawalipii maji wanayoyatumia - na 8% tu ya washiriki wa Dar es Salaam ndiyo wanaopata maji bure - 77% hulipia huduma hiyo kwa watu binafsi (watu wenye pampu, vibanda, majirani au wachuuzi wa maji). 13% tu ndiyo walioandikishwa kwa huduma hiyo na mamlaka ya maji (DAWASCO).

Kwa kipindi cha mwaka mmoja kabla ya utafiti huu, tatizo lililotajwa zaidi kuhusu upatikanaji wa maji ni kuwepo kwa hali ya ukame. Watu wengi waliosailiwa walishuhudia kupungua badala ya kuongezeka kwa huduma ya maji, usafi wake, kupanda kwa gharama na kuwepo kwa foleni ndefu kupata huduma hiyo. Kuwepo kwa maji machafu lilikuwa tatizo kubwa zaidi vijijini, na gharama kubwa na foleni ndefu kwa Dar es Salaam.

Shule za msingi mbili tu kati ya ishirini zilizofanyiwa utafiti ndizo zilizokuwa na maji ya kunywa ya bomba kwa ajili ya watoto. Jijini Dar es Salaam, watoto walibeba maji yao ya kunywa kutoka makwao au walinunua kwenye vibanda vya karibu na shule. Mkoani Mtwara, watoto walipata maji wakati pale tu walipokwenda nyumbani wakati wa mapumziko au wakati wa chakula cha mchana. Karibu 44% ya vijana wote wa shule waliosailiwa waliarifu kutokuwepo kabisa kwa huduma ya maji shuleni kwao, na 64% ya wanafunzi wa vijijini waliarifu kutokuwepo kwa huduma ya maji shuleni.

## Utawala Bora na Uwajibikaji

Vigezo vilivyotumiwa na utafiti huu wa Maoni ya Watu ili kupima mtazamo wa watu kuhusu masuala ya utawala bora na uwajibikaji vinajumuisha ushiriki wa wananchi katika masuala ya umma, juhudi za kuwafanya viongozi wa serikali kuwajibika, kuwepo kwa mfumo unaofaa katika kupata habari na kufanya mawasiliano, ufahamu na maoni ya watu kuhusu siasa na sera, rushwa na uwajibikaji, jamii, uaminifu, ushirikiano na usalama, na utambulisho wa kiutamaduni wa taifa.

### Ushiriki katika Masuala ya Umma

Zaidi ya moja ya tano, 22%, ya washiriki vijijini walisema kuwa walishiriki katika zoezi la kubuni mipango ya maendeleo katika maeneo yao, na 16% walifanya kazi kwenye miradi ya umma, hususan ujenzi na ukarabati wa barabara. Viwango vya ushiriki viliripotiwa kulingana kwa washiriki kutoka maeneo ya mijini isipokuwa Dar es Salaam (18% kwa miji mingine na 13% kwa Dar es Salaam). Washiriki wachache zaidi wa Dar es Salaam waliarifu kuwepo kwa ushiriki kama huo (7% na 6%). Hali kadhalika, watu wazima wachache wa mijini na vijijini, 9%, walihudhuria vikao vikuu vya baraza katika maeneo yao.

Zaidi ya hayo, 15% ya washiriki walionyesha kuwa waliomba taarifa kutoka ngazi ya serikali zao za vijiji / mitaa katika kipindi cha mwaka mmoja kabla utafiti huu haujafanyika, wakati huo theluthi mbili ya maombi haya yalikubaliwa. Wakazi wa vijijini wanaonekana kuwa makini zaidi katika kutafuta taarifa kutoka kwenye ofisi za serikali, ambapo 20% ya wakazi waliosailiwa waliomba kupatiwa taarifa, ikilinganishwa na 10% kwa wale wa Dar es Salaam.

Katika maeneo yote ambayo utafiti ulifanyika, zaidi ya nusu ya waliosailiwa, 53%, (bila kuzingatia iwapo aliyesailiwa ni mkazi wa mjini au kijijini), walikuwa na mtazamo kwamba wananchi wanaoeleza maoni yao mbele ya hadhara huleta mabadiliko, huku 39% walikuwa na matazamo kwamba viongozi wa serikali hawasikilizi yale yanayosemwa na watu.

**Juhudi za Kuwafanya Viongozi wa Serikali Kuwajibika**

Utafiti huu ulichunguza iwapo Watanzania wanaona kama kuna hatua za maendeleo katika juhudi za kuwafanya viongozi wa serikali kuwajibika zaidi. Washiriki waliulizwa iwapo kulikuwa na matukio yoyote katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita yaliyohusisha viongozi wa serikali kuu au serikali za mitaa ambayo kwao yanaashiria kuboreshwa kwa utoaji huduma na uwajibikaji. Zaidi ya 30% ya washiriki walithibitisha kuwepo kwa hali hiyo, huku kukiwa na tofauti ndogo sana ya maoni kati ya washiriki wa mijini na vijijini. Kwa kiasi kikubwa sana, majibu yaliyotolewa na watu walio wengi - takriban 56% ya washiriki - yalihusu kuboreshwa kwa shule, vyumba vya madarasa na nyumba za walimu.

Kama uthibitisho wa kuwepo kwa uwajibikaji, 32% ya washiriki walisema kuwa walishuhudia viongozi wa serikali wakituhumiwa kwa kufuja rasilimali za umma na viongozi kufukuzwa kazi kwa rushwa na uzembe kazini.

**Habari na Mawasiliano**

Redio ni chanzo muhimu zaidi cha habari nchini kote, na zaidi hasa katika maeneo ya mijini kuliko ya vijijini. Magazeti na televisheni ni vyanzo muhimu mno vya habari jijini Dar es Salaam kuliko kwingineko nchini. Washiriki wachache sana wa vijijini (6%) ndio wanaoweza kuvipata. 'Taarifa za kuambiwa' ni chanzo muhimu cha habari kwa karibu 20% ya watu waliosailiwa mijini na vijijini. Makanisa na misikiti iliripotiwa na watu wachache (7%) kuwa vyanzo vya habari. Kwa ujumla, wananchi wa Dar es Salaam wana wigo mpana zaidi wa kupata habari kuliko wengine.

**Ufahamu na Maoni ya Watu kuhusu Siasa na Sera**

Maoni yalitafutwa pia kuhusu masuala yanayohusiana na sera chache maalumu zilizoteuliwa, lengo likiwa kuchunguza kiwango cha ufahamu walicho nacho watu kuhusu mijadala ya siku za karibuni inayozungumzia sera na iwapo watu huifuatilia mijadala hiyo. Karibu theluthi moja ya watu wazima waliosailiwa walisema hawapendi sana au hawapendi hata kidogo kufuatilia mambo ya kisiasa au kiuchumi. Karibu nusu ya watu wazima hawakuweza kusema chochote iwapo makampuni ya uchimbaji madini yalikuwa yanalipa kodi ya kutosha, wala kuhusu kitu kilichosababisha kuwepo kwa tatizo kubwa la umeme mwaka 2006, au kuhusu faida na hasara za kuwahamisha *wamachinga* (wafanyabiashara wadogowadogo) kutoka kwenye maeneo ya katikati ya miji kwenda maeneo mengine. Kati ya nusu ya watu waliotoa maoni yao, karibu wote (96%) walisema kuwa makampuni ya madini hayana budi kulipa kodi kubwa zaidi; 74% wanaamini kuwa tatizo la umeme lilisababishwa na ukame, huku maoni yakitofautiana kuhusu suala la *wamachinga* - 58% wakiunga mkono sera ya kuwahamisha, na 34% wakiikosoa hatua hiyo ya serikali, wengine hawakuwa na maoni yoyote.

Washiriki waliombwa pia kutoa maoni yao iwapo misaada kutoka nchi za nje hunufaisha viongozi wa serikali au watu maskini. Kati ya 86% ya washiriki waliotoa maoni yao, 81% waliamini kuwa 'kwa kiasi kikubwa, misaada kutoka nchi za nje hunufaisha viongozi wa serikali,' na 64% ya waliosailiwa walikubaliana sana na mtazamo huu.

Maswali kadhaa yaliulizwa katika jitihada za kutathmini maoni ya wananchi kuhusu utendaji wa wanasiasa na viongozi wa serikali. Washiriki walio wengi walitoa maoni yanayounga mkono sana utendaji wa Rais, 77%, na wa Waziri Mkuu, 72%. Jeshi la Polisi lilipongezwa zaidi kuliko kukosolewa kwani 17% tu ya waliosailiwa ndio walioona kuwepo kwa utendaji duni zaidi katika Jeshi la Polisi.

**Rushwa na Uwajibikaji**

Karibu 40% ya watu wazima waliosailiwa hawakuwa na maoni yoyote kuhusu kiwango cha rushwa kilichopo katika jamii. Kwa wale waliotoa maoni yao, idadi sawa na hiyo walisema kuwa rushwa ndogo, kubwa, na ya kisiasa ni jambo la 'kawaida sana' (50%) au 'kawaida' (karibu 20%) nchini Tanzania.

Vilevile, karibu 43% ya wananchi waliosailiwa walikuwa na mtazamo kuwa rushwa huathiri maisha yao, shughuli zao na siasa. 8% tu ya washiriki ndio walioamini kuwa rushwa haiathiri maeneo haya matatu. Idadi kubwa ya watu waliosailiwa (karibu 40%) hawakuwa na maoni yoyote; hivyo basi, idadi kubwa ya waliotoa maoni yao walikuwa na mtazamo kuwa maisha yao, biashara zao na siasa huathiriwa na rushwa. Hata hivyo, inawezekana kwamba wengi wa wale ambao hawakuwa na maoni wanaweza kuwa hawajaathiriwa na rushwa. Idadi karibu sawa na hiyo, 38%, hawakuwa na maoni yoyote kuhusu utendaji wa serikali ya sasa katika kupambana na rushwa. 45% walisema kuwa serikali inapambana vilivyo na rushwa na 17% tu walisema kuwa vita ya serikali dhidi ya rushwa haina nguvu.

Jeshi la Polisi na mfumo wa mahakama zinaonekana machoni mwa jamii kama taasisi zinazoendekeza rushwa kuliko taasisi nyingine zote. Kwa ujumla, wakazi wa mijini wanaona kuwepo zaidi kwa rushwa katika sekta ya umma kuliko wale wa vijijini, pengine kwa kuwa vyombo vya habari huzungumzia kwa kina tuhuma za rushwa. Wananchi wenye hali nzuri kimaisha wanaona kuwepo kwa kiwango kikubwa zaidi cha rushwa kuliko waonavyo wananchi maskini zaidi waliosailiwa.

Katika maoni yao, washiriki wa utafiti huu waliridhishwa kwa kiwango kikubwa mno mwitikio wa serikali wa siku za karibuni katika masuala ya amani, utulivu na usalama miongoni mwa watu. Idadi kubwa, 55%, walikuwa na maoni kuwa kiwango cha amani, utulivu na usalama miongoni mwa watu kimeongezeka kwa siku za karibuni. Wengine 44% walisema kuwa kiwango cha ubora wa huduma za msingi kimeongezeka, huku 40% wakidai hivyohivyo kuhusu mwenendo wa serikali katika kufuata sheria. Hata hivyo, 44% ya wananchi waliosailiwa hawakuwa na maoni yoyote. Licha ya hayo, wananchi bado wana wasiwasi mkubwa kuhusu kuwepo kwa vitendo vya uhalifu, vurugu, na kukosekana kwa usalama.

### Jamii, Uaminifu, Ushirikiano na Usalama

Kiwango cha jumla cha watu kukosa uaminifu kinaripotiwa sana. Hali kadhalika, watu wachache tu waliosailiwa ndio wanaoamini kuwa siku hizi watu wengi wanaweza kuaminiwa, huku 78% wanaamini kuwa hiyo sio kweli. Kiwango cha kukosa uaminifu kiko juu zaidi jijini Dar es Salaam, 85%, kuliko vijijini ambako ni 75%. Hata hivyo, walipoulizwa kuhusu mienendo ya makundi maalumu ya watu, kulikuwa na viwango vya chini zaidi vya kukosa uaminifu vilivyoripotiwa. Katika hali isiyoshangaza, watu waliosailiwa walielekea zaidi kuwaamini ndugu na jamaa zao kuliko watu wa makundi mengine ambayo wanahusiana nayo kwa mbali katika jamii. 40% ya watu waliosailiwa waliwachukulia wageni Watanzania kuwa watu wasioaminika, na idadi karibu sawa na hiyo waliwachukulia hivyo pia vijana wa kiume. 60% waliwachukulia wageni wasio Watanzania kuwa watu wasioaminika.

Kiwango cha utayari wa watu katika kuaminiana kinaashiria, na kuashiriwa na, kiwango cha uhalifu, vurugu na usalama binafsi kilichopo katika jamii. Utafiti huu ulichunguza maoni ya wananchi kuhusu athari na mwekekeo wa mambo haya na matatizo ya kijamii yanayohusiana nayo. Ulevi (kwa kuuhusisha na uhalifu) unachukuliwa kuwa ni tatizo kubwa na 63% ya watu waliosailiwa, hususan vijijini. Kwa wastani, inachukuliwa kwamba athari zitokanazo na ulevi zinazidi kuongezeka, huku matatizo mengine ya kijamii, ikiwa ni pamoja na migogoro ya mirathi na umiliki wa ardhi, utumiaji wa madawa ya kulevya, tuhuma za uchawi na unyanyasaji majumbani, yanasemekana kuwa yanapungua, aghalabu kwa kiwango kikubwa. Wizi wa mali za watu unachukuliwa kuwa tatizo kubwa na zaidi ya nusu ya watu waliosailiwa, hususan jijini Dar es Salaam. Hali kadhalika, matumizi ya madawa ya kulevya na watu kujichukulia sheria mkononi yanachukuliwa kuwa matatizo makubwa zaidi jijini Dar es Salaam (na karibu 40% ya washiriki wa huko) kuliko kwingineko.

Washiriki wengi zaidi waliona kupungua badala ya kuongezeka kwa huduma zitolewazo na jamii kwa watu maskini, wagonjwa na wazee, kuwalinda watoto dhidi ya ukatili na udhalilishaji na kuwafunza tabia njema. Tabia ya wanajamii kukarabati barabara na madaraja, na kushirikiana katika kutayarisha mashamba na kuvuna mazao mashambani vilevile inaonyesha kupungua. Kwa ujumla, kulikuwa na tofauti ndogo tu za maoni kati ya wakazi wa mijini na wale wa vijijini waliosailiwa, ambapo wote wanataja kushuka kwa kiwango cha ushirikiano katika jamii, kuwatunza na kuwasaidia wazee na ushirikiano wa wanajamii katika malezi ya vijana.

## Hitimisho

Mambo makuu yafuatayo yanaweza kuchukuliwa kuwa ndiyo maoni ya wananchi waliosailiwa:

### Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini

Kwa kutumia maoni ya watu kuhusu hali yao kiuchumi kwa siku za karibuni, mambo makuu matatu yanaweza kuonyeshwa. Kwanza, watu wengi zaidi wanaona kuwa hali yao kiuchumi ni duni zaidi sasa kuliko ilivyokuwa miaka mitatu iliyopita; pili, pengo kati ya 'matajiri' na 'maskini' linaonekana kukua zaidi; na tatu, 'tofauti ya umaskini kati ya watu wa mijini na vijijini' inaonyesha kuzidi kuwa kubwa.

Kwa watu wa madaraja yote ya vipato, ikiwa ni pamoja na wale wenye nafuu kimaisha, watu wengi zaidi wanashuhudia kushuka badala ya kupanda kwa viwango vya maisha. Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha pia kuwa wengi wa wakulima, wafugaji, na wavuvi kwa hakika wanaona kuwa hawapati msaada wowote kutoka serikalini na wengi wao wanalalamikia kupanda kwa gharama za maisha (hususan gharama za ununuzi wa chakula). Wanatoa wito wa kuboreshwa zaidi kwa hali ya upatikanaji wa pembejeo, nyenzo na mikopo.

Hali ya barabara za vijijini ilijitokeza pia kama kikwazo kikuu cha shughuli za kiuchumi na jitihada za kupunguza umaskini, ingawa katika maeneo ya mijini wananchi wengi wanakiri kuboreshwa kwa hali ya barabara.

### Utoaji Huduma

Utafiti huu unathibitisha furaha waliyo nayo wananchi wengi kuhusu uwekezaji unaofanywa na serikali katika elimu, ingawa bado kuna wasiwasi kuhusu ubora wake (kwa mfano, kuendelea kuwepo kwa upungufu wa vitabu katika shule za msingi na sekondari). Hata hivyo, utoaji wa huduma nyingine za msingi uliripotiwa kuzorota na washiriki walio wengi. Gharama kubwa za tiba na ununuzi wa madawa na ukosefu wa madawa ni miongoni mwa vikwazo vikuu katika kupata huduma za afya. Wananchi wengi wazee hukumbana na vikwazo katika kupata huduma za bure za tiba. Katika maeneo ya mijini na vijijini, huduma za maji majumbani bado linaendelea kuwa tatizo sugu kama linavyoonyeshwa kwa kutumia vigezo vya ukosefu wa maji safi na salama, na ongezeko la gharama za maji kwa wakazi wa mijini.

### Utawala Bora

Ukuaji endelevu kiuchumi, kupunguza umaskini na kuboreshwa kwa shughuli za utoaji huduma, yote haya hayawezi kufanyika bila kuboreshwa kwa shughuli za utawala katika serikali kuu na serikali za mitaa. Ingawa serikali imedhamiria kuleta maendeleo katika sekta binafsi, matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kuwa wananchi wanatarajia serikali itoe huduma stahili za kuendeleza uchumi, hususan upatikanaji wa nyenzo za uzalishaji mali. Hivyo basi, kuna wigo mpana zaidi hapa wa kutafakari kwa kina zaidi kuhusu wajibu wa serikali kwa sekta binafsi.

Utafiti huu unaonyesha kuwa wananchi wana imani kubwa na uwezo wa viongozi wa serikali iliyopo madarakani katika kuendeleza na kutekeleza sera mbalimbali kwa manufaa ya umma. Licha ya hali hiyo, utafiti huu unabainisha pia kuenea kwa rushwa na wananchi kukabiliana moja kwa moja na vitendo vya rushwa kutoka kwa watendaji wanaotoa huduma mbalimbali za msingi. Watu wanaarifu kuwa rushwa imeenea zaidi katika Jeshi la Polisi na mfumo wa mahakama. Vilevile, wananchi wengi zaidi waliosailiwa hawaoni manufaa ya misaada ya maendeleo inayotolewa kwa ajili yao. Walio wengi wanawachukulia watumishi wa umma kuwa ndio wanufaika wakuu wa misaada ya maendeleo, siyo wananchi wote.

Huku ikikabiliwa na kushuka kwa kiwango cha mshikamano na ushirikiano kama ilivyoripotiwa na wananchi wa maeneo mbalimbali, kwa hakika kubuni mbinu za pamoja za kushughulikia kasoro za kiutawala ambapo serikali, wananchi, sekta binafsi, asasi za kiraia, na jumuiya mbalimbali watafanya kazi pamoja katika kufikia lengo moja kitaifa, kutabaki kuwa miongoni mwa changamoto kuu zinazoikabili Tanzania kwa miaka mingi ijayo.

# UTANGULIZI NA METHODOLOJIA

## 1.1 Usuli

Utekelezaji wa mikakati ya kitaifa[1] ya kupunguza umaskini nchini Tanzania unasimamiwa na Mfumo wa Usimamizi wa MKUKUTA kitaifa unaoendeshwa na makundi matatu[2] ya wataalamu. Kundi la Wataalamu ya Utafiti na Uchambuzi, Kundi la Wataalamu wa Usimamizi na Uratibu wa Takwimu, na Kundi la Wataalamu wa Mawasiliano; makundi yote haya kwa pamoja huwajibika kukusanya, kuchambua na kusambaza taarifa za MKUKUTA.

Mei 2006, Kundi la Mawasiliano lilitunga hadidu za rejea kwa ajili ya kuendesha utafiti mkubwa ili kupata 'Maoni ya Watu' kuhusu utekelezaji wa MKUKUTA na utendaji wa Serikali ya Tanzania kwa ujumla. Timu ya wataalamu iliundwa kutoka makundi yote matatu ya wataalamu ili kubuni methodolojia ya utafiti unaojulikana kama 'Maoni ya Watu (2007)'. Kundi la Wataalamu wa Utafiti na Uchambuzi ilikasimu mamlaka kwa Taasisi ya Utafiti wa Kupunguza Umaskini (REPOA) ili kuendesha utafiti huo. Hojaji za utafiti zilitungwa kwa mtindo wa kusisitiza ushiriki wa wajumbe wa makundi ya wataalamu, ambao ni wawakilishi kutoka serikalini, jamii za kiraia, watafiti na wasomi, kwa kuwezeshwa na mshauri kutoka REPOA.

Kwa kutambua kuwa nusu ya Watanzania wana umri wa chini ya miaka 18, Mpango wa REPOA wa Utafiti wa Masuala ya Watoto uliendesha 'utafiti wa Maoni ya Watoto' ili kupata maoni ya kada hiyo kwa ajili ya kujaliza utafiti huu. Hii ilikuwa mara ya kwanza nchini Tanzania kwa maoni ya watoto wanaoshiriki katika utafiti kitaifa kuchambuliwa kwa utaratibu maalumu.

Ripoti hii inaeleza kwa muhtasari, taarifa za vipengele mbalimbali vya maisha ya watu, ikiwa ni pamoja na maendeleo yao kiuchumi kwa siku za karibuni, mabadiliko ya viwango vya maisha, na ubora na upatikanaji wa huduma za kiuchumi na kijamii. Hali kadhalika, kuna taarifa za maoni ya watu kuhusu mwelekeo wa shughuli za utawala, ikiwa ni pamoja na ushiriki wa wananchi katika masuala ya umma, utungaji sera, rushwa, na uaminifu. Zaidi ya hayo, ripoti hii inalinganisha matokeo ya utafiti huu na yale ya tafiti nyingine zinazofanana na huu, hususan utafiti wa Tathmini Shirikishi ya Umaskini (uliofanywa na Ofisi ya Makamu wa Rais, 2004), Utafiti wa Utoshelevu wa Sera na Huduma (PSSS, uliofanywa na REPOA, 2003) na tafiti za *Afrobarometer* (REPOA, 2003, 2005), tafiti ambazo zililenga pia kupata maoni ya watu kuhusu sera na masuala ya kisiasa na kijamii. Ripoti hii inajumuisha mambo makuu yaliyojitokeza katika utafiti wa Maoni ya Watoto, huku ripoti kamili ya utafiti huo ikitarajiwa kutolewa hivi karibuni.

Utafiti huu ulitengeneza taarifa kuhusu viashiria maalumu vya mfumo wa usimamizi wa MKUKUTA. Utafiti ulichambua maoni ya watu kuhusu maendeleo kwa kuzingatia viashiria mahususi kutoka kwenye makundi matatu ya MKUKUTA, ambayo ni: kukuza uchumi na kupunguza umaskini wa kipato, maisha bora na ustawi wa jamii, na utawala bora na uwajibikaji. Hivyo basi, utafiti huu unatoa taarifa kuhusu namna watu wanavyotambua na kuchambua mabadiliko ya sera na jinsi mabadiliko hayo yanavyoathiri maisha yao.

Kama ilivyo kawaida ya tafiti za maoni ya watu, utafiti wa Maoni ya Watu (2007) ulikusanya maoni ya washiriki kuhusu watendaji na utendaji wa asasi za umma. Wakati taarifa hizi ni muhimu kwa ajili ya mjadala wa sera kitaifa, ni muhimu kutambua kuwa matokeo ya tafiti za maoni ya watu yanaweza kutofautiana na yale ya tafiti zilizozoeleka zaidi za kaya. Mara nyingi tafiti za maoni ya watu zina mipaka kuhusu aina ya maswali yanayoweza kuulizwa kwa ajili ya kukusanya takwimu za utafiti, na kwa sababu hiyo, kuwa na mipaka pia kuhusu kiwango cha uchambuzi kinachowezekana.

1 Mkakati wa Kupunguza Umaskini (2000/01-2004) na ule ulioufuatia, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania, MKUKUTA, 2005-2010.
2 Kulikuwa na Timu nne za Wataalamu chini ya Mkakati wa Kupunguza Umaskini. Kitengo cha Sensa na Uratibu wa Takwimu na Kitengo cha Usimamizi vimeunganishwa kuwa kitengo kimoja cha kusimamia shughuli za MKUKUTA.

Hata hivyo, kumejitokeza kufanana kwa maoni ya watu kuhusu maendeleo ya kiuchumi kwa siku za karibuni, mabadiliko ya viwango vya maisha ya watu, ubora na upatikanaji wa huduma za kiuchumi na kijamii, na utawala bora, ikiwa ni pamoja na ushiriki wa wananchi katika masuala ya umma, utungaji sera, rushwa, na vilevile uaminifu, ushirikiano na usalama miongoni mwa jamii mbalimbali.

## 1.2 Methodolojia

Utafiti huu ulitafuta maoni ya Watanzania zaidi ya 7,879 wenye umri kati ya miaka 7 na 90 mwezi Machi na Aprili 2007. Utafiti ulifanywa katika mikoa kumi ya Tanzania Bara, ambayo ni Arusha, Tanga, Dar es Salaam, Lindi, Mtwara, Iringa, Singida, Rukwa, Shinyanga na Mwanza. Mikoa hii ilichaguliwa kwa kuangalia viwango vya umaskini wa mtu mmoja mmoja kama vilivyoonyeshwa katika Utafiti wa Bajeti ya Kaya 2000/01. Mikoa iligawanywa katika makundi matatu: ile iliyo chini katika jedwali ikiwa na kiwango cha juu cha umaskini wa kipato wa mtu mmoja mmoja, ile ya kati ikiwa na kiwango cha kati, na ile ya juu ikiwa na kiwango kidogo cha umaskini wa kipato wa mtu mmoja mmoja. Jedwali 1.1 hapa chini linaonyesha kwa muhtasari mgawanyo wa makundi hayo.

**Jedwali 1.1** Mgawanyo wa Viwango vya Umaskini wa Mtu Mmoja Mmoja

| Kiwango cha Umaskini kwa Mtu Mmoja Mmoja | Mikoa | | |
|---|---|---|---|
| Juu | Mwanza | Iringa | Lindi |
| Kati | Singida | Mtwara | Shinyanga, Rukwa |
| Chini | Dar es Salaam | Tanga | Arusha |




Utafiti huu ulishirikisha watoto, vijana, watu wazima na wazee. Aidha, vijana, watu wazima na wazee wapatao 1,000 hivi walishiriki majadiliano wakiwa katika vikundi maalumu.

Wilaya tatu kutoka kila mkoa zilichaguliwa kwa kuchanganya wilaya za mjini (huku wilaya tatu za mkoa wa Dar es Salaam zikichaguliwa mahususi kwa upande huo) na wilaya za vijijini, na kutoka katika madaraja matatu tofauti ya vipato vya watu: maeneo yenye watu maskini kupindukia, umaskikni kiasi, na wenye umaskini kidogo. Katika utafiti wa maoni ya watoto, shule moja ya msingi ilichaguliwa kutoka kila wilaya kwa wilaya zote kumi zilizochaguliwa kwa ajili ya utafiti, na kwa mara nyingine uwiano uliwekwa kati ya Dar es Salaam, miji mingine, maeneo ya vijijini na mchanganyiko wa watu wa viwango tofauti vya kipato.

Makundi ya watu waliosailiwa katika utafiti ni:
Watoto wenye umri wa miaka 7-14: Wanafunzi 512 wa shule ya msingi (wavulana 245 na wasichana 267), ambao walichaguliwa bila kufuata utaratibu wowote maalumu kutoka kwenye madaftari ya mahudhurio katika shule kumi, walishiriki katika utafiti kwa kutumia mbinu shirikishi zinazofaa kwa umri wao. Hawa waligawanywa katika makundi mawili - kundi moja kwa watoto wenye umri wa miaka 7-10 na lingine kwa watoto wenye umri wa miaka 11-14. Vipengele mahsusi vilivyochunguzwa na utafiti wa Maoni ya Watoto vilihusu masuala ya elimu, mahusiano na watu wazima na ushiriki wa watoto katika jamii wanamoishi, na vilevile malengo yao ya baadaye.

Vijana wenye umri wa miaka 15-24: Utafiti huu ulihusisha usaili wa ana kwa ana kwa vijana 1,525 (wasichana 885 na wavulana 640), ambapo theluthi moja ya idadi hiyo walikuwa bado wanafunzi. Mada zilizojadiliwa zilihusu masuala ya elimu, maoni yao kuhusu sera, ajira, matatizo binafsi, na malengo yao ya baadaye.

Watu wazima wenye umri wa miaka 25-59: Jumla ya watu wazima 4,967 (wanawake 2,560 - sawa na 51% ya watu waliokuwa katika sampuli ya utafiti - na wanaume 2,427 - sawa na 49% ya sampuli hiyo) walijibu maswali kuhusu ustawi wao na mwelekeo wa hali yao kiuchumi; utendaji katika utoaji wa huduma za umma za afya, maji, na barabara; ushiriki wao katika masuala ya umma, maoni yao kuhusu sera mbalimbali za serikali, mwelekeo wa masuala ya rushwa, utawala bora na uaminifu. Watu wazima wanaoishi vijijini walisailiwa kwa kina zaidi kuhusu matumizi yao ya maliasili, na namna wanavyojipatia riziki zao kupitia katika kilimo, ufugaji, na uvuvi.

Wazee (miaka 60 na kuendelea): Utafiti huu ulisaili jumla ya wazee 855 (ambapo 39% walikuwa wanawake na 61% wanaume) wenye umri wa zaidi ya miaka 60 kuhusu ustawi wao na njia za kujipatia riziki zao, huduma wanazozitoa na wanazozipata kutoka kwa watu wengine, na mambo wanayokabiliana nayo wao binafsi kutokana na uzee.

Utafiti huu ulitumia mbinu mbili za utafiti: zinazotumia vigezo vya ubora, na vile vinavyotumia vigezo vya idadi. Sehemu kubwa ya utafiti wa Maoni ya Watu ilihusisha hojaji iliyozungumzia kwa kina masuala mahususi ya makundi maalumu kama inavyoelezwa kwa muhtasari hapa chini. Uchunguzi wa vigezo vya ubora wa mada kuu za utafiti ulifanywa kupitia katika majadiliano ya vikundi maalumu. Majadiliano haya yaliendeshwa katika vikundi vya watu wa rika mbalimbali ili kutoa fursa ya kufanyika kwa uchambuzi wa kina zaidi wa mada zilizochaguliwa kutoka kwenye vipengele mbalimbali za hojaji. Takwimu zinazotumia vigezo vya ubora na idadi kutoka kwa watu waliosailiwa zilichambuliwa kwa kuzingatia malengo ya makundi matatu ya MKUKUTA. Kisanduku Namba 1 kurasa inayofuata kinaonyesha kwa muhtasari mawanda ya utafiti huu.

**SANDUKU 1: MAWANDA YA UTAFITI WA MAONI YA WATU (2007)**

**Maoni ya nani?**
Maoni ya watoto 512 wa shule za msingi wenye umri wa miaka 7-14, vijana 1,525 wenye umri wa miaka 15-24, watu wazima 4,967 wenye umri wa miaka 25-59 na wazee 855 wenye umri wa miaka 60 na kuendelea yalikusanywa kutoka mikoa kumi ya Tanzania Bara – Arusha, Dar es Salaam, Iringa, Lindi, Mtwara, Mwanza, Rukwa, Shinyanga, Singida, na Tanga mwezi Machi na Aprili 2007. Aidha, karibu watu 1,000 wenye umri wa miaka 15 na kuendelea walishiriki katika majadiliano wakiwa katika vikundi maalumu.

**Maoni kuhusu nini?**
Watoto: Elimu, habari, mawasiliano, ushiriki katika kufanya maamuzi, malengo ya baadaye

Vijana: Elimu, maoni kuhusu sera, ajira, matatizo binafsi, malengo ya baadaye

Watu wazima: Mwelekeo wa hali binafsi ya kiuchumi na ustawi
Utendaji katika utoaji huduma za umma za afya, maji, na barabara
Ushiriki katika masuala ya umma
Maoni kuhusu sera mbalimbali za serikali
Mwelekeo wa masuala ya rushwa, utawala na uaminifu
Maliasili, kilimo, ufugaji, uvuvi

Wazee: Ustawi na njia za kujipatia riziki
Huduma wanazozitoa na wanazozipata kutoka kwa wengine,masuala ya uzee

**Ni nani anayetaka kujua?**
Utafiti wa Maoni ya Watu unashughulikia masuala ya sera za umma na utendaji wa serikali, ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa MKUKUTA, kwa kuzingatia maoni ya wananchi.
Serikali, watafiti, na wawakilishi kutoka asasi za kiraia wametoa mchango wao katika Maoni ya Watu na watayatumia matokeo ya utafiti huu.
Utafiti wa Maoni ya Watu 2007 unatoa matokeo yake kuhusu wanaume na wanawake, kwa kuzingatia kiwango chao cha umaskini/utajiri na iwapo makazi yao ni mjini au kijijini.

### 1.3 Taswira ya Ripoti

Ripoti hii inatoa uchambuzi wa jumla wa maoni ya watu, hisia na tabia zao kwa kuzingatia maeneo wanayotoka, jinsia yao, na viwango vyao vya umaskini na kulinganisha matokeo ya utafiti huu na yale ya tafiti zilizopita. Muhtasari wa vipimo vya utajiri/umaskini viliandaliwa ili kurahisisha uchambuzi wa takwimu. Usuli wa utafiti huu umetolewa katika Sura ya 1 ikifuatiwa na:

Sura ya 2 hadi ya 7: Maoni kuhusu masuala ya Kundi la Kwanza la MKUKUTA, ikiwa ni pamoja na kukuza uchumi na kupunguza umaskini. Hii inajumuisha mabadiliko yaliyoonekana katika huduma za kiuchumi, kipato na njia za kujipatia riziki za wananchi wa mijini na vijijini, na vigezo vikuu vya kupima shughuli za vijana za kujipatia riziki.

Sura ya 8 hadi ya 12: Mwelekeo wa masuala ya Kundi la Pili la MKUKUTA, ikiwa ni pamoja na utoaji wa huduma za jamii, mifano ikiwa elimu ya msingi na sekondari, huduma za afya na upatikanaji wa maji majumbani, msisitizo katika masuala yanayowahusu watoto, vijana na wazee.

Sura ya 13 na ya 14: Masuala ya utawala bora kwa mtazamo wa wananchi, ikiwa ni pamoja na tathmini kuhusu ufahamu wa Watanzania wa taarifa mbalimbali na ushiriki wao katika masuala ya umma. Sura hii inachunguza pia maoni ya watu kuhusu sera za kiuchumi na kisekta na athari zake. Mwishoni, sura hii inazungumzia maoni na uzoefu wa washiriki katika masuala ya rushwa na uwajibikaji katika utoaji huduma kwa umma. Aidha, yameripotiwa matokeo ya utafiti kuhusu kiwango cha uaminifu kati ya mtu na mtu na miongoni mwa makundi ya watu katika jamii, na kiwango ambacho watu hutatua matatizo ya pamoja kwa kushirikiana na kwa kufuata utaratibu ama kila mmoja kwa namna yake na kwa faida yake binafsi. Aidha, sura ya 14 inachambua maoni ya watu kuhusu watu wanaoaminika na wasioaminika.

Sura ya 15: inatoa hitimisho la utafiti wote kwa ujumla.

# SEHEMU YA KWANZA:

## MKUKUTA KUNDI LA I

### KUKUZA UCHUMI NA KUPUNGUZA UMASKINI

# HALI YA UCHUMI WA WATU

Malengo makuu ya sera za umma nchini Tanzania ni kuchochea ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini. Utafiti wa Maoni ya Watu uliuliza kuhusu uzoefu na maoni ya watu kuhusu mabadiliko yao kiuchumi na upatikanaji wa huduma mbalimbali.

## 2.1 Mwelekeo wa Hali ya Uchumi wa Watu

Watu wazima waliosailiwa walibaini kuwepo kwa mabadiliko ya hali yao kiuchumi katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, na matokeo hayo yameonyeshwa kwa muhtasari katika Jedwali 2.1. Kuna watu wazima wachache mno wanaoona kuwa wanafaidi matunda ya kukua kwa uchumi ikilinganishwa na wale wanaoona kuwa shughuli zao za kujipatia riziki zinazidi kudorora. Wakati nusu ya watu wazima walishuhudia kozorota kwa hali yao kiuchumi katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, 26% hawakuona mabadiliko yoyote na 24% walisema kuwa hali yao kiuchumi ilizidi kuwa nzuri. Kulikuwa na tofauti ndogo sana ya maoni kati ya washiriki wa vijijini na mijini.

**Jedwali 2.1** Maoni ya Wananchi kuhusu Mabadiliko ya Kiuchumi 2004 - 07[3]

| Hali ya Uchumi | Dar es Salaam % | Miji Mingine % | Maeneo ya Vijijini % | Kote % |
|---|---|---|---|---|
| Ilikuwa mbaya | 46 | 50 | 52 | 50 |
| Haikubadilika | 31 | 22 | 25 | 26 |
| Ilikuwa nzuri zaidi | 22 | 27 | 23 | 24 |

Uchambuzi wa hali ya uchumi ya makundi mbalimbali ya kiuchumi unaonyesha mwelekeo unaofanana, kama ilivyoonyeshwa katika Jedwali 2.2. Watu wa madaraja yote ya vipato, ikiwa ni pamoja na wale wenye nafuu kimaisha, waliona kuzorota badala ya kuboreka kwa hali ya maisha. Kwa watu maskini waishio mijini, idadi ya 'walioshindwa' maisha ni mara tatu zaidi ya wale 'waliofanikiwa' Baadhi ya watu wanajiona kuwa 'wamefanikiwa' maisha, hata miongoni mwa wakazi maskini wa mijini 18%, na wa vijijini 21%.

**Jedwali 2.2** Mabadiliko ya Hali ya Kiuchumi 2004-07 kwa Madaraja ya Vipato

| Mabadiliko ya Hali ya Uchumi | Maskini Mijini % | Daraja la Kati Mijini % | Wenye Nafuu Mijini % | Wote Mijini % | Wote Vijijini % | Wote % |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Nzuri zaidi | 0.4 | 0.5 | 1.2 | 0.7 | 0.7 | 0.7 |
| Nzuri kidogo | 18 | 21 | 31 | 23 | 21 | 22 |
| Hakuna mabadiliko | 24 | 29 | 28 | 26 | 25 | 26 |
| Mbaya kidogo | 23 | 22 | 21 | 22 | 24 | 23 |
| Mbaya zaidi | 33 | 27 | 18 | 26 | 29 | 28 |

**Angalizo:** Jedwali hili halihusishi takwimu za washiriki ambao hawakutoa majibu.

3 Katika jedwali hili na baadhi ya majedwali yanayofuata, jumla ya asilimia ni pungufu ya 100% kwani tarakimu zimekadiriwa kwa namba iliyo karibu na vilevile baadhi ya wananchi waliosailiwa hawakuwa na majibu kwa maswali waliyoulizwa.

Kwa swali lililowataka washiriki kutoa maoni yao washiriki waliulizwa kama kulikuwa na mabadiliko makubwa katika hali ya maisha kwa miaka mitatu iliyopita - Jedwali 2.3. Karibu 79% ya watu waliosailiwa mijini na vijijini hawakuona mabadiliko yoyote. Kujenga nyumba, ingawa ulitajwa na 7% tu ya washiriki, ndiyo mafanikio makubwa zaidi kwa washiriki wa maeneo yote, ukifuatiwa na manunuzi makubwa - kwa mfano, ununuzi wa simu ya mkononi, baiskeli au bidhaa nyingine.

**Jedwali 2.3** **Mabadiliko katika Maisha 2004-07**

| Mabadiliko katika Maisha | Dar es Salaam % | Miji Mingine % | Maeneo ya Vijijini % | Kote % |
|---|---|---|---|---|
| Hakuna mabadiliko | 79 | 76 | 80 | 79 |
| Nimejenga nyumba | 7 | 6 | 8 | 7 |
| Nimenunua simu, baiskeli, bidhaa nyingine | 4 | 6 | 3 | 4 |
| Nimenunua mifugo | 0 | 1 | 2 | 2 |
| Nimenunua ardhi, nimeongeza eneo la ardhi (kununua au kukodi) | 3 | 3 | 2 | 2 |
| Kipato kimeongezeka | 2 | 3 | 2 | 2 |
| Nimewekeza katika elimu | 2 | 3 | 1 | 2 |
| Nimeanzisha biashara | 1 | 1 | 2 | 1 |

# KUENDELEZA UKUAJI MPANA WA UCHUMI: MIUNDOMBINU

Miundombinu ya kiuchumi huchangia moja kwa moja na kwa kupitia njia nyingine katika kukuza uchumi na kupunguza umaskini. Maoni ya wananchi yalitafutwa kuhusu mwelekeo wa utendaji katika mambo makuu matatu ya miundombinu ya kiuchumi.

## 3.1 Barabara

Hali mbaya ya barabara na kutozifanyia matengenezo ni tatizo kubwa, hususan vijijini. 70% ya watu wazima waliosailiwa vijijini waliichukulia hali ya ubovu wa barabara kuwa 'tatizo kuu', kulinganisha na 57% ya wananchi waliosailiwa katika miji mingine na 41% kwa wakazi wa Dar es Salaam. Kutofautisha kwa makundi ya kiuchumi kunaonyesha hali kuwa mbaya zaidi machoni mwa watu wengi walio maskini - 72%, kulinganisha na makundi yenye kipato cha kati - 63%, na yale ya watu wenye nafuu kimaisha - 60%, kama inavyotarajiwa kwani watu maskini wanaelekea zaidi kuwa wakazi wa vijijini.

**Jedwali 3.1** Asilimia ya Watu Wazima Walioripoti Hali ya Barabara kuwa Tatizo Kuu

| Dar es Salaam % | Miji Mingine % | Maeneo ya Vijijini % | Watu Maskini % | Daraja la Kati % | Wenye Nafuu % | Wote % |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 41 | 57 | 70 | 72 | 63 | 60 | 60 |

Matokeo haya yanathibitishwa na maoni ya watu kuhusu hali ya barabara za vijijini. 28% tu ya washiriki wa vijijini waliona kuwepo kwa maboresho ya hali ya barabara katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, huku 47% wakiripoti kuwa barabara zilizidi kuchakaa (Jedwali 3.2).

**Jedwali 3.2** Maoni kuhusu Mabadiliko ya Ubora wa Barabara 2004-2007

| Hali ya Barabara | Dar es Salaam % | Miji Mingine % | Maeneo ya Vijijini % | Kote % |
|---|---|---|---|---|
| Imeboreka | 56 | 42 | 28 | 38 |
| Haijabadilika | 27 | 28 | 26 | 27 |
| Imechakaa zaidi | 16 | 30 | 47 | 36 |

Maboresho ya hali ya barabara yalionekana katika maeneo ya mijini - 56% kwa Dar es Salaam na 42% kwa miji mingine. Mifano ya maoni ya washiriki kuhusu hali ya barabara imetolewa kwenye Kisanduku Namba 2.

**SANDUKU 2**: HALI YA BARABARA

*"Barabara ni mbaya sana. Wakulima hulazimika kusafirisha mazao na wanyama kwa mkokoteni (tela la wanyama)."*
• Kikundi Maalumu, Singida

*"Hakuna utengenezaji wa barabara huku mpaka ujio wa Raisi ambaye alipita [Mzee Mwinyi] mara ya mwisho mwaka 1988."*
• Kikundi Maalumu, Kata ya Nyarugusu, Mwanza

*"Barabara hazipitiki. Kama kuna kata zilizosahaulika kimiundombinu ni Igogo."*
• Kikundi Maalumu, Kata ya Igogo, Mwanza

Kutokana na hali mbaya ya barabara za vijijini, ukuaji wa uchumi katika maeneo haya hukwama kwa kiwango kikubwa mno. Nusu ya watu wa vijijini waliosailiwa walibainisha kuwa kutokana na ubovu wa barabara, huwa vigumu kwao kuyafikia masoko ya kuuzia mazao yao na kupata huduma mbalimbali mijini.

### 3.2 Nishati

Washiriki walio wengi hutumia kuni na mkaa kwa kupikia, na mafuta ya taa (kwenye koroboi, taa ya chemli, karabai) kwa ajili ya kupata mwanga majumbani, tazama Jedwali 3.3. Matumizi ya mkaa yanatajwa zaidi jijini Dar es Salaam ambako hutumiwa na 83% ya washiriki. Kuni hutumiwa kama chanzo cha nishati na 87% ya washiriki wa vijijini na 57% ya washiriki kutoka miji mingine. Kwa ujumla, umeme ulitajwa kuwa chanzo cha nishati ya mwanga na 23% ya washiriki - ukitajwa na 59% ya washiriki wa Dar es Salaam, 43% ya washiriki wa miji mingine, na 11% ya washiriki wa vijijini.

Upatikanaji na gharama za ununuzi wa mkaa kwa wakazi wengi wa mjini na kuni kwa wakazi wengi wa vijijini yaliripotiwa kuwa matatizo makuu. Kwa maeneo ya mijini, 59% ya watu waliosailiwa waliichukulia hali ya upatikanaji na gharama za nishati ya kupikia kuwa 'tatizo kuu', kama ilivyokuwa kwa 50% ya wakazi wa vijijini. Nusu ya washiriki wa mijini na vijijini waliichukulia hali ya upatikanaji wa umeme kuwa ni tatizo kuu. Katika maeneo ya mijini, matatizo ya upatikanaji wa huduma ya umeme yanajumuisha gharama kubwa na ugumu wa kuunganishiwa umeme, na vilevile umeme kukatwa mara kwa mara. Katika maeneo ya vijijini, tatizo ni kwamba vijiji vingi havina umeme kutoka kwenye *gridi* ya taifa au kwenye vyanzo vingine.

**Jedwali 3.3** Vyanzo vya Nishati ya Mwanga na ya Kupikia

| Chanzo cha Nishati | Dar es Salaam % | Miji Mingine % | Maeneo ya Vijijini % | Kote % |
|---|---|---|---|---|
| **Kupikia** | | | | |
| Mkaa | 83 | 34 | 12 | 35 |
| Kuni | 8 | 57 | 87 | 60 |
| Jiko la mafuta ya taa | 7 | 8 | 0 | 3 |
| **Mwanga** | | | | |
| Umeme | 59 | 43 | 11 | 23 |
| Taa za mafuta ya taa | 36 | 54 | 76 | 72 |

**Angalizo:** Jumla ya asilimia yaweza kuwa pungufu ya 100 kwa sababu baadhi ya watu waliosailiwa hawakujibu maswali.

### 3.3 Simu

Idadi ya watu wanaomiliki simu imeongezeka mara nne zaidi ya ile iliyokuwepo miaka minne iliyopita. Watanzania wengi zaidi sasa wanawasiliana kwa kutumia simu za mkononi na kwa ujumbe mfupi wa maandishi (SMS) kuliko ilivyokuwa siku zilizopita. Karibu 33% ya watu wazima waliosailiwa walimiliki simu za mkononi: 65% jijini Dar es Salaam, 37% katika miji mingine, na 16% vijijini. Jijini Dar es Salaam, 17% ya watu maskini zaidi waliosailiwa wanamiliki simu za mkononi, kulinganisha na 86% ya wale wenye hali nzuri kimaisha. Jedwali 3.4 linaonyesha kuwa, wakati washiriki wachache tu ndio huandikiana barua, idadi kubwa ajabu hutumiana ujumbe mfupi wa maandishi mara kwa mara.

**Jedwali 3.4** Njia za Mawasiliano, kwa Maeneo

| Njia za Mawasiliano | Dar es Salaam % | Miji Mingine % | Maeneo ya Vijijini % | Kote % |
|---|---|---|---|---|
| Kupiga simu | 53 | 31 | 15 | 28 |
| Ujumbe mfupi | 42 | 24 | 9 | 21 |
| Kuandika barua | 4 | 4 | 3 | 4 |

Ongezeko la kasi la hivi karibuni la idadi ya watu wanaomiliki simu za mkononi limeongeza kiwango cha mawasiliano miongoni mwa watu nchini kote kwa namna ya kustaajabisha, ijapokuwa hali hiyo inaweza kutabirika miongoni mwa wakazi wa mijini na wale wa vijijini na miongoni mwa matajiri na maskini. Licha ya hivyo, kuboreshwa kwa mawasiliano ya simu kunaweza kuwa hakujachangia vya kutosha katika kukuza uchumi kwani karibu 75% ya watu wanaomiliki simu waliarifu kuwa hutumia simu zao kwa masuala binafsi badala ya shughuli za kiuchumi na 25% tu ndiyo walioarifu kuwa hutumia simu zao kwa masuala binafsi na yale ya kibiashara.

# HALI YA UCHUMI

Maoni ya watu yalitathminiwa kwa kutumia vigezo kadhaa kuhusu hali yao kiuchumi, ni pamoja na suala la ajira na njia nyingine za kujipatia riziki, upatikanaji na gharama za ununuzi wa nyenzo za uzalishaji mali na upatikanaji na gharama za ununuzi wa chakula na mahitaji mengine ya msingi.

## 4.1 Gharama za Maisha

Wakati gharama za maisha - gharama za ununuzi wa chakula na mahitaji mengine ya msingi - kulitajwa kuwa tatizo kuu na 67% ya watu wazima, huku hali hiyo ikiathiri watu wa mijini na vijijini, 47% walisema kamwe hawakuwa na matatizo ya upungufu wa chakula mwaka uliopita na 63% walisema walikula milo mitatu kwa siku (Jedwali 4.1). Ingawa watu maskini walikuwa na wasiwasi zaidi kuhusu kupanda kwa bei ya chakula na bidhaa nyingine za msingi kuliko watu wenye nafuu kimaisha, karibu 66% ya washiriki wenye hali nzuri kimaisha nao pia walichukulia kupanda kwa gharama za maisha (bei ya chakula na bidhaa nyingine muhimu) kuwa tatizo kuu.

**Jedwali 4.1** Matatizo ya Bei ya Chakula na Bidhaa Muhimu

| Bei ya Bidhaa Ni Tatizo Kuu | Dar es Salaam % | Miji Mingine % | Maeneo ya Vijijini % | Kote % |
|---|---|---|---|---|
| Bei ya bidhaa muhimu | 65 | 70 | 71 | 69 |
| Bei ya chakula | 72 | 72 | 63 | 67 |

Washiriki waliulizwa ni mara ngapi hula nyama au samaki, kwa wastani hula milo mingapi kwa siku, na iwapo walikuwa na chakula cha kutosha kwa kipindi chote cha mwaka uliopita. Wakazi wa mijini walidai kuwa hula nyama au samaki kwa siku karibu tatu kwa wiki, wakati katika maeneo ya vijijini wastani ulikuwa chini ya siku mbili kwa wiki. Takriban robo tatu, 78%, ya washiriki wa Dar es Salaam hula milo mitatu kwa siku, kulinganisha na theluthi mbili, 64%, katika mji mingine na 55% tu katika maeneo ya vijijini.

Walipoulizwa iwapo walikumbwa na njaa katika kipindi cha mwaka uliopita, moja ya tano, 19%, ya wanavijiji walijibu ‘mara kwa mara’ na wengine wapatao 43% walijibu ‘wakati mwingine’. Theluthi moja, 32%, ya washiriki wa Dar es Salaam waliripoti kuwa ‘wakati mwingin’ hukumbwa na njaa, na 5% walisema ‘mara kwa mara’. Kisanduku Namba 3 kinaonyesha baadhi ya maoni ya watu kuhusu bei za vyakula na uhusiano uliopo kati ya kipato cha mtu na upatikanaji wa chakula.

**SANDUKU 3**: **MAONI KUHUSU BEI ZA VYAKULA**

*“Vyakula vinapatikana, inategemea na kipato cha mtu… Mazingira ya upatikanaji wa chakula ni magumu kwani bei ni kubwa na kipato ni kidogo na wengine hawana kabisa kipato.”*
• Kikundi Maalumu, Keko, Dar es Salaam

### 4.2 Njia za Kujipatia Riziki Mijini na Vijijini

Kipengele hiki kinazungumzia njia mbalimbali za watu kujipatia riziki. Jedwali 4.2 linaonyesha kwa muhtasari vyanzo vya kipato kwa watu wazima (4,967 wenye umri wa miaka 25-59) waliosailiwa katika utafiti huu.

**Jedwali 4.2** Kazi / Vyanzo vya Riziki

| Njia za Kujipatia Riziki | Wanaume % | Wanawake % | Dar es Salaam % | Miji Mingine % | Maeneo ya Vijijini % | Jumla % |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Kilimo, ufugaji, uvuvi | 68 | 49 | 4 | 51 | 87 | 58 |
| Waliojiajiri, hakuna waajiriwa | 15 | 22 | 41 | 23 | 6 | 19 |
| Wafanyakazi wa nyumbani / wafanyakazi mashambani wasio na ujira / biashara ya familia | 2 | 17 | 23 | 11 | 2 | 10 |
| Waajiriwa* | 7 | 4 | 15 | 6 | 5 | 6 |
| Wategemezi: wastaafu / wanafunzi | 2 | 4 | 7 | 2 | 0 | 3 |
| Waliojiari na wenye waajiriwa | 3 | 1 | 6 | 4 | 0 | 3 |
| Hawakuajiriwa: wanatafuta kazi | 0 | 1 | 3 | 1 | 0 | 1 |
| Wengineo | 2 | 0 | 1 | 0 | 1 | 1 |

**Waajiriwa**: Sekta rasmi = 41%
Serikalini/mashirika ya umma/vyama vya ushirika/bodi za masoko = 37%
Sekta isiyo rasmi = 15%
Makanisa, mashirika ya hisani na asasi zisizo za kiserikali = 6%

Asilimia 87 ya watu wazima waishio vijijini walijishughulisha na kilimo, pamoja na ufugaji au uvuvi. Jijini Dar es Salaam 41% walikuwa wamejiajiri na 23% waliripotiwa kwamba walikuwa wafanyakazi wa nyumbani / wafanyakazi wa familia wasio na ujira, 15% walikuwa wameajiriwa, hususan katika taasisi za sekta rasmi. Katika maeneo mengine ya mijini 51% walijishughulisha na kilimo, pamoja na ufugaji au uvuvi 23% walikuwa wamejiajiri na 11% walikuwa wafanyakazi wa nyumbani / wafanyakazi wa familia wasio na ujira. Watu wazima wachache waliosailiwa walisema hawakuwa na ajira, huku wengine wakiwa wa Dar es Salaam na miji mingine. Ukosefu wa ajira ulikuwa tatizo kubwa zaidi miongoni mwa vijana, kama itakavyoonyeshwa katika vipengele vinavyofuata vya sehemu hii.

Zaidi kidogo ya nusu ya watu wazima waliosailiwa vijijini, 52% walisema kuwa wanahisi hali yao kiuchumi ni mbaya zaidi sasa kuliko ilivyokuwa miaka mitatu iliyopita, 25% walisema ilikuwa ileile na 23% walisema ilikuwa imekuwa nzuri zaidi.

Wakati mwingine kaya huamua kuwa na vyanzo mbalimbali vya kujipatia riziki kama hatua ya tahadhari dhidi ya matatizo yanayoweza kujitokeza, ingawa utafiti uliofanywa kwa watu wazima ulibaini kuwa wengi wao walikuwa na chanzo kimoja tu cha mapato. Mathalani, katika maeneo ya vijijini 74%, na jijini Dar es Salaam 81% ya watu wazima waliosailiwa walikiri kuwa hawakuwa na chanzo cha pili cha mapato. Katika maeneo ya vijijini, watu waliokuwa na vyanzo vingine vya mapato ni wale waliokuwa wamejiajiri - 59%, wale waliokuwa na shughuli nyingine za kujipatia riziki maeneo ya vijijini - 26%, au shughuli nyingine mbalimbali. Jijini Dar es Salaam, shughuli kuu ya ziada ya kujiongezea kipato ilikuwa kujiajiri - 16%. Hata hivyo, inawezekana kwamba wanafamilia wengine katika kaya za watu waliosailiwa katika utafiti huu walichangia pia katika pato la familia kupitia njia nyingine za kujipatia riziki. Sehemu zinazofuata zinachunguza kwa kina zaidi shughuli za kujipatia riziki vijijini.

# KILIMO

Sura hii inazungumzia shughuli zinazofanywa na wakulima ili kujipatia riziki. Nayo imegawanywa katika makundi matatu kwa kutumia viashiria mbalimbali vya nguvu za kiuchumi kama vile rasilimali alizo nazo mtu, ubora wa nyumba ya kuishi, upatikanaji wa huduma ya maji na vigezo vingine mbalimbali. Neno 'wakulima' linajumuisha wanaume na wanawake walioarifu kuwa shughuli yao kuu ya kujipatia riziki ni kilimo. Vigezo vilivyotumiwa hapa kupima viwango vya umaskini au utajiri vinazingatia hali ilivyo kwa kaya nzima na siyo hali ya mtu mmoja mmoja. Hivyo basi, mambo ya ndani ya familia kama vile kutokuwepo kwa mgawanyo sawa wa kazi, ustawi wa wanafamilia au kiwango cha rasilimali zinazotumiwa na kila mwanafamilia hayakuzingatiwa. Makundi hayo matatu ya shughuli za kujipatia riziki vijijini yanatajwa katika maelezo ya uchambuzi yanayofuata kama 'watu maskini zaidi' (kundi la kwanza), 'watu wa daraja la kati' (kundi la pili), na 'watu wenye nafuu kimaisha' (kundi la tatu). Makundi haya matatu ni ya kufikirika tu. Yameundwa kwa sababu za kiuchambuzi tu. Si makundi halisi yanayojibainisha katika jamii.

## 5.1 Umiliki wa Ardhi na Teknolojia ya Kilimo

Idadi ya mashamba na ukubwa wa mashamba yaliyoripotiwa katika utafiti huu kuwa yanamilikiwa na wakulima hauonyeshi kuwepo kwa wakulima wakubwa. Wakati wakulima wa kundi la watu maskini zaidi walilima shamba 1.9, wale wa daraja la kati na wenye nafuu kimaisha walikuwa na mashamba 2.2. Jumla ya ukubwa wa mashamba yaliyokuwa yakilimwa ulianzia ekari 4.5 kwa wakulima maskini hadi ekari 6.4 kwa wale wenye nafuu kimaisha, sawa na tofauti ya 42%. Kikwazo kikuu cha watu kumiliki mashamba makubwa ni aina ya teknolojia iliyotumiwa katika kulima mashamba hayo. Hivyo basi, wakati wakulima wote walitumia zana hafifu ya jembe la mkono kwa shughuli nyingi za kilimo, 42% ya wakulima wasio maskini walitumia plau, huku robo (25%) tu ya wakulima maskini ndio wakitumia zana hiyo. 5% tu ya wakulima wenye nafuu kimaisha ndio waliotumia trekta.

Aidha, shughuli za ukodishaji na ununuzi wa ardhi zinaonekana kuwa hazijaendelezwa kwani 82% ya wakulima hulima mashamba yao ya asili, na chini ya 20% hukodi baadhi au mashamba yote wanayoyalima. Hapakuwa na mwelekeo wa wakulima wenye hali bora kukodi mashamba zaidi ya wakulima maskini. Karibu 25% ya wakulima walikuwa na vyanzo vingine vya mapato, wengi wao wakiwa wazalishaji mali au wafanyabiashara wadogo wadogo.

## 5.2 Aina ya Mazao Yanayolimwa

Wakulima waliulizwa kuhusu aina ya mazao ya chakula waliyolima na iwapo kwa kiasi kikubwa mazao hayo yalilimwa kwa ajili ya matumizi ya nyumbani - rejea Jedwali 5.1 na Jedwali 5.2. Karibu wakulima wote walilima mahindi, na 64% ya wakulima wa mahindi walisema kuwa kiasi chote au karibu chote

**Jedwali 5.1** Asilimia ya Wakulima wa Mazao Makuu ya Chakula

| Zao | Maskini Zaidi % | Daraja la Kati % | Wenye Nafuu Kimaisha % | Wote % |
|---|---|---|---|---|
| Mahindi | 90 | 92 | 94 | 92 |
| Maharage / jamii ya kunde | 49 | 54 | 62 | 55 |
| Matunda / mbogamboga | 37 | 47 | 52 | 45 |
| Viazi | 34 | 46 | 49 | 43 |
| Mtama / ulezi / uwele | 48 | 48 | 29 | 42 |
| Mhogo | 37 | 40 | 33 | 37 |
| Mpunga | 28 | 33 | 26 | 29 |
| Ndizi | 12 | 16 | 20 | 16 |

cha mahindi yao kilikuwa kwa ajili ya matumizi ya nyumbani. Wakulima maskini zaidi, kulinganisha na wale wenye nafuu kimaisha, walielekea zaidi kulima mtama, ulezi, uwele, na mhogo, wakati wakulima wenye hali bora walielekea zaidi kulima maharage, matunda na mbogamboga, viazi, na ndizi. Kwa sehemu kubwa, wakulima walio wengi walilima mazao kwa ajili ya matumizi ya nyumbani.

**Jedwali 5.2 Asilimia ya Wakulima Walioripoti Kutumia Sehemu Kubwa ya Mazao kwa Matumizi ya Nyumbani**

| Zao | Maskini Zaidi % | Daraja la Kati % | Wenye Nafuu Kimaisha % | Wote % |
|---|---|---|---|---|
| Viazi | 88 | 87 | 78 | 84 |
| Matunda / mbogamboga | 76 | 81 | 71 | 76 |
| Mtama / ulezi / uwele | 71 | 75 | 72 | 73 |
| Maharage / jamii ya kunde | 69 | 69 | 63 | 67 |
| Ndizi | 67 | 75 | 57 | 66 |
| Mahindi | 68 | 68 | 57 | 64 |
| Mhogo | 59 | 65 | 67 | 64 |
| Mpunga | 57 | 55 | 42 | 51 |

### 5.3 Matatizo Makubwa Yanayowakabili Wakulima

Wakulima waliulizwa iwapo bei na upatikanaji wa pembejeo na mambo mengineyo ilikuwa tatizo katika kipindi cha miezi kumi na miwili kabla ya kufanywa kwa utafiti huu. Jedwali 5.3 linaonyesha kwa muhtasari majibu waliyoyatoa. Mambo kumi ya kwanza yaliyoorodheshwa katika jedwali yalitajwa kuwa 'tatizo kuu' na nusu au zaidi ya nusu ya watu waliosailiwa. Kwa ujumla, kulikuwa na kufanana kwa matatizo yaliyotajwa kuwakabili watu waliokuwa katika daraja sawa la kipato.

**Jedwali 5.3 Matatizo Makubua Yanayowakabili Wakulima**

| Matatizo Makubua Yaliyotajwa na Wakulima | Maskini Zaidi % | Daraja la Kati % | Wenye Nafuu Kimaisha % | Wote % |
|---|---|---|---|---|
| Bei za pembejeo | 87 | 87 | 82 | 85 |
| Upatikanaji wa pembejeo | 77 | 71 | 64 | 71 |
| Kufaa / ubora wa pembejeo | 75 | 72 | 61 | 70 |
| Magonjwa, wadudu waharibifu, wanyama waharibifu | 73 | 69 | 65 | 69 |
| Hali ya barabara | 67 | 67 | 63 | 66 |
| Majira ya mvua yasiyoaminika | 71 | 68 | 58 | 66 |
| Bei za mazao sokoni | 62 | 64 | 59 | 62 |
| Ushauri wa wataalamu | 68 | 57 | 55 | 60 |
| Umbali wa kuyafikia masoko / gharama za usafirishaji | 50 | 51 | 49 | 50 |
| Upatikanaji wa habari za masoko | 50 | 52 | 47 | 50 |
| Ardhi yenye rutuba / mmomonyoko wa udongo | 42 | 42 | 42 | 42 |
| Uhaba wa ardhi ya kilimo | 44 | 43 | 40 | 42 |
| Mashamba kuwa mbali mbali/muda wa kuyafikia mashamba | 38 | 40 | 42 | 40 |
| Maji kwa umwagiliaji | 43 | 40 | 35 | 39 |
| Vyama vya ushirika / vyama vya wakulima | 34 | 35 | 33 | 34 |
| Maghala ya kuhifadhia mazao | 37 | 35 | 29 | 34 |
| Uhalifu na wizi | 28 | 29 | 30 | 29 |
| Bodi za ununuzi wa mazao | 22 | 26 | 24 | 24 |
| Ushuru, kodi, makato | 19 | 19 | 16 | 18 |
| Udhibiti wa serikali za mitaa | 12 | 15 | 14 | 13 |

## 5.4 Matumizi ya Mbolea na Pembejeo Nyinginezo

Wakulima walio wengi hawajawahi kamwe kutumia mbolea za kemikali, au pembejeo nyingine za kemikali, au mbegu zilizoboreshwa. Miongoni mwa watu wenye kipato cha daraja la kati, wachache sana ndio waliowahi kutumia pembejeo hizi, na wachache wamewahi kutumia dawa za kemikali za kuua wadudu waharibifu wa mazao ya kilimo na sumu za mimea. Zaidi ya theluthi mbili, 69%, ya wakulima wenye nafuu kimaisha pia hawajawahi kamwe kutumia mbolea za kemikali.

**Jedwali 5.4** Matumizi ya Pembejeo Asilia na za Kibiashara katika Kilimo

| Matumizi ya Pembejeo za Kilimo | Wakulima Maskini Zaidi % | Wakulima wa Daraja la Kati % | Wakulima Wenye Nafuu Kimaisha % | Wote % |
|---|---|---|---|---|
| **Mbolea za Kemikali** | | | | |
| Makubwa | 0 | 1 | 9 | 3 |
| Kiasi karibu kilekile | 1 | 4 | 10 | 5 |
| Kiasi kidogo | 1 | 5 | 12 | 6 |
| Hawajawahi kutumia | 98 | 90 | 69 | 86 |
| **Madawa ya Kilimo ya Kemikali** | | | | |
| Makubwa | 2 | 5 | 9 | 3 |
| Kiasi karibu kilekile | 6 | 12 | 19 | 12 |
| Kiasi kidogo | 8 | 11 | 12 | 10 |
| Hawajawahi kutumia | 84 | 72 | 60 | 72 |
| **Mbolea za Asili** | | | | |
| Makubwa | 11 | 17 | 16 | 15 |
| Kiasi karibu kilekile | 12 | 17 | 19 | 16 |
| Kiasi kidogo | 7 | 10 | 14 | 10 |
| Hawajawahi kutumia | 70 | 56 | 52 | 60 |
| **Mbegu Zilizoboreshwa** | | | | |
| Makubwa | 3 | 6 | 11 | 7 |
| Kiasi karibu kilekile | 3 | 9 | 14 | 9 |
| Kiasi kidogo | 4 | 8 | 9 | 7 |
| Hawajawahi kutumia | 89 | 76 | 66 | 77 |

## 5.5 Ushauri wa Kitaalamu Unaotolewa kwa Wakulima

Jedwali 5.5 linaonyesha kiwango cha ushauri ambacho wakulima walikipata kutoka kwa wataalamu wa kilimo wa serikali na wa sekta binafsi katika kipindi cha mwaka mmoja kabla ya kufanywa kwa utafiti huu. Ushiriki wa sekta binafsi katika kutoa huduma za kitaalamu kwa wakulima ulikiwa mdogo sana. Idadi ndogo tu ya wakulima - maskini kwa matajiri - ndiyo waliopata ushauri wa kitaalamu. Mathalani, wakati wa usaili wa vikundi mkoani Lindi, wakulima walieleza kuwa wanajua kwamba kuna bwana shamba ambaye jukumu lake ni pamoja na kuwapa ushauri wa kitaalamu na huduma nyinginezo, lakini ziara zake hazitabiriki, na wakulima wengi hawapati ushauri wowote wa kitaalamu mwaka hadi mwaka (rejea maelezo yaliyonukuliwa kwenye Kisanduku Namba 4).

**Jedwali 5.5** Ushauri wa Kitaalamu kwa Wakulima

| Ushauri wa Kitaalamu kwa Wakulima | Maskini Zaidi % | Daraja la Kati % | Wenye Nafuu Kimaisha % | Wote % |
|---|---|---|---|---|
| **Je, ulipokea ushauri wowote kutoka kwa mtaalamu wa kilimo wa serikali (mwaka jana)?** | | | | |
| Ndiyo | 18 | 24 | 22 | 21 |
| Hapana | 82 | 76 | 78 | 79 |
| **Je, ulipokea ushauri wowote kutoka kampuni binafsi (mwaka jana)?** | | | | |
| Ndiyo | 1 | 3 | 3 | 2 |
| Hapana | 99 | 97 | 97 | 98 |

**SANDUKU 4: UPATIKANAJI WA HUDUMA ZA USHAURI WA KITAALAMU KWA WAKULIMA**

*"Wataalamu wanakaa wilayani tu, vijijini tunayumba."*
• Kikundi Maalumu, Lindi

### 5.6 Masoko

Washiriki waliulizwa kuhusu namna wanavyouza mazao yao makuu ya biashara. Njia iliyotumiwa na wengi wa wakulima maskini na wale wenye nafuu kimaisha ni kuwauzia wanunuzi binafsi, ikifuatiwa na kuwauzia moja kwa moja walaji au masoko yaliyo kwenye maeneo husika. Wakulima wachache waliuza mazao yao kwenye vyama vya ushirika. Kisha wakulima waliulizwa kuhusu njia waliyoipendelea katika kuuza mazao yao. Theluthi moja, 30%, ya wakulima waliosailiwa hawakuwa na chaguo maalumu kwa suala la kuuza mazao yao, idadi karibu sawa na hiyo (21% hadi 26%) walipendelea vyama vya ushirika, wanunuzi binafsi, au njia mseto za kuuza mazao. Hakukuwa na tofauti kubwa ya maoni kati ya wakulima maskini na wale wenye nafuu kimaisha. Ni jambo la kutia moyo kuona kuwa karibu robo (23%) ya wakulima bado walipendelea kuuza mazao yao kwenye vyama vya ushirika pekee, na wengine 21% walipendelea mseto baina ya vyama vya ushirika na wanunuzi binafsi katika kuuza mazao, hali inayoonyesha kuwa wakulima - maskini na wasio maskini - hawakufurahishwa na kitendo cha kuanguka kwa mfumo wa vyama vya ushirika.

### 5.7 Mwelekeo wa Utoaji wa Huduma za Kilimo

Wakulima walizidi kuulizwa kuhusu mwelekeo walioouona katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita katika utoaji wa huduma za kilimo, iwe huduma hizo zilitolewa na serikali au watu binafsi.

**Jedwali 5.6 Mwelekeo wa Upatikanaji wa Huduma za Kilimo, Mabadiliko kwa Miaka Mitatu Iliyopita, kwa Kiwango cha Umaskini kwa Mtu Mmoja Mmoja**

| Upatikanaji wa Huduma za Kilimo | Wakulima Maskini Zaidi % | | | | Wakulima wa Daraja la Kati % | | | | Wakulima Wenye Nafuu Kimaisha % | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | KM | HM | HD | Sj | KM | HM | HD | Sj | KM | HM | HD | Sj |
| Upatikanaji wa mbolea | 7 | 31 | 31 | 31 | 11 | 32 | 32 | 25 | 21 | 32 | 30 | 17 |
| Bei ya mbolea | 2 | 24 | 36 | 38 | 2 | 24 | 44 | 29 | 5 | 25 | 50 | 21 |
| Upatikanaji wa dawa za kilimo za kemikali | 7 | 30 | 34 | 28 | 11 | 31 | 35 | 22 | 20 | 29 | 34 | 16 |
| Bei ya dawa za kilimo za kemikali | 2 | 22 | 43 | 33 | 3 | 25 | 47 | 26 | 6 | 24 | 51 | 19 |
| Upatikanaji wa mikopo | 3 | 21 | 40 | 37 | 4 | 23 | 42 | 32 | 7 | 23 | 41 | 28 |
| Gharama za mikopo | 0 | 15 | 27 | 57 | 2 | 15 | 32 | 52 | 2 | 16 | 31 | 51 |
| Utendaji wa bodi ya mazao | 1 | 15 | 9 | 75 | 1 | 19 | 10 | 70 | 1 | 16 | 12 | 71 |
| Utendaji wa wanunuzi binafsi | 5 | 25 | 33 | 38 | 7 | 30 | 35 | 31 | 8 | 25 | 35 | 32 |
| Utendaji wa vyama vya ushirika | 2 | 18 | 18 | 62 | 3 | 22 | 19 | 56 | 3 | 18 | 21 | 58 |
| Bei za mazao | 4 | 24 | 47 | 25 | 7 | 29 | 46 | 19 | 7 | 25 | 45 | 23 |
| Kodi / ushuru / makato | 6 | 35 | 19 | 40 | 7 | 36 | 21 | 36 | 9 | 36 | 16 | 39 |
| Ushauri wa kitaalamu | 9 | 36 | 41 | 14 | 13 | 37 | 33 | 17 | 12 | 33 | 36 | 19 |
| Upatikanaji wa habari za masoko | 5 | 35 | 32 | 28 | 6 | 37 | 31 | 26 | 6 | 34 | 35 | 25 |

**Ufunguo:** **KM** = Kuna Mabadiliko **HD =** Hali ni Duni Zaidi
**HM** = Hakuna Mabadiliko **Sj =** Sijui

| Jedwali 5.7 Mwelekeo wa Upatikanaji wa Huduma za Kilimo, Mabadiliko kwa Miaka Mitatu Iliyopita | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Huduma** | **Kuna Mabadiliko %** | **Hakuna Mabadiliko %** | **Hali ni Duni Zaidi %** | **Sijui %** |
| Upatikanaji wa mbolea | 13 | 31 | 31 | 24 |
| Bei ya mbolea | 3 | 24 | 43 | 30 |
| Upatikanaji wa dawa za kuua wadudu waharibifu / mimea / kuvu | 13 | 30 | 35 | 22 |
| Bei ya dawa za kuua wadudu waharibifu / mimea / kuvu | 4 | 23 | 47 | 26 |
| Upatikanaji wa mikopo | 4 | 22 | 41 | 33 |
| Gharama za mikopo (riba na ratiba ya kuirejesha) | 1 | 15 | 30 | 54 |
| Utendaji wa jumla wa bodi za uuzaji wa mazao nje ya nchi | 1 | 16 | 10 | 72 |
| Utendaji wa jumla wa wanunuzi binafsi wa mazao | 7 | 25 | 34 | 34 |
| Utendaji wa jumla wa vyama vya ushirika | 3 | 19 | 19 | 59 |
| Bei za kuuzia mazao / mifugo | 6 | 26 | 45 | 23 |
| Kodi / ushuru / makato mengine | 7 | 35 | 19 | 39 |
| Huduma za ushauri wa kitaalamu katika kilimo / ufugaji | 11 | 35 | 36 | 17 |
| Upatikanaji wa habari za masoko, bei | 6 | 35 | 33 | 26 |

Wakulima walio wengi ama waliona huduma, mawakala au masoko yaliyo mengi yakiwa hayapigi hatua kubwa za mabadiliko katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, au hawakutoa maoni yoyote. Kwa wale walioripoti kuwepo kwa mabadiliko, wengi zaidi miongoni mwao waliona kuwepo kwa mabadiliko hasi badala ya mabadiliko chanya. Wakulima maskini zaidi walikosoa zaidi mabadiliko hayo kulinganisha na wakulima wenye hali bora kimaisha. Chini ya 10% ya wakulima maskini walidai kuwepo kwa mabadiliko yaliyoleta hali bora. Kushuka kwa bei za kuuzia mazao na kupanda kwa bei za kununulia mbolea na madawa ya kilimo ni mambo yaliyolalamikiwa mara kwa mara na wakulima wa makundi yote matatu ya vipato. Kwa namna iliyo tofauti, baadhi ya wakulima wenye hali bora kimaisha walidai kulikuwepo kuboreshwa kwa hali ya upatikanaji wa mbolea na pembejeo nyingine za kemikali, na huduma za ushauri wa kitaalamu. Mabadiliko haya yalitajwa hata hivyo yalipingwa na idadi kubwa zaidi ya wakulima waliosema kulikuwa na hali ya kudorora kwa shughuli za kilimo.

## 5.8 Msaada wa Serikali kwa Wakulima

Licha ya sera ya serikali ya kusambaza pembejeo za kilimo zilizowekewa ruzuku, kuongeza shughuli za utafiti wa mazao na kuwashawishi wakulima kutumia matokeo ya tafiti hizi kupitia kwenye ushauri unaotolewa na wataalamu wa kilimo, 75% ya wakulima walidai kuwa serikali haiwapatii huduma yoyote ile. Aidha, kuna tofauti kubwa sana ya maoni miongoni mwa wakulima wa madaraja tofauti ya vipato, ambapo zaidi ya 82% ya wakulima maskini wanadai kuwa serikali haiwapi huduma yoyote kulinganisha na 66% ya wakulima wenye nafuu kimaisha.

| Jedwali 5.8 Msaada wa Serikali kwa Wakulima | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Msaada wa Serikali** | **Maskini Zaidi %** | **Daraja la Kati %** | **Wenye Nafuu Kimaisha %** | **Wote %** |
| Hakuna msaada | 82 | 76 | 66 | 75 |
| Huweka ruzuku kwenye mbolea | 1 | 5 | 15 | 7 |
| Husambaza mbegu zilizoboreshwa | 4 | 6 | 6 | 5 |
| Masoko | 2 | 4 | 3 | 3 |
| Hutoa mikopo | 1 | 1 | 1 | 1 |
| Ushauri wa kitaalamu | 1 | 3 | 2 | 2 |
| Mengineyo | 2 | 1 | 1 | 1 |
| Sijui / Hakuna jibu lililotolewa | 7 | 4 | 5 | 6 |

Mwishowe, kwenye swali lililowataka kutoa maoni yao, wakulima waliulizwa: “Ni jambo lipi moja muhimu zaidi ambalo serikali inaweza kulifanya ili kuwasaidia wakulima kama ninyi?” - Jedwali 5.9. Kwa idadi kubwa mno, jibu lililotolewa na wakulima wengi zaidi, 42%, lilikuwa kuboreshwa kwa upatikanaji wa pembejeo za kilimo, hususan mbolea. Hali hiyo inaeleweka, ukizingatia kwamba kuna mahitaji makubwa sana ya pembejeo za kilimo na ukweli kwamba tayari serikali imeonyesha dhamira ya kuongeza upatikanaji wa mbolea iliyowekewa ruzuku kwa ajili ya wakulima.

**Jedwali 5.9** **Msaada Kutoka Serikalini Wanaoupendelea kwa Wakulima Ili Kuongeza Uzalishaji Katika Kilimo**

| Misaada Inayopendelewa Kutoka Serikalini | Maskini Zaidi % | Daraja la Kati % | Matajiri % | Wote % |
|---|---|---|---|---|
| Kuongeza upatikanaji wa pembejeo | 43 | 42 | 42 | 42 |
| Mikopo | 21 | 19 | 16 | 19 |
| Zana za kilimo | 9 | 10 | 12 | 11 |
| Kutafuta, kuboresha masoko ya mazao | 8 | 7 | 7 | 7 |
| Hakuna jibu lililotolewa / Sijui / Sihitaji msaada wa serikali | 6 | 8 | 9 | 7 |
| Kuboresha elimu, ushauri wa kitaalamu | 7 | 7 | 7 | 7 |
| Mengineyo | 3 | 3 | 4 | 3 |
| Bei nzuri zaidi za mazao | 1 | 1 | 1 | 1 |
| Kuboresha miundombinu | 1 | 2 | 1 | 1 |
| Punguzo la kodi kwa wakulima | 1 | 1 | 1 | 1 |

## 5.9 Wafugaji na Wakulima Wanaojishughulisha na Ufugaji

Jumla ya wafugaji 616 walifanyiwa utafiti na kuulizwa maswali kuhusu masuala na matatizo sawa na yale waliyoulizwa wakulima. Mifugo ya kienyeji ambayo huchungwa au hujitafutia chakula yenyewe, kama vile ng'ombe, kondoo, mbuzi na kuku, ndiyo wanyama wanaofugwa zaidi na wafugaji hawa. Ng'ombe wa kienyeji ambao huchungwa kwenye maeneo ya wazi ni wanyama waliofugwa na 62% ya wafugaji waliosailiwa, mbuzi na kondoo walifugwa na 58% ya wafugaji, huku kuku wakifugwa na 56% ya wafugaji hao. Wafugaji wachache sana waliosailiwa walikuwa wakiifungia na kuiletea mifugo yao chakula nyumbani, 3%.

Wafugaji waliulizwa iwapo kulikuwa ma masuala mahususi yaliyokuwa yakitatiza shughuli zao za kujipatia riziki katika kipindi cha miezi kumi na miwili kabla ya kufanywa kwa utafiti huu.

**Jedwali 5.10** **Matatizo Yanayowakabili Wafugaji**

| Matatizo Yanayowakabili Wafugaji | Tatizo Kuu % | Tatizo Dogo % | Siyo Tatizo % | Hainihusu % |
|---|---|---|---|---|
| Bei ya madawa / huduma za mifugo | 78 | 8 | 11 | 3 |
| Ukosefu wa huduma za mifugo | 63 | 9 | 27 | 1 |
| Ushauri wa kitaalamu | 58 | 11 | 29 | 2 |
| Ukame | 54 | 15 | 27 | 3 |
| Magonjwa, wadudu na wanyama wanaoshambulia mifugo | 53 | 21 | 23 | 2 |
| Umbali wa kuyafikia masoko / gharama za usafirishaji | 49 | 14 | 28 | 9 |
| Bei ya kuuzia mifugo | 48 | 17 | 28 | 8 |
| Ukosefu wa maeneo ya malisho | 39 | 16 | 38 | 7 |
| Ukosefu wa habari za masoko | 38 | 19 | 36 | 7 |
| Huduma za vyama vya ushirika / vyama vya wakulima | 26 | 9 | 24 | 41 |
| Wizi na uhalifu | 22 | 19 | 57 | 1 |
| Udhibiti wa serikali za mitaa | 13 | 11 | 56 | 20 |
| Ushuru, kodi na makato | 13 | 14 | 44 | 30 |

‘Tatizo kuu’ lililotajwa na wafugaji walio wengi ni gharama kubwa za madawa na huduma za mifugo. Ukosefu wa huduma za mifugo na ushauri wa kitaalamu, ukame, magonjwa, umbali mrefu wa kuyafikia masoko, bei ndogo ya kuuzia mifugo yao, ukosefu wa maeneo ya malisho na ukosefu wa habari za masoko yalitajwa pia kuwa miongoni mwa matatizo yanayowakabili wafugaji.

Kama ilivyokuwa kwa wakulima, wafugaji pia waliulizwa iwapo walipata ushauri wa kitaalamu. Karibu 41% ya wafugaji waliosailiwa walipokea ushauri katika kipindi cha mwaka mmoja kabla ya kufanywa kwa utafiti huu, idadi ambayo ni kubwa sana katika kupata ushauri wa kitaalamu ikilinganishwa na ile ya wakulima. Hata hivyo, nusu ya wafugaji waliosailiwa walikuwa hawajawahi kamwe kupata ushauri wa kitaalamu. Maelezo yanayofuata yanatoa maoni ya washiriki kutoka maeneo ya wafugaji kuhusu kuwepo kwa urasimu katika kutenga maeneo kwa ajili ya shughuli za ufugaji na upatikanaji wa huduma za ushauri wa kitaalamu.

**SANDUKU 5**: **MATATIZO YA ARDHI NA USHAURI WA KITAALAMU KWA WAFUGAJI**

*“Maeneo ya kulima hakuna, ni machache mno. Matatizo tunayopata kuhusiana na upatikanaji wa ardhi ni ule urasimu wa kufuatilia kugawiwa ardhi. Mambo haya yanaanzia wilayani badala ya kuanzia maeneo ya kata na vijiji ambao wanafahamu matatizo yetu zaidi… Sisi wafugaji tunapata matatizo makubwa kutokana na uwekezaji wa makampuni makubwa na watu binafsi katika ardhi. Hawa ni kikwazo cha upatikanaji wa ardhi hapa kijijini kwetu.”*

• Kikundi Maalumu, Manyara

*“Mtaalamu aliyepo hapa ni wa serikali ila ukimhitaji ni mpaka umfuate na umlipe… Mshauri wa mifugo hapa hayupo kabisa ila ukihitaji ni mpaka uende mjini na ni mbali na utamleta kwa gharama zako. Hivyo ushauri kwa kilimo na mifugo ni adimu hapa.”*

• Kikundi Maalumu, Tanga.

Ingawa zaidi ya 40% ya wafugaji waliarifu kuwa walipata ushauri wa kitaalamu, walipoulizwa kuhusu mambo ambayo serikali inayafanya katika kuwasaidia, 76% walisema serikali haikuwa ikifanya chochote cha kuwasaidia (Jedwali 5.11). Wafugaji wachache tu ndiyo waliotaja huduma ya ushauri wa kitaalamu. Hii inamaanisha kuwa ama huduma hizi hazithaminiwi sana au kwamba zinatolewa na sekta binafsi au asasi zisizo za kiserikali. Hali hii pengine inamaanisha kuwa wataalamu kutoka serikalini huonekana pale tu kunapokuwa na mlipuko wa magonjwa ya wanyama (kama vile Homa ya Bonde la Ufa) na si kwa ajili ya kutoa ushauri wa kitaalamu kwa wafugaji kila wakati. Walipoulizwa ni jambo lipi serikali inapaswa kulifanya ili kuwasaidia wafugaji, jibu lililotolewa mara kwa mara na wafugaji wapatao theluthi moja ya wale waliosailiwa lilikuwa kuongezwa kwa upatikanaji wa huduma za chanjo na madawa ya mifugo, na kusema kuwa wao (kama walivyosema pia wakulima) bado wanaichukulia serikali kuwa ndiyo mhusika mkuu katika kusambaza huduma za mifugo.

**Jedwali 5.11** **Msaada wa Serikali katika Kuboresha Shughuli za Ufugaji**

| Msaada Unaotolewa na Serikali | % |
|---|---|
| Hakuna | 76 |
| Ushauri wa kitaalamu | 9 |
| Punguzo la bei za madawa ya mifugo | 4 |
| Mengineyo | 3 |
| Mikopo ili kununua mifugo | 3 |
| Hakuna jibu lililotolewa | 4 |

| **Jedwali 5.12** Msaada kutoka Serikalini Wanaoupendelea Wafugaji | |
|---|---|
| **Msaada Wanaoupendelea Wafugaji** | **%** |
| Kuongeza upatikanaji wa chanjo na madawa ya mifugo | 31 |
| Ushauri wa kitaalamu | 16 |
| Tiba ya mifugo | 13 |
| Majosho | 11 |
| Mikopo | 9 |
| Hakuna jibu lililotolewa | 7 |
| Kupunguza bei, kutoa madawa bure | 6 |
| Mengineyo | 6 |

## 5.10 Wavuvi

Utafiti huu uliomba maoni kutoka kwa wavuvi 32 wa maji chumvi na 42 wa maji baridi kuhusu shughuli zao za kujipatia riziki. Theluthi moja tu ya wavuvi hawa ndio waliokuwa wakiifanya kazi hii kama kazi ya kudumu, na waliobaki walijishughulisha pia na kilimo, ufugaji, au biashara ndogondogo. Wengi wao, 76%, walikuwa wanamiliki, wanachangia, au wanakodi mitumbwi kwa ajili ya shughuli zao za uvuvi. Wakati zaidi ya nusu ya wavuvi (57%) walimiliki, kuchangia au kukodi nyavu za kuvulia samaki, kuna wachache sana waliomiliki zana nyingine yoyote ya uvuvi. Walio wengi, 72%, walifanya shughuli za uvuvi kwa kushirikiana na mvuvi mwingine mmoja au zaidi.

Walipoulizwa kuhusu mwelekeo wa upatikanaji wa samaki, 70% walisema kiwango cha upatikanaji wa samaki kilikuwa kinashuka, na 16% tu ndiyo waliosema kuwa kiwango kilikuwa kinaongezeka. Kwa waliosema kuwa upatikanaji wa samaki ulikuwa ukipungua, nusu yao (51%) walisema sababu ilikuwa ni kuwepo kwa wavuvi wadogo wengi kupita kiasi, ingawa nusu nyingine hawakukubaliana nao kuwa hii ndiyo iliyokuwa sababu. Kulikuwepo pia kutofautiana kwa maoni iwapo wavuvi wanaotumia nyavu zenye matundu madogo madogo ndio waliokuwa wakisababisha ukosefu wa samaki. Wavuvi wachache zaidi walitaja uvuvi wa kibiashara, ujio wa wavuvi kutoka maeneo mengine, na matumizi ya baruti kama sababu za kushuka kwa mavuno ya samaki. Walipoulizwa kuhusu matatizo yanayowakabili wavuvi, karibu nusu (47%) walisema kuwa matumizi ya 'nyavu za mtando' husababisha matatizo. Kisanduku Namba 6 kinaonyesha baadhi ya maoni kuhusu matatizo yanayowakabili wavuvi.

**SANDUKU 6**: **VIKWAZO KATIKA UVUVI**

*"Samaki wanapungua sana, kila siku wanapungua sana. Hali imeshuka kupita kiasi – kwa uvuvi wa mishipi. Sababu: Tuliingiliwa na uvuvi endelevu unaitwa mtando."*
• Kikundi Maalumu, Lindi

*"Serikali inalazimisha tukavue vina virefu wakati nyavu zetu ni chakavu, na boti tunazotumia ni zile za kuendesha kwa mkono hivyo kuongeza umaskini hapa kwetu."*
• Kikundi Maalumu, Tanga

Walipoulizwa iwapo wanapendelea kuuza samaki nje ya nchi au kuuza kwa masoko ya ndani pekee, wavuvi wengi - 53%, walipendelea kuuza nje huku 38% wakipendelea soko la ndani. Sababu kubwa iliyotajwa na walio wengi ni mapato makubwa yanayotokana na mauzo ya bidhaa nje ya nchi ikilinganishwa na mauzo ya ndani.

Mwishowe, wavuvi waliulizwa (swali lililowataka kutoa maoni yao) kuwa ni msaada upi ambao serikali inautoa katika kuboresha shughuli za uvuvi na serikali ifanye nini ili kusaidia kuboresha shughuli za uvuvi. Zaidi ya 80% ya wavuvi waliosailiwa walisema kuwa serikali haifanyi chochote katika kuboresha shughuli za uvuvi huku idadi ndogo tu, 5%, wakitaja kuzuiwa kwa matumizi ya nyavu zenye matundu madogo. Jedwali 5.13 linaonyesha maoni kuhusu aina ya misaada kutoka serikalini inayopendelewa na wavuvi ili kuboresha uvuvi. Wavuvi walio wengi walijibu kwamba wangependa serikali iwapatie vitendea kazi kama vile injini na nyavu, huku wachache tu ndio wakitaja 'elimu', jukumu ambalo ni dhahiri kabisa serikali inabidi ilitekeleze.

| Jedwali 5.13 Msaada kutoka Serikalini Wanaoupendelea Wavuvi Kuboresha Viwanda vya Samaki | |
|---|---|
| **Msaada Inayohitajiwa kutoka Serikalini** | **%** |
| Kuwapa wavuvi zana za uvuvi (nyavu) | 34 |
| Kuwapa wavuvi injini za boti / mitumbwi | 22 |
| Sijui / Hakuna jibu lililotolewa | 14 |
| Mikopo | 9 |
| Mengineyo | 9 |
| Elimu kuhusu ufugaji na hifadhi ya samaki | 8 |
| Kuzuia uvuvi haramu | 4 |

## 5.11 Matumizi ya Maliasili

Katika kuhitimisha masuala yahusuyo shughuli za kujipatia riziki vijijini, wakazi wa vijijini waliulizwa maswali kadhaa kuhusu namna wanavyotumia maliasili katika kuboresha maisha yao.

| Jedwali 5.14 Matumizi ya Maliasili | | | |
|---|---|---|---|
| **Maliasili** | **Hupata Bure %** | **Hununua %** | **Hawatumii %** |
| Nyasi / makuti kwa kuezekea | 42 | 35 | 23 |
| Miti ya kujengea nyumba | 32 | 54 | 14 |
| Mitishamba kwa ajili ya dawa | 31 | 40 | 29 |
| Matunda pori, jamii ya njugu, asali, matunguu | 27 | 42 | 31 |
| Ukindu wa kusukia mikeka, matandiko | 20 | 51 | 29 |
| Miti ya kujengea maboma, ua wa kuzunguka shamba | 10 | 38 | 52 |
| Vyombo vya nyumbani na vya kuhifadhia | 9 | 76 | 15 |
| Miti / mbao za kutengenezea vigoda, viti, meza, vitanda | 7 | 83 | 10 |
| Nyama ya wanyama pori | 6 | 22 | 72 |
| Samaki | 3 | 84 | 13 |
| Miti / mbao za kutengenezea mitumbwi, ngalawa, mashua / boti | 2 | 6 | 92 |
| Ala za muziki | 2 | 15 | 83 |
| Vifaa vya uchongaji na sanaa za mikono | 2 | 19 | 79 |

Nyasi / makuti kwa ajili ya kuezekea nyumba, stoo na mabanda mara nyingi hupatikana bure pasipo gharama yoyote. Karibu 20% hadi 32% ya wananchi waliosailiwa walijipatia bure chakula mwitu na ukindu, dawa za mitishamba na miti ya kujengea, huku 40% hadi 54% ya wananchi waliosailiwa walinunua vitu hivi. Wakazi wachache tu wa mijini ndio walioweza kujipatia bure badala ya kununua baadhi ya maliasili hizi (kama vile mbao / miti, vyombo vya nyumbani, samaki, nyama pori, ala za muziki, vifaa vya sanaa ya uchongaji).

# VYANZO VYA RIZIKI KWA VIJANA

Jumla ya vijana 974 wenye umri wa miaka 15 hadi 24 waliokuwa tayari wamemaliza masomo yao shuleni waliulizwa maswali kuhusu kazi wanazozifanya ili kuendesha maisha yao na matatizo makuu wanayokumbana nayo. Kulikuwa na vijana 620 wa kike na 354 wa kiume.

## 6.1 Hali ya Uchumi kwa Vijana

Awali, yalirekodiwa maelezo mafupi yahusuyo kazi wanazozifanya vijana ambao tayari wamemaliza shule, kama ilivyoonyeshwa katika Jedwali 6.1. Karibu theluthi moja ya vijana, 35%, hawakuwa na ajira, mara nyingi wakiishi nyumbani na wazazi wao au ndugu zao. Vijana wengine 31% wa kiume na 23% wa kike walikuwa wanafanya kazi za vijijini na 34% ya vijana wa kiume na 23% ya vijana wa kike walisema walikuwa na ajira, ambapo karibu nusu yao walikuwa wamejiajiri wenyewe. Ingawa idadi ndogo tu ya vijana wa kike waliosailiwa ndio waliokuwa wanafanya ‘kazi za vijijini’ (hususan kilimo), inawezekana kwamba idadi kubwa tu ya wale waliojibainisha kuwa ‘wafanyakazi wa nyumbani’ au ‘mama wa nyumbani’ walikuwa wanajishughulisha na kilimo pia.

**Jedwali 6.1** Hali ya Uchumi kwa Vijana Kijinsia

| Hali ya Uchumi | Wa Kiume % | Wa Kike % | Wote % |
|---|---|---|---|
| Wasio na ajira | 33 | 35 | 35 |
| Kazi za vijijini | 31 | 23 | 26 |
| Waliojiajiri | 13 | 10 | 11 |
| Wafanyakazi wa nyumbani | 2 | 16 | 11 |
| Vibarua / wafanyakazi wa muda | 11 | 5 | 7 |
| Waajiriwa | 7 | 6 | 6 |
| Waliojiari na wenye waajiriwa | 3 | 2 | 2 |
| Wengineo | 1 | 2 | 2 |

## 6.2 Mwelekeo wa Hali yao ya Uchumi

Vijana waliomaliza shule waliulizwa kuhusu mabadiliko ya hali yao kiuchumi ikilinganishwa na ile waliyokuwa nayo miaka mitatu iliyopita. Majibu ya walio wengi, karibu 39%, ni kwamba hali yao haikuwa imebadilika (Jedwali 6.2). Kwa ujumla, 32% ya vijana waliomaliza shule wanaichukulia hali yao kiuchumi kuwa imeshuka katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita (imeshuka sana au imeshuka kidogo) na 26% wanaona kuwa imeimarika. Maoni ya vijana wa kike na wa kiume yalikaribia kufanana.

**Jedwali 6.2** Mwelekeo wa Hali ya Uchumi kwa Vijana

| Mabadiliko ya Hali ya Uchumi kwa Miaka Mitatu Iliyopita | Dar es Salaam % | Miji Mingine % | Vijijini % | Wa Kiume % | Wa Kike % | Wote % |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Imeshuka sana | 15 | 18 | 15 | 19 | 18 | 18 |
| Imeshuka kidogo | 14 | 13 | 14 | 13 | 14 | 14 |
| Haijabadilika | 40 | 31 | 41 | 39 | 38 | 39 |
| Imeimarika kidogo | 27 | 32 | 27 | 27 | 24 | 25 |
| Imeimarika sana | 1 | 1 | 1 | 0 | 2 | 1 |
| Sijui / Hakuna jibu lililotolewa | 2 | 5 | 3 | 3 | 4 | 4 |

Walipoulizwa kubainisha mabadiliko yao kiuchumi kwa siku za karibuni, 79% ya vijana waliosailiwa hawakuweza kutaja mabadiliko yoyote. Vijana wa kike walielekea zaidi kusema ‘hakuna mabadiliko’ kuliko vijana wa kiume (Jedwali 6.3).

| **Jedwali 6.3** Mabadiliko ya Siku za Karibuni katika Maisha ya Vijana | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mabadiliko Makubwa** | Dar es Salaam % | Miji Mingine % | Vijijini % | Wa Kiume % | Wa Kike % | Wote % |
| Hakuna mabadiliko | 75 | 79 | 83 | 75 | 82 | 79 |
| Kipato kimeongezeka | 8 | 4 | 5 | 8 | 5 | 6 |
| Nimenunua bidhaa za kudumu | 7 | 7 | 3 | 7 | 4 | 5 |
| Nimemaliza shule | 5 | 6 | 3 | 5 | 4 | 5 |
| Mengineyo | 5 | 3 | 4 | 3 | 5 | 4 |
| Nimenunua shamba / kiwanja | 1 | 1 | 2 | 2 | 1 | 1 |

Matarajio ya vijana kiuchumi yanaonyeshwa katika Jedwali 6.4. Karibu robo ya vijana wa kiume (23%) na 31% ya vijana wa kike hawakuwa na uhakika. Kwa wale waliotoa maoni yao, wengi wao - 70% kwa vijana wa kiume na 66% kwa vijana wa kike - walitarajia kupata maisha mazuri zaidi katika kipindi cha miaka mitatu ijayo. Kulikuwa na tofauti ndogo sana ya maoni kati ya vijana wa mijini na wale wa vijijini.

| **Jedwali 6.4** Matarajio ya Vijana Kiuchumi | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Matarajio ya Kiuchumi kwa Miaka Mitatu Ijayo** | Dar es Salaam % | Miji Mingine % | Vijijini % | Wa Kiume % | Wa Kike % | Wote % |
| Hali itakuwa mbaya zaidi | 6 | 8 | 5 | 6 | 4 | 5 |
| Hali itakuwa mbaya kidogo | 2 | 2 | 2 | 3 | 2 | 3 |
| Hali itabaki vilevile | 19 | 15 | 19 | 13 | 18 | 16 |
| Hali itakuwa nzuri kidogo | 38 | 36 | 37 | 43 | 34 | 37 |
| Hali itakuwa bora zaidi | 12 | 14 | 11 | 11 | 12 | 12 |
| Sijui / Hakuna jibu lililotolewa | 25 | 26 | 25 | 23 | 31 | 28 |

## 6.3 Matatizo Yanayowakabili Vijana

Kupata kazi ni tatizo kubwa lililowaumiza vichwa vijana nchini kote, kama ilivyoonyeshwa na 63% ya vijana waliosailiwa (Jedwali 6.5). Wengi walisema kuwa wangeendelea na masomo yao kama wangepata rasilimali. Baadhi ya mambo yalibainishwa kuwa ni matatizo ‘makubwa’, lakini hakuna hata moja miongoni mwa hayo lililotajwa na vijana walio wengi. Kama yalivyokuwa majibu ya ndugu zao wenye umri wa utu uzima, baadhi ya vijana (47%) pia yalitaja kuwa gharama za maisha, ambazo zilipimwa kwa kuangalia bei ya chakula na bidhaa nyingine za msingi kuwa ni tatizo kubwa; na wengine (39%) walitaja kipato kidogo kuwa ni tatizo kubwa. Aidha, idadi kubwa ya vijana, hususan wa vijijini, walilalamikia hali mbaya ya barabara na ukosefu wa mikopo na matatizo ya huduma ya maji.

Kwa ujumla, hakukuwa na tofauti kubwa sana ya maoni kati ya wavulana na wasichana ingawa wavulana walilalamika zaidi kuhusu kazi, mazingira ya kufanyia kazi na kipato ikilinganishwa na wasichana.

| **Jedwali 6.5** Matatizo Yanayowakabili Vijana | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Matatizo Makuu** | Dar es Salaam % | Miji Mingine % | Vijijini % | Kote % |
| Upatikanaji wa kazi | 63 | 67 | 61 | 63 |
| Bei kubwa ya chakula na bidhaa nyingine za msingi | 46 | 45 | 48 | 47 |
| Mazingira duni ya kazi / kipato kidogo | 36 | 40 | 40 | 39 |
| Hali ya barabara zinazotumiwa mara nyingi | 37 | 52 | 69 | 54 |
| Upatikanaji wa mikopo | 41 | 47 | 51 | 47 |
| Maji kwa kilimo na mifugo | 8 | 26 | 44 | 27 |
| Upatikanaji wa ardhi na pembejeo za kilimo | 8 | 33 | 39 | 26 |

# KULINGANISHA NA MATOKEO MENGINE YA UTAFITI WA MWAKA 2003 NA 2007 KUHUSU KUKUZA UCHUMI NA KUPUNGUZA UMASKINI

Sura hii inaripoti ulinganifu mpana wa taarifa ya matokeo ya Utafiti wa Maoni ya Watu na yale ya Utafiti wa Sera na Utoshelevu wa Huduma uliofanywa Septemba 2003 (REPOA, 2003). Jedwali 7.1 linazungumzia masuala yanayohusiana na kukuza uchumi na kupunguza umaskini wa kipato.

Tafiti hizi zina matokeo yanayofanana hasa katika idadi ya wananchi wanaoona kuwa hali yao kiuchumi imedorora. Bei kubwa ya chakula na bidhaa nyingine muhimu ni matatizo mawili makubwa yaliyobainishwa na tafiti zote mbili, ingawa idadi ya watu waliosema hivyo ni kubwa zaidi katika utafiti huu - 67% kwa bei ya chakula na 69% kwa bei ya bidhaa nyingine muhimu - ikilinganishwa na idadi ya watu waliosema hivyo katika Utafiti wa Sera na Utoshelevu wa Huduma - 63% kwa bei ya chakula na 58% kwa bei ya bidhaa nyingine muhimu. Inaonekana dhahiri kuwa watu wengi wanaona ongezeko kubwa la bei ya bidhaa isiyo chakula.

Tafiti zote mbili zinaonyesha kuwepo kwa kiwango kidogo sana cha fursa za ajira, hususan mijini.

Matatizo kuhusu upatikanaji na bei kubwa ya kuni na mkaa yanatajwa kuwa yameongezeka katika kipindi cha miaka minne iliyopita, na katika utafiti wa mwaka 2007, zaidi ya nusu ya watu wazima waliosailiwa walilitaja jambo hili kuwa ni tatizo kubwa.

**Jedwali 7.1 Matatizo Makuu kwa Madaraja kama Yalivyoripotiwa Mwaka 2003 na 2007**

| Dar es Salaam | | Maeneo ya Vijijini | | Kote | |
|---|---|---|---|---|---|
| 2003 | 2007 | 2003 | 2007 | 2003 | 2007 |
| Bei ya chakula | Bei ya chakula | Bei ya chakula | Barabara | Bei ya chakula | Bidhaa za msingi |
| Ajira | Bidhaa za msingi | Bidhaa za msingi | Bidhaa za msingi | Bidhaa za msingi | Bei ya chakula |
| Bidhaa za msingi | Kazi | Ukame | Bei ya chakula | Ajira | Barabara |
| Kodi ya nyumba | Kuni | Ajira | Kuni | Ukame | Ajira |
| - | Umeme | Kuni | Masoko / huduma | Kuni | Kuni |
| - | - | Masoko / huduma | Umeme | Masoko / huduma | Umeme |

**Angalizo:** 'Masoko / huduma' humaanisha umbali / upatikanaji
Utafiti wa Sera na Utoshelevu wa Huduma (2003) ulihoji wakuu wa kaya; Utafiti wa Maoni ya Watu (2007) ulihoji watu wazima wanaume kwa wanawake.
Mwaka 2003 utafiti uliendeshwa katika mikoa mbalimbali

Matokeo ya utafiti wa *Pew Global Attitudes Project* (Aprili 2007)[4] yanaonyesha kuwa 52% ya Watanzania waliosailiwa kitaifa waliichukulia hali yao kiuchumi wakati huo kuwa 'nzuri' au 'nzuri sana' kulinganisha na 47% walioichukulia kuwa 'mbaya' au 'mbaya sana'. Idadi kubwa kidogo ya wananchi waliosailiwa walisema kwamba walikuwa na hali bora zaidi miaka mitano iliyopita kuliko sasa, 38%, kulinganisha na 34% waliosema kinyume chake. Katika utafiti huo wa Pew, karibu nusu ya watu waliosailiwa (46%) walidhani kwamba watu wa kizazi kijacho watapata shida zaidi kuliko wale wa kizazi cha sasa, wakati 36% walisema watakuwa na hali bora zaidi.

4 Rejea tovuti: www.pewglobal.org kwa taarifa za utafiti

Jambo lingine muhimu linalotokana na kulinganisha matokeo ya tafiti hizi linahusu umiliki wa simu, hususan simu za mkononi. Kwa kulinganisha na matokeo ya Utafiti wa Sera na Utoshelevu wa Huduma (2003), inaonyesha kuwa idadi ya wananchi wanaomiliki simu imeongezeka zaidi ya mara nne, kutoka 8% mwaka 2003 hadi 35% mwaka 2007.

Hata hivyo, maoni kuhusu hali aliyonayo mtu huathiriwa na watu wengine wanaomzunguka. Watu wanapoona wenzao wanapiga hatua za maendeleo haraka kuliko wao, wanaweza kuchukulia kuwa hali yao imeshuka (ingawa ni kweli kushuka huko kunaweza kuwa ni kwa hadhi au 'mtu kujishusha pindi anapojilinganisha na mwenzake'). Kwa hakika, kuongezeka kwa hali ya kutokuwepo usawa miongoni mwa watu kunaweza hata kudhoofisha hatua za dhati zilizopigwa katika kuboresha hali ya maisha. Utafiti wa Sera na Utoshelevu wa Huduma (2003) pamoja na tafiti nyingine nyingi zinaonyesha kuwa Watanzania wengi mno wanaona kuwa kuna ongezeko la hali ya kutokuwepo kwa usawa miongoni mwa watu. Katika utafiti wa Maoni ya Watu (2007), kwa kila Mtanzania mmoja mwenye umri wa utu uzima anayeona kuimarika kwa hali yake kimaisha, kuna wengine wawili wanaoona kuwa hali yao imekuwa duni zaidi.

Hata hivyo, kiwango halisi cha umaskini katika kaya na hali ya kutokuwepo kwa usawa miongoni mwa watu hakiwezi kubainishwa katika utafiti huu. Takwimu za Utafiti wa Bajeti ya Kaya zinaonyesha kuwa hali ya kutokuwepo kwa usawa miongoni mwa watu iliongezeka kidogo kwenye muongo ulioanzia mwaka 1992 hadi 2002, huku kukiwa na tofauti ndogo katika maeneo ya vijijini na tofauti kubwa zaidi jijini Dar es Salaam (Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 2002). Takwimu zaidi kuhusu hali ya kutokuwepo kwa usawa miongoni mwa watu zitapatikana katika Utafiti wa Bajeti ya Kaya (2007) unaofanywa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu.

Utafiti wa Maoni ya Watu (2007) na ule unaojaziliza wa Maoni ya Watoto ulitafuta maoni ya vijana na watoto. Vijana walioshiriki katika utafiti huu, wenye umri wa miaka 15-24, wana matumaini mema kwa maisha yao ya baadaye. Itakuwa muhimu iwapo tafiti linganishi za siku zijazo zitaweza kutathmini kiwango cha mafanikio kilichofikiwa katika kukidhi matumaini haya mema na jinsi matumaini haya yanavyoweza kuhusishwa na mambo mema.

# SEHEMU YA PILI:

## MKUKUTA KUNDI LA II

MAISHA BORA NA USTAWI WA JAMII

# ELIMU YA MSINGI NA SEKONDARI

Utafiti wa Maoni ya Watu (2007) ulichunguza hali ya elimu hususan kwa kutumia mtazamo wa watoto na vijana. Hali kadhalika, watu wazima nao walichangia maoni yao kuhusu elimu kutokana na maswali ya jumla waliyoulizwa kuhusu hali ya huduma za jamii. Pamoja na uzoefu wao katika elimu, watoto wa shule waliulizwa pia kuhusu shughuli zao za nyumbani na shughuli nyingine wanazozifanya mbali na masomo, ushiriki wao katika masuala ya jamii, na matumaini waliyo nayo kwa siku za baadaye. Mfumo wa usimamizi wa MKUKUTA unaangalia zaidi kiwango cha ufanisi kilichofikiwa kwa kutumia vigezo vya idadi au vitu vinavyoweza kuonekana kwa macho - vitabu, vyumba vya madarasa - na pia wanafunzi walioandikishwa na matokeo ya mitihani. Utafiti wa 'Maoni ya Watoto' ulitoa pia fursa ya kuchunguza zaidi vigezo vya ubora kuhusu uzoefu walio nao wanafunzi katika masuala ya kujifunza na kufundishwa, masuala ambayo yatazungumziwa katika sura hii.

Vipengele vinavyofuata vinaeleza kuhusu majibu waliyoyatoa vijana wenye umri wa miaka 15-24 waliokuwa bado wanasoma shule. Kipengele kingine kitakachofuatia baadaye kinaripoti maoni ya wanafunzi wa shule ya msingi wenye umri mdogo zaidi.

Jumla ya wanafunzi 561 wenye umri wa miaka 15 na kuendelea waliulizwa maswali kuhusu masuala mbalimbali ya kielimu. Idadi ya wavulana waliosailiwa ilikuwa kubwa kidogo kuliko ya wasichana. Wengi wa wanafunzi wa vijijini walikuwa wanasoma shule ya msingi, huku wanafunzi wengi wa mjini walisoma shule ya sekondari.

## 8.1 Kwenda Shuleni

Asilimia 90 ya wanafunzi wa shule ya msingi wenye umri wa miaka 15 na kuendelea, walisema kuwa huenda shule kwa miguu, kama wafanyavyo karibu nusu ya wanafunzi wa shule ya sekondari waliosailiwa katika utafiti huu. Karibu theluthi moja ya wanafunzi wote wa Dar es Salaam husafiri kwa mabasi ya abiria waendapo shule. Kwa kuwa shule za msingi ziko karibu, 75% ya wanafunzi wa shule ya msingi hutumia muda usiozidi nusu saa kufika shuleni, huku 40% ya wanafunzi wa shule ya sekondari hutumia zaidi ya nusu saa ingawa wengi wao husafiri kwa basi.

**Jedwali 8.1** Kwenda Shuleni

| Usafiri wa Kwenda Shuleni | Shule ya Msingi | | Shule ya Sekondari | | Wote % |
|---|---|---|---|---|---|
| | Wavulana % | Wasichana % | Wavulana % | Wasichana % | |
| Kutembea | 88 | 92 | 49 | 47 | 68 |
| Basi la shule | 3 | 5 | 29 | 35 | 19 |
| Usafiri binafsi | 6 | 2 | 14 | 12 | 9 |
| Mabasi ya abiria | 3 | 1 | 8 | 7 | 5 |

## 8.2 Vyumba vya Madarasa

Zaidi ya nusu ya vijana waliosailiwa ambao bado wanasoma shule walisema kulikuwa na vyumba vya madarasa vya kutosha. Maoni ya kuwepo upungufu wa vyumba vya madarasa yanafanana miongoni mwa wavulana na wasichana wa shule ya msingi huku karibu robo ya watu waliosailiwa wakisema kuna haja ya vyumba zaidi vya madarasa. Hata hivyo, wasichana wa shule za sekondari walilalamika zaidi kuliko wavulana kuhusu upungufu huo.

| **Jedwali 8.2** Utoshelevu wa Vyumba vya Madarasa | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Utoshelevu wa Vyumba vya Madarasa** | **Shule ya Msingi** | | **Shule ya Sekondari** | | **Wote %** |
| | **Wavulana %** | **Wasichana %** | **Wavulana %** | **Wasichana %** | |
| Ndiyo, vinatosheleza | 61 | 58 | 55 | 45 | 55 |
| Mikondo kadhaa tofauti hutumia chumba kimoja | 14 | 14 | 18 | 20 | 17 |
| Mikondo mingi tofauti hutumia chumba kimoja | 4 | 7 | 8 | 8 | 6 |
| Havitoshelezi. Tunahitaji vyumba vingi zaidi vya madarasa | 22 | 21 | 19 | 27 | 22 |

Hali ya upungufu wa madawati ilifanana na ile ya upungufu wa vyumba vya madarasa, huku upungufu mkubwa zaidi ukitajwa na watu wa mijini na pia wanafunzi wa shule ya sekondari, hususan wanafunzi wa kike.

Zaidi ya nusu (54 %) ya wanafunzi waliosailiwa waliona kuimarika kwa hali ya vyumba vya madarasa, na 34% hawakuona mabadiliko yoyote tofauti na hali iliyokuwepo awali (Jedwali 8.3). Wanafunzi wa shule ya msingi waliona kuwepo kwa mabadiliko makubwa zaidi kuliko wanafunzi wa shule ya sekondari.

| **Jedwali 8.3** Mabadiliko ya Hali ya Vyumba vya Madarasa | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Hali ya Vyumba vya Madarasa** | **Shule ya Msingi** | | **Shule ya Sekondari** | | **Wote %** |
| | **Wavulana %** | **Wasichana %** | **Wavulana %** | **Wasichana %** | |
| Madarasa yanapendeza zaidi kuliko zamani | 58 | 62 | 48 | 48 | 54 |
| Hali ya madarasa ni ileile | 28 | 26 | 39 | 42 | 34 |
| Hali ya madarasa ni mbaya zaidi kuliko zamani | 11 | 9 | 9 | 5 | 8 |
| Sijui / Hakuna jibu lililotolewa | 3 | 2 | 4 | 5 | 4 |

### 8.3 Vitabu vya Kiada

Karibu 66% ya vijana wanaosoma shule walisema kuwa vitabu vya kiada vilikuwa vichache au kwamba huvitumia kwa nadra sana, na 16% ya wavulana wa shule ya sekondari na 19% ya wasichana wa shule ya sekondari walidai kuwa husoma masomo yao bila kutumia vitabu vya kiada hata kidogo. Kuna upungufu zaidi wa vitabu vya kiada katika maeneo ya vijijini kuliko maeneo ya mijini, lakini hata jijini Dar es Salaam, 61% ya watu waliosailiwa hawakuridhishwa na hali ya usambazaji wa vitabu vya kiada

| **Jedwali 8.4** Upatikanaji wa Vitabu vya Kiada | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Upatikanaji wa Vitabu** | **Shule ya Msingi** | | **Shule ya Sekondari** | | **Wote %** |
| | **Wavulana %** | **Wasichana %** | **Wavulana %** | **Wasichana %** | |
| Vitabu vipo kwa wingi | 23 | 26 | 23 | 17 | 22 |
| Kuna vitabu vichache | 52 | 51 | 40 | 41 | 45 |
| Tunatumia vitabu kwa nadra | 20 | 16 | 21 | 23 | 21 |
| Hakuna vitabu | 4 | 7 | 16 | 19 | 12 |

### 8.4 Vyoo

Kwa ujumla, upungufu wa vyoo haukuripotiwa katika shule za msingi au za sekondari, ingawa hali ilikuwa mbaya zaidi vijijini kuliko mijini. Wengi walidai kuwa vyoo vilikuwa safi, huku kwa kiwango cha juu vyoo vya shule za sekondari vikidaiwa kuwa safi zaidi ya vyoo vya shule za msingi.

**Jedwali 8.5** Utoshelevu wa Vyoo vya Shule

| Hali ya Vyoo | Shule ya Msingi | | Shule ya Sekondari | | Wote % |
|---|---|---|---|---|---|
| | Wavulana % | Wasichana % | Wavulana % | Wasichana % | |
| Vyoo vipo kwa wingi | 47 | 48 | 36 | 40 | 43 |
| Kuna vyoo vichache sana | 36 | 36 | 45 | 46 | 41 |
| Kuna choo kimoja au viwili tu | 12 | 10 | 19 | 11 | 13 |
| Hakuna vyoo | 4 | 7 | 0 | 3 | 3 |

### 8.5 Kompyuta

Taarifa zilitafutwa pia kuhusu upatikanaji na utumiaji wa kompyuta shuleni. Kulikuwa na kiwango kidogo sana cha matumizi ya kompyuta, hususan katika shule za msingi ambako 90% ya wanafunzi wenye umri mkubwa walisema hakukuwa na kompyuta katika shule zao. Zaidi ya nusu ya wanafunzi wa shule ya sekondari waliosailiwa (55%) walisema hakukuwa na kompyuta katika shule zao, na kwa wale waliosema kuwa kulikuwa na kompyuta shuleni kwao, ilidaiwa kuwa kompyuta hizo zilitumiwa zaidi kwa kazi za kiutawala na siyo kwa matumizi ya wanafunzi.

**Jedwali 8.6** Upatikanaji na Utumiaji wa Kompyuta

| Upatikanaji na Utumiaji wa Kompyuta | Shule ya Msingi | | Shule ya Sekondari | | Wote % |
|---|---|---|---|---|---|
| | Wavulana % | Wasichana % | Wavulana % | Wasichana % | |
| Kwa wanafunzi wote | 2 | 3 | 14 | 12 | 8 |
| Kwa wanafunzi wakubwa tu | 1 | 2 | 9 | 5 | 5 |
| Kwa utawala tu | 8 | 3 | 20 | 27 | 15 |
| Hakuna kompyuta | 88 | 91 | 58 | 55 | 72 |
| Sijui / Hakuna jibu lililotolewa | 1 | 1 | 0 | 1 | 0 |

### 8.6 Mahudhurio ya Wanafunzi Shuleni

Watoto waliripoti kuwa hukosa kuhudhuria masomo shuleni kwa nadra. Zaidi ya 70% ya vijana wanaosoma walisema kuwa 'kamwe' hawakosi kuhudhuria masomo shuleni au hukosa 'kwa nadra', na 20% tu ndio waliosema kuwa 'wakati mwingine' hukosa kuhudhuria shule, na 9% walisema 'mara kwa mara'. Hakukuwa na tofauti kubwa ya majibu baina ya wanafunzi wa kike na wa kiume. Pindi wanapokosa kuhudhuria masomo shuleni, kwa kiwango kikubwa 'ugonjwa' ndiyo sababu kuu ya kutohudhuria kwa wanafunzi wote wakubwa wa shule ya msingi na sekondari (kwa 61% ya waliosailiwa), huku wengi zaidi wakiwa wa vijijini kuliko wa mijini. 'Sina fedha ya ada ya shule' ni sababu kubwa iliyofuatia kwa kutajwa na wanafunzi wengi, ikitajwa na 36% ya wanafunzi wa sekondari, ambao gharama zao za masomo ni kubwa zaidi kuliko zile za shule ya msingi. Dharura ya harusi na mazishi pia huwachukulia wanafunzi muda wao, kwani sababu hii ilitajwa na 41% ya wasichana wa shule ya sekondari na 31% ya wavulana wa shule ya sekondari.

| **Jedwali 8.7** Sababu Zilizotolewa na Wanafunzi za Kutohudhuria Masomo | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Sababu za Kutohudhuria Masomo** | **Shule ya Msingi** | | **Shule ya Sekondari** | | **Wote %** |
| | **Wavulana %** | **Wasichana %** | **Wavulana %** | **Wasichana %** | |
| Ugonjwa | 61 | 60 | 64 | 58 | 61 |
| Harusi, mazishi | 36 | 33 | 31 | 41 | 36 |
| Sina fedha ya ada | 23 | 14 | 41 | 33 | 28 |
| Kuuguza mgonjwa | 13 | 11 | 16 | 12 | 13 |
| Kusaidia familia kazi shambani | 9 | 7 | 8 | 6 | 8 |
| Usafi binafsi | 9 | 9 | 4 | 3 | 7 |
| Kusaidia kazi nyumbani | 7 | 3 | 7 | 4 | 6 |
| Kusaidia biashara ya familia | 5 | 5 | 7 | 5 | 6 |
| Kutegea kazi shuleni | 7 | 6 | 7 | 4 | 6 |
| Kufanya kazi ili kujipatia pesa | 6 | 7 | 6 | 1 | 5 |

### 8.7 Walimu

Walimu ni watu muhimu sana katika suala la elimu, na utafiti wa Maoni ya Watu uliuliza maswali kuhusu vipengele mbalimbali vya mwingiliano wa walimu na wanafunzi wao. Karibu 60% ya vijana wanaosoma shule walisema kuwa kamwe walimu hawakukosa kuhudhuria vipindi vyao au walikosa kwa nadra. Utoro wa walimu uliripotiwa kuwa juu kidogo vijijini kuliko mijini, lakini hakuna tofauti kubwa ya utoro kati walimu wa shule ya msingi na wale wa sekondari au tofauti katika maelezo yaliyotolewa na wanafunzi wa kike na wa kiume.

| **Jedwali 8.8** Utoro wa Walimu | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Utoro wa Walimu** | **Shule ya Msingi** | | **Shule ya Sekondari** | | **Wote %** |
| | **Wanaume %** | **Wanawake %** | **Wanaume %** | **Wanawake %** | |
| Walimu si watoro kamwe | 27 | 32 | 33 | 23 | 29 |
| Walimu hukosa kuhudhuria kwa nadra | 31 | 26 | 31 | 31 | 30 |
| Walimu hukosa kuhudhuria wakati mwingine | 40 | 37 | 33 | 42 | 38 |
| Walimu ni watoro mara kwa mara | 1 | 5 | 3 | 4 | 4 |

Kwa ujumla, walimu walichukuliwa kuwa ni wapole na siyo wakali kwa wanafunzi wao. Zaidi ya 60% ya wanafunzi walisema kuwa walimu wao wote, wengi, au baadhi yao ni wapole, lakini 40% ya wanafunzi walichukulia kuwa 'baadhi' au 'wengi' wa walimu wao ni wakali, idadi kubwa kidogo wakiwa walimu wa shule ya msingi kuliko wa shule ya sekondari, na wanafunzi wengi zaidi wa kike ndio walioripoti hivyo kuliko wanafunzi wa kiume (Jedwali 8.9). Katika swali lililofuatia zaidi hali hiyo, wanafunzi waliulizwa kuhusu adhabu ya viboko. 20% tu ya wanafunzi ndiyo walioripoti kutokuwepo kwa adhabu ya viboko. Katika 16% ya shule zilizofanyiwa utafiti, walisema kuwa walimu 'wote au walio wengi' hutoa adhabu zinazoumiza mwili kama vile kuwachapa wanafunzi wao. Wanafunzi wa shule ya msingi walielekea kuripoti zaidi matumizi ya adhabu zinazoumiza mwili kuliko wanafunzi wa shule ya sekondari, na wasichana wa shule ya msingi wakitaja zaidi kupokea adhabu za aina hii kuliko wavulana wa shule ya msingi (Jedwali 8.10).

| **Jedwali 8.9** Mitazamo ya Wanafunzi kwa Walimu Wao | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Mitazamo kuhusu Walimu** | **Shule ya Msingi** | | **Shule ya Sekondari** | | **Wote %** |
| | **Wanaume %** | **Wanawake %** | **Wanaume %** | **Wanawake %** | |
| Wote / wengi wao ni wapole | 30 | 25 | 38 | 32 | 32 |
| Baadhi yao ni wapole | 28 | 27 | 30 | 30 | 29 |
| Baadhi yao ni wakali | 34 | 34 | 27 | 25 | 30 |
| Wengi wao / wote ni wakali | 8 | 14 | 5 | 13 | 10 |

| Jedwali 8.10 Walimu na Utoaji wa Adhabu ya Viboko | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Walimu na Adhabu ya Viboko** | **Shule ya Msingi** | | **Shule ya Sekondari** | | **Wote %** |
| | **Wanaume %** | **Wanawake %** | **Wanaume %** | **Wanawake %** | |
| Hakuna hata mmoja wao anayetuchapa / anayetupiga | 15 | 10 | 30 | 23 | 20 |
| Wachache miongoni mwao hutuchapa / hutupiga | 45 | 38 | 29 | 42 | 38 |
| Baadhi yao hutuchapa / hutupiga | 25 | 31 | 27 | 21 | 26 |
| Wote au wengi wao hutuchapa / hutupiga | 16 | 21 | 14 | 14 | 16 |

Wengi wa wanafunzi wa shule ya msingi na sekondari walisema kuwa baadhi au wengi wa walimu wao waliwahimiza kuuliza maswali wawapo darasani. Kwa ujumla 84% walijibu hivyo. Idadi kubwa kidogo ya wanafunzi wa sekondari walijibu hivyo pia. Wasichana walielekea zaidi kuliko wavulana kusema kuwa walimu hawakuwahimiza kuuliza maswali.

| Jedwali 8.11 Walimu Kuhimiza Wanafunzi Kuuliza Maswali | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Kuhimiza Wanafunzi Kuuliza Maswali** | **Shule ya Msingi** | | **Shule ya Sekondari** | | **Wote %** |
| | **Wanaume %** | **Wanawake %** | **Wanaume %** | **Wanawake %** | |
| Walio wengi | 47 | 50 | 55 | 51 | 51 |
| Baadhi yao | 37 | 26 | 35 | 33 | 33 |
| Wachache | 11 | 16 | 6 | 14 | 11 |
| Hakuna | 6 | 8 | 4 | 3 | 5 |

## 8.8 Utafiti wa 'Maoni ya Watoto'

Maoni ya watoto wadogo 512 wa shule ya msingi wenye umri wa miaka 7 hadi 14 yalitafutwa pia. Maoni yao kuhusu masuala ya elimu na nafasi yao katika jamii yamejumuishwa katika ripoti ya utafiti wa *'Maoni ya Watoto Tanzania'* itakayotolewa hivi karibuni. Maoni hayo yanajadiliwa kwa muhtasari katika sehemu inayofuata.

Mtindo unaotumiwa kujifunza, kama unavyoelezwa na watoto wadogo wa shule ya msingi, wenye umri wa miaka 7-14, ni ule unaotegemea kwa kiwango kikubwa mno kunakili maandiko kutoka ubaoni na vitabuni. Mara kwa mara watoto walitaja haja ya walimu wao kuwa na mwandiko mzuri ubaoni, hali inayoonyesha jinsi jambo hili lilivyo muhimu ili watoto waweze kusoma vizuri kilichoandikwa ubaoni. Vitabu vinathaminiwa na kupendwa sana na watoto hawa, lakini vilevile ni chanzo cha kuwavunja moyo, kwani ingawa kwa ujumla kuna ongezeko la usambazaji wa vitabu, bado vitabu ni vichache sana ikilinganishwa na mahitaji yaliyopo. Watoto wangependa kujisomea vitabu kwa muda wao wenyewe, lakini kwa ujumla vitabu hukusanywa mwishoni mwa kila kipindi.

Hali kadhalika, watoto walieleza bayana sifa wanazotaka awe nazo mwalimu wao. Mwalimu hana budi kuwa mtu anayependa kweli kufundisha, huwapenda watoto, anayo juhudi, na huhakikisha kuwa wanafunzi wanaelewa. Ilidhihirika katika utafiti huu kwamba baadhi ya watoto kwa hakika walikuwa na walimu walio hodari kiasi hicho. Hata hivyo, kila shule iliyofanyiwa utafiti ilionyesha kuwepo kwa matatizo mbalimbali kama vile kuwepo kwa walimu wasiokidhi matakwa muhimu ya mkataba, au kwa maneno mazuri zaidi, walimu wenye sifa duni kitaaluma. Walimu kutohudhuria vipindi ni tatizo kubwa. Watoto walitaja kuwepo kwa walimu waliokuwa wakitoa vitini bila kueleza kile kinachozungumziwa katika vitini hivyo, au waliwaambia wakaombe msaada kwa wanafunzi wa madarasa ya juu ili wawaeleweshe. Hofu ya adhabu ya viboko - inayosababishwa, kwa mfano, na walimu wanaoingia na fimbo darasani - ilielezwa na watoto kuwa ni kikwazo kikubwa katika kujifunza.

Kwa ujumla, mchakato wa kujifunza katika mazingira ya shule unaonekana kuwabana wanafunzi kufuata wanayoyasema walimu kama 'amri zilizowekwa' kwa ajili ya watoto ambao kwa kiwango kikubwa kazi yao ni kuzifuata tu. Watoto waliosailiwa katika utafiti huu hawakuwa wamezoea kufundishwa kwa mbinu shirikishi za ufundishaji.

Mawasiliano kati ya shule na wazazi yalikuwa hafifu.

Watoto walitarajiwa kutoa michango ya hali na mali katika shule zote zilizokuwa katika sampuli ya utafiti, na husimamishwa masomo kwa kushindwa kuilipa.

Watoto walikuwa na maoni mbalimbali iwapo kwa ujumla hali ya elimu ilikuwa bora zaidi mwaka juzi kuliko mwaka jana. Watoto wengi zaidi walihisi kwamba njia bora zaidi ya kuimarisha elimu ni kuongeza usambazaji wa nyenzo za ziada, ikiwa ni pamoja na miundombinu, walimu, na vifaa vya shule. Vilevile walitaka wawe na walimu bora zaidi, mtaala mpana zaidi, na huduma nyingine shuleni (kama vile huduma za afya). Watoto wa Dar es Salaam walioshiriki katika utafiti huu walionyesha ujasiri kwa kusema kuwa kuongeza juhudi yao binafsi katika masomo na kuwasikiliza walimu na wazazi ni kigezo muhimu pia katika kuboresha elimu yao.

# AFYA

Hali ya afya ya watu hutegemea mambo mbalimbali ya msingi, ikiwa ni pamoja na lishe, mtindo wa maisha alio nao mtu na usafi wa mazingira. Huduma za msingi za afya zinaweza kuwa za tiba au za kujikinga dhidi maradhi, lakini gharama nyingi za afya hutumiwa katika tiba, yaani kuwatibu wagonjwa. Utafiti huu ulichunguza hali ya jumla ya afya za watu na maoni waliyokuwa nayo kuhusu upatikanaji, ubora, gharama na namna wanavyozifikia huduma za msingi za afya zinazotolewa na serikali. Sura hii inataarifa kuhusu maoni ya watu wazima na watoto. Masuala muhimu ya kiafya ya wazee yameripotiwa katika sura ya 11.

## 9.1 Hali ya Afya na Matatizo Yanayohusiana Nayo

Watu wazima katika utafiti huu waliulizwa kuhusu hali ya afya zao kwa siku za karibuni: iwapo waliugua katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita, na kama waliugua, je, waliugua ugonjwa upi na mara ngapi. Theluthi mbili, 66%, ya watu wazima waliarifu kuwa walishikwa na ugonjwa wa malaria mara moja au zaidi katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita, 60% wakiugua kikohozi, homa au mafua, na 32% waliugua ugonjwa wa kuhara. Watu wachache tu waliosailiwa, 5%, ndio waliopata ajali katika mwaka huo.

Ugonjwa wa malaria ulitajwa zaidi katika maeneo ya mijini, na ugonjwa wa kuhara katika maeneo ya vijijini. Karibu robo tatu, 73%, ya watu waliosailiwa waliarifu kuwa walitumia vyandarua kuzuia mbu, vingi kati ya hivyo vikitajwa kuwa vimetiwa dawa ya kuzuia mbu, ingawa kwa ujumla 42% tu ya watu waliosailiwa ndiyo waliosema kuwa walikuwa na vyandarua vilivyotiwa dawa. Vyandarua vilitumiwa kwa wingi zaidi mijini kuliko vijijini.

**Jedwali 9.1** Matatizo ya Afya na Matumizi ya Vyandarua kwa Mwaka Uliopita

| Matatizo ya Afya Mwaka Uliopita | Dar es Salaam % | Miji Mingine % | Maeneo ya Vijijini % | Kote % |
|---|---|---|---|---|
| **Matukio ya Ugonjwa** | | | | |
| Malaria | 76 | 63 | 63 | 66 |
| Kikohozi, homa, mafua | 62 | 57 | 60 | 60 |
| Kuhara | 29 | 24 | 35 | 32 |
| Ajali | 5 | 4 | 4 | 5 |
| **Matumizi ya Vyandarua** | | | | |
| Vilivyotiwa dawa | 56 | 45 | 34 | 42 |
| Visivyo na dawa | 32 | 34 | 27 | 31 |
| Wasio na vyandarua | 12 | 21 | 39 | 27 |

## 9.2 Huduma za Afya

Walipoulizwa kuhusu matatizo makubwa zaidi yanayowakabili katika kupata huduma za afya, 32% ya watu wazima waliosailiwa walilalamikia suala la ubora / upatikanaji wa huduma hiyo, 16% walilalamikia umbali, 13% walitaja upatikanaji wa madawa na 10% bei yake. Zaidi ya robo ya watu waliosailiwa hawakuwa na jibu kwa swali hili. Kwa watu wazima waliotumia huduma za afya, karibu theluthi mbili walilalamikia gharama kubwa za tiba na ununuzi wa madawa kuwa tatizo kubwa. Vilevile, zaidi ya mbili ya tano (44%) ya watu wazima walilalamika kuhusu ukosefu wa madawa.  Watu wengi zaidi wa mijini (zaidi ya 50%) walilalamikia muda mwingi wa kusubiri kupewa huduma, wakati wakazi wengi zaidi wa vijijini (42%) walilalamika kuhusu ukosefu wa huduma za afya. Kati ya watu waliosailiwa wachache walilalamikia tabia ya ukali ya wahudumu wa afya (18%), ukosefu wa huduma za uzazi (13%) na huduma za chanjo (2%), na usafi katika utoaji wa huduma za afya (10%), angalia Jedwali 9.2.

**Jedwali 9.2** Matatizo katika Huduma za Afya

| Matatizo Makubwa Yahusuyo Afya | Dar es Salaam % | Miji Mingine % | Vijijini % | Kote % |
|---|---|---|---|---|
| Gharama za tiba na madawa | 62 | 69 | 61 | 62 |
| Upatikanaji wa madawa | 50 | 56 | 45 | 44 |
| Muda mrefu wa kusubiri huduma | 55 | 52 | 42 | 43 |
| Upatikanaji wa huduma za afya | 34 | 35 | 42 | 35 |
| Ukali wa wahudumu wa afya | 25 | 23 | 16 | 18 |
| Upatikanaji wa huduma za uzazi | 13 | 14 | 13 | 13 |
| Kiwango duni cha usafi katika huduma | 10 | 10 | 10 | 10 |
| Ukosefu wa chanjo | 3 | 3 | 2 | 2 |

### 9.3 Huduma za Afya Shuleni

Watoto wa shule ya msingi waliulizwa kuhusu huduma za afya katika shule zao, ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa huduma ya kwanza, au urahisi wa kupata ruhusa ya kwenda hospitali (na umbali uliokuwepo kwenda huko). Nusu ya shule zilizokuwa katika sampuli ya utafiti zilikuwa na namna fulani ya utoaji wa huduma ya kwanza. Katika shule nyingine, mtoto anapougua hupelekwa katika hospitali au zahanati iliyo karibu. Mkoa wa Dar es Salaam ndio uliokuwa na utaratibu unaoeleweka zaidi wa utoaji huduma ambapo watoto walitaja kuwa hupata chanjo, uchunguzi wa meno na dawa ya meno shuleni. Shule mojawapo ilihakikisha kuwa watoto wa darasa la kwanza walipata bure huduma ya tiba, na katika shule moja ya Lindi wanafunzi wakubwa waliweza kukumbuka kuwa siku zilizopita kama mtu aliende na daftari la wagonjwa, basi angepewa huduma za tiba bure, lakini wakaarifu kuwa sasa hivi wanatakiwa kulipia ada ya shilingi 1,000/-. Shule moja peke yake ndiyo iliyoonekana haikuwa na utaratibu wa kutoa huduma za afya kwa watoto wagonjwa.

Majibu ya watoto kuhusu hali ya utoaji wa huduma za afya shuleni yanaonyesha wanatambua kuwa lishe bora, kupata chakula wanapokuwa shuleni na vilevile upatikanaji wa maji safi ni miongoni mwa mambo muhimu kwa afya zao. Utafiti huu uliangalia masuala ya lishe miongoni mwa watoto 512 iliowashirikisha katika utafiti. Shule tatu tu kati ya kumi zilizokuwa katika sampuli ya utafiti ndizo zilizotajwa kuwa na utaratibu wa kutoa chakula kwa watoto - moja ikiwa ni shule wanayosoma watoto wa watu wenye kipato cha juu na nyingine mbili za wenye kipato cha kati - na hata katika shule hizi mbili, utaratibu huo ulionekana kutotumika kwa wakati huo. Katika shule nyingine mbili (moja ya Arusha na nyingine ya Dar es Salaam), ilibainishwa kuwa chakula huuzwa kwenye maduka madogo na vibanda vilivyo jirani na shule. Shule nyingine moja ambayo pia ina shule ya chekechea hutoa huduma ya uji kwa gharama ya shilingi 1,500/- kwa mwezi.

Walipoulizwa kuhusu mpangilio wao wa ulaji, zaidi ya theluthi moja, 35%, ya wanafunzi waliosailiwa wenye umri wa miaka 15 na kuendelea ndio waliosema kuwa siku zote hula kabla ya kwenda shule, idadi hiyo ikianzia robo, 26%, ya wanafunzi wa vijijini hadi nusu, 48%, kwa wale wa Dar es Salaam. Wanafunzi wapatao 15% walisema kuwa hula vyakula vidogovidogo wakati wa mapumziko shuleni, wakati wanafunzi walio wengi zaidi, 85%, walisema kuwa hula warudipo nyumbani kutoka shuleni.

### 9.4 Usalama Barabarani

Kutokana na hali iliyopo sasa ya ajali za barabarani kama inavyoripotiwa katika vyombo mbalimbali vya habari, watu wazima waliulizwa iwapo rafiki wa karibu, ndugu au jirani yao alifariki au kujeruhiwa vibaya katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita kwa ajali barabarani.

**Jedwali 9.3 Matukio ya Vifo na Majeraha Makubwa (kwa marafiki, ndugu, majirani) Kutokana na Ajali Barabarani**

| Matukio ya Ajali Barabarani | Dar es Salaam % | Miji Mingine % | Vijijini % | Kote % |
|---|---|---|---|---|
| Waliofariki | 17 | 13 | 11 | 13 |
| Waliojeruhiwa | 19 | 16 | 11 | 14 |
| Jumla | 36 | 29 | 22 | 27 |

Zaidi ya 40% ya ajali zilizosababisha vifo au majeraha ziliwatokea watu waliokuwa wakitumia magari ya abiria. Robo ya wahanga wa ajali hizi walikuwa wakitembea kwa miguu wakati ajali hizi zilipowafika. Ajali zilizowakumba waendesha baiskeli au pikipiki zilikuwa 19% ya ajali zilizoripotiwa, huku ajali chache zaidi zikiwakumba watu waliokuwa wakisafiri kwa magari yao binafsi. Washiriki wa utafiti huu mkoani Dar es Salaam waliripoti ajali nyingi zaidi kuliko wale wa miji mingine au wa vijijini. Ajali zilizoripotiwa ziliathiri zaidi magari ya abiria - *daladala* - jijini Dar es Salaam, na kusababisha karibu nusu ya idadi ya vifo au majeraha makubwa kwa watu katika mji huo. Vilevile, ajali nyingi sana ziliwakumba waenda kwa miguu jijini Dar es Salaam, idadi yake ikiwa ni 29%. Karibu 25% ya ajali zilizosababisha vifo au majeraha makubwa katika maeneo ya vijijini ziliwakumba waendesha baiskeli na pikipiki.

**Jedwali 9.4 Chanzo cha Vifo au Majeraha**

| Vifo na Majeruhi Safarini | Dar es Salaam % | Miji Mingine % | Maeneo ya Vijijini % | Kote % |
|---|---|---|---|---|
| Magari ya abiria | 46 | 40 | 41 | 42 |
| Waenda kwa miguu | 29 | 25 | 22 | 25 |
| Baiskeli / pikipiki | 9 | 21 | 25 | 19 |
| Magari ya binafsi | 16 | 15 | 12 | 14 |

# HUDUMA YA MAJI

Huduma ya maji safi na salama majumbani na mfumo mzuri wa kutiririsha maji taka ni mambo ya lazima kwa afya bora na kuzuia magonjwa yanayosambazwa kwa njia ya maji, magonjwa ambayo huua na kuwadhoofisha watoto na watu wazima. Taarifa zilikusanywa kutoka kwa watu wazima waliosailiwa kuhusu mwenendo wa utoaji wa huduma ya maji safi na maji taka.

## 10.1 Vyanzo vya Maji Majumbani na Utaratibu wa Malipo

Jedwali 10.1 na Jedwali 10.2 zinaonyesha jinsi watu waliosailiwa wanavyopata na kulipia huduma ya maji. Kati ya 80% na 90 % ya watu wazima waliosailiwa hupata maji yao ya kunywa kutoka kwenye vyanzo vilivyopo katika jamii au kwa majirani zao. Hata mijini, 16% - 20% tu ya watu ndio wenye maji ya bomba kwenye nyumba zao au karibu na nyumba zao. Wakati 73% ya watu wazima vijijini hawalipii maji wanayoyatumia, huku 8% tu ya wakazi wa Dar es Salaam ndio pia wakijipatia maji bure, 77% ya wakazi hao wa Dar es Salaam huwalipa wauzaji binafsi wa maji (watu wenye pampu za kuvuta maji, vibanda, majirani au wachuuzi wa maji). Wanaopata maji kutoka mamlaka ya maji (DAWASCO) ni 13% tu.

**Jedwali 10.1** Vyanzo Vikuu vya Maji ya Kunywa

| Vyanzo vya Maji ya Kunywa | Dar es Salaam % | Miji Mingine % | Vijijini % | Kote % |
|---|---|---|---|---|
| Vyanzo vinavyomilikiwa na jamii / watu binafsi | 41 | 55 | 89 | 70 |
| Maji ya bomba kwenye mji wa jirani | 42 | 23 | 5 | 18 |
| Maji ya bomba ndani ya nyumba / karibu na nyumba | 16 | 20 | 3 | 10 |
| Vyanzo vinginevyo | 1 | 2 | 3 | 2 |

**Jedwali 10.2** Utaratibu wa Kulipia Maji ya Kunywa

| Utaratibu wa Kulipia Maji ya Kunywa | Dar es Salaam % | Miji Mingine % | Vijijini % | Kote % |
|---|---|---|---|---|
| Silipii (maji ni ya bure) | 8 | 38 | 73 | 49 |
| Ninalipia pesa (kwa mwenye pampu, kibanda, jirani) | 64 | 36 | 17 | 33 |
| Ninalipa bili mamlaka ya maji | 13 | 19 | 3 | 9 |
| Ninalipia pesa (kwa wachuuzi wa maji) | 13 | 6 | 4 | 6 |
| Vyanzo vinginevyo | 1 | 1 | 3 | 3 |

## 10.2 Mwelekeo na Matatizo katika Utoaji wa Huduma ya Maji

Jedwali 10.3 linaonyesha mwelekeo uliokuwepo katika utoaji wa huduma ya maji katika kipindi cha miezi kumi na miwili iliyopita. Jibu lililotolewa na watu wengi waliosailiwa ni kwamba hawakuona kuwepo kwa mabadiliko - karibu 70% walisema hapakuwa na tofauti kwenye umbali wa kuyapata maji, usafi wa maji, gharama yake wala muda wa kujipanga kwenye foleni ya kulipia, na 49% walisema hapakuwa na tofauti kwenye kiasi cha maji yanayotolewa. Miongoni mwa wale waliobaini kuwepo kwa mabadiliko katika utoaji wa huduma ya maji, kwa ujumla, wengi wao waliona kupungua badala ya kuongezeka kwa kiwango cha ubora wa huduma ya maji, usafi, kuongezeka kwa gharama na muda wa kupanga foleni, ingawa kuna mabadiliko kiasi yaliyoonekana katika kupunguza umbali wa kupata huduma za maji katika maeneo ya mijini (ikiwemo Dar es Salaam).

| Jedwali 10.3 Mwelekeo wa Utoaji wa Huduma ya Maji | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwelekeo wa Utoaji wa Huduma ya Maji** | **Dar es Salaam %** | | **Miji Mingine %** | | **Maeneo ya Vijijini %** | | **Kote %** | |
| | **Bora** | **Duni** | **Bora** | **Duni** | **Bora** | **Duni** | **Bora** | **Duni** |
| Upungufu | 20 | 33 | 27 | 26 | 20 | 29 | 21 | 29 |
| Umbali | 17 | 13 | 17 | 11 | 9 | 14 | 13 | 13 |
| Usafi | 15 | 17 | 17 | 14 | 7 | 22 | 11 | 19 |
| Gharama | 8 | 32 | 14 | 16 | 12 | 8 | 11 | 16 |
| Muda wa kujipanga foleni | 12 | 26 | 17 | 14 | 12 | 13 | 12 | 17 |

Upungufu wa maji wakati wa kiangazi ulitajwa kuwa jambo la kawaida mijini na vijijini. Hususan wakazi wa vijijini waliosailiwa walilalamika kuhusu kupata maji machafu na yasiyowekewa dawa. Umbali wa kuvifikia vyanzo vya maji ni tatizo kubwa zaidi vijijini, wakati wakazi wa mijini waliosailiwa walilalamika zaidi kuhusu kukaa sana kwenye foleni na gharama kubwa za maji (tatizo kubwa zaidi likiwa jijini Dar es Salaam).

| Jedwali 10.4 Matatizo ya Utoaji wa Huduma ya Maji | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Matatizo Makubwa ya Utoaji wa Huduma ya Maji** | **Dar es Salaam %** | **Miji Mingine %** | **Vijijini %** | **Kote %** |
| Upungufu wakati wa kiangazi | 54 | 59 | 68 | 63 |
| Maji machafu / yasiyo na dawa | 31 | 35 | 54 | 45 |
| Umbali wa kwenda kwenye vyanzo | 16 | 21 | 35 | 28 |
| Muda wa kupanga foleni | 41 | 20 | 20 | 26 |
| Gharama | 54 | 25 | 10 | 25 |

### 10.3 Huduma ya Maji Shuleni

Suala la upatikanaji na usafi wa maji si tatizo lililoko kwenye makazi ya watu pekee. Watoto wa shule ya msingi nao pia wanatambua umuhimu wa maji safi kwa ajili ya kunywa na kwa shughuli za usafi. Umuhimu wa maji huongezeka zaidi na zaidi ikiwa watoto hutembea umbali mrefu kwenda shule, na kwa sababu hiyo hushikwa na kiu sana. Pamoja na ukweli huo, shule mbili tu za msingi zilizokuwa katika sampuli ya utafiti huu (moja mkoani Mwanza na nyingine mkoani Tanga) ndizo zilizokuwa na maji salama ya kunywa kwa ajili ya watoto. Kaimu mwalimu mkuu katika shule moja mkoani Mtwara alisema kuwa ugonjwa wa kipindupindu na kuhara ni matatizo yanayojitokeza mara kwa mara shuleni hapo kutokana na tatizo la maji. Mkoani Dar es Salaam, watoto walichukua maji yao ya kunywa kutoka makwao au walijinunulia kwenye vibanda vilivyo karibu na shule. Mkoani Mtwara, watoto walipata maji ya kunywa kama walirudi makwao wakati wa mapumziko au wakati wa chakula cha mchana. Vinginevyo, iliwabidi kusubiri hadi warudipo makwao baada ya muda wa masomo shuleni kuisha ndipo wapate maji safi ya kunywa.

Kwenye shule ya mkoani Tanga, maji ya kunywa yaliyochemshwa yalipatikana kwenye ofisi ya walimu na kwenye maktaba ingawa baadhi ya watoto walijinywea maji moja kwa moja kutoka bombani. Utoaji wa maji ya kunywa yaliyochemshwa unaonekana kuwa mfano wa mwenendo mwema ambao unaweza kuigwa na wengine wengi hususan kama tayari watoto wamezoea kupeleka kuni shuleni (kama ilivyo kwenye shule moja ya Lindi), ambazo zinaweza kutumiwa kuchemsha maji.

Upatikanaji wa maji safi shuleni lilikuwa tatizo kubwa kwa vijana wa vijijini waliokuwa bado wanasoma shule, ambapo 64% kati yao waliripoti kuwa hawakuwa na maji shuleni. Mkoani Dar es Salaam, 58% walisema walikuwa na maji tele shuleni, na 7% tu walisema hapakuwa na maji.

**Jedwali 10.5 Upatikanaji wa Maji Shuleni**

| Upatikanaji wa Maji Shuleni | Dar es Salaam % | Miji Mingine % | Vijijini % | Kote % |
|---|---|---|---|---|
| Ndiyo, yapo tele | 58 | 31 | 12 | 26 |
| Ndiyo, yapo kiasi | 24 | 17 | 15 | 18 |
| Kuna maji kidogo tu | 10 | 26 | 8 | 13 |
| Hakuna maji shuleni | 7 | 27 | 64 | 44 |
| Sijui / Hakuna jibu lililotolewa | 1 | 0 | 1 | 0 |

# WAZEE

Ukosefu wa usalama kwa baadhi ya makundi ya watu huonyesha hali halisi ya maisha, huku watoto wadogo na wazee wakiwa katika mazingira hatarishi zaidi. Serikali, jamii, makanisa, asasi zisizo za kiserikali na vyama vya hisani vinaweza kuwasaidia watu wazima kuwatunza watoto na wazee, na makundi mengine ya watu wanaoishi katika mazingira hatarishi, lakini mwenye jukumu la kwanza ni ndugu wa karibu wa watu hawa. Vyanzo vya riziki kwa wazee, misaada wanayoitoa kwa watu wengine, na ile wanayoipokea kutoka kwa watu wengine, na maoni yao kuhusu maadili ya jamii na raha na taabu ya mtu kuzeeka ni mambo yanayochunguzwa katika sura hii. Aidha, sura hii inachunguza pia masuala yahusuyo mahitaji yao ya maji, hali yao kiafya na mambo wanayoyafanya ili kujenga afya zao.

Zaidi kidogo ya 60% ya wazee 855 waliosailiwa katika utafiti huu walikuwa wanaume na 80% walikuwa wakuu wa kaya zao. Zaidi ya nusu ya waliokuwa katika sampuli - (57%) waliishi na wenzi wao, 33% walikuwa wamefiwa na wenzi wao, na 10% walikuwa wametengana.

### 11.1 Vyanzo vya Riziki kwa Wazee

Wakati wengi wa wanawake wazee hutegemea ndugu zao wa karibu ili waweze kujikimu kimaisha, 34% ya wanaume na 20% ya wanawake walidai kuwa bado wanafanya kazi ya kudumu. Wazee wachache sana waliosailiwa ndio waliokuwa wanapata malipo ya pensheni. Misaada kutoka asasi za kiraia, asasi za kidini, asasi za kijamii na zisizo za serikali vilevile ilikuwa michache sana. Kisanduku Namba 7 kitakachofuatia baadaye katika sura hii kinaonyesha baadhi ya hisia za wazee na uwezo wao mdogo katika kujitafutia riziki.

**Jedwali 11.1** Vyanzo Vikuu vya Wazee Kujikimu

| Vyanzo Vikuu vya Wazee Kujikimu | Wanaume % | Wanawake % | Wote % |
|---|---|---|---|
| Watoto / ndugu wanaonizunguka | 34 | 60 | 45 |
| Ninafanya kazi ya kudumu | 34 | 20 | 28 |
| Ninatumiwa fedha | 20 | 22 | 21 |
| Ninafanya kazi ya muda | 8 | 3 | 7 |
| Ninapata malipo ya pensheni | 7 | 1 | 5 |
| Ninasaidiwa na asasi za kidini, kijamii /zisizo za kiserikali, majirani | 1 | 2 | 2 |

**Angalizo:** Majibu ya aina mbalimbali yaliruhusiwa.

### 11.2 Vyanzo vya Misaada kwa Wazee

Wazee vilevile walitoa maoni yao kuhusu watu wanaoelekea kuwasaidia wanapofikwa na matatizo makubwa. Kwa wazee wengi - 88% ndugu wa karibu ndiyo wana uwezekano au wana uwezekano mkubwa kutoa msaada. Asilimia 38 ya wazee waliosailiwa walisema kuwa marafiki na majirani zao wanaweza kuwasaidia. Karibu 11% hawakutarajia namna yoyote ya kupata msaada (tazama Jedwali 11.2).

| Jedwali 11.2 Vyanzo vya Misaada kwa Wazee | | | |
|---|---|---|---|
| **Vyanzo vya Misaada Wakati wa Matatizo Makubwa** | **Wanaume %** | **Wanawake %** | **Wote %** |
| Wanafamilia | 88 | 88 | 88 |
| Marafiki na majirani | 38 | 38 | 38 |
| Ukoo, wazee wenzangu | 35 | 29 | 33 |
| Viongozi / asasi za kidini | 22 | 18 | 21 |
| Serikali ya mtaa | 13 | 10 | 12 |
| Kikundi cha wazee | 12 | 10 | 11 |
| Sina mtu wa kunisaidia | 10 | 12 | 11 |
| Asasi za kijamii / zisizo za kiserikali kwenye eneo husika | 5 | 6 | 5 |

### 11.3 Huduma ya Maji kwa Wazee

Wazee waliosailiwa waliulizwa kuhusu namna wanavyopata maji kwa matumizi ya nyumbani na matatizo wanayokumbana nayo. Wazee wachache, 28%, hujitekea maji wao wenyewe; walio wengi (68%) hutekewa na ndugu au mfanyakazi wa nyumbani. Wanawake wengi wazee hujitekea maji wenyewe ikilinganishwa na wanaume wazee.

Walipoulizwa kama wana matatizo yoyote katika kupata huduma ya maji, wazee waliosailiwa walitaja kukumbana na baadhi ya matatizo yaliyo sawa na yale yaliyotajwa na watu wazima kama ilivyoonyeshwa katika Sura 10.

### 11.4 Huduma za Afya kwa Wazee

Theluthi mbili, 65% ya wazee walisema kuwa walikuwa na matatizo ya afya yanayohitaji uangalizi wa mara kwa mara, 62% wakiwa wanaume na 68% wanawake. Tatizo lililotajwa mara nyingi zaidi ni uwezo wao wa kutembea, tatizo ambalo liliripotiwa na 42% ya wazee wanaume na wanawake.

Theluthi mbili ya wazee wenye umri wa zaidi ya miaka sitini walitafuta huduma za tiba katika kipindi cha miezi mitatu kabla ya kufanywa kwa utafiti huu, huku wanawake wengi zaidi wakitafuta tiba kuliko wanaume. Kwa wale waliotafuta huduma za tiba, 35% walijilipia wenyewe gharama za tiba, 27% walilipiwa na ndugu zao, 15% walipata tiba bure, na 14% hawakupata huduma yoyote ya tiba. Karibu nusu (44%) walikwenda kutibiwa kwenye hospitali za serikali, 27% walinunua dawa kwenye maduka ya kuuza dawa, na robo, 24%, walienda kutibiwa kwenye hospitali za binafsi.

| Jedwali 11.3 Ulipiaji wa Huduma za Afya | | | |
|---|---|---|---|
| **Kulipia Matibabu** | **Wanaume %** | **Wanawake %** | **Wote %** |
| Nilijilipia mwenyewe | 43 | 27 | 35 |
| Familia yangu ilinilipia | 18 | 41 | 27 |
| Nilipata matibabu bure | 15 | 14 | 15 |
| Sikupata matibabu | 13 | 16 | 14 |
| Mengineyo | 8 | 9 | 8 |
| Bima ya afya | 2 | 3 | 2 |

Jambo la kusikitisha, karibu nusu ya wazee wenye umri wa zaidi ya miaka sitini (48%) hawakujua kuwa wana haki ya kupata bure huduma za tiba kwenye hospitali za serikali (42% kwa wanaume na 58% kwa wanawake). Zaidi ya hayo, takriban moja ya tano (18%) ya wazee waliosailiwa walisema kuwa walinyimwa huduma za tiba kwenye hospitali za serikali kwa kuwa hawakuwa na uwezo wa kulipia gharama za tiba, na 13% walisema kuwa walinyimwa huduma za bure za tiba kwa kukosa uthibitisho wa umri wao.

Jedwali 11.4 linaonyesha kwa muhtasari matatizo yanayowakabili wazee wanapotafuta huduma za afya. Wakati wazee wengi waliotafuta huduma za tiba walisema kuwa hawakupata matatizo katika kupata huduma hizo, 38% walisema kuwa tatizo lao kubwa ni kwamba waliombwa kulipia huduma hizo.

**Jedwali 11.4** **Matatizo Yanayowakabili Wazee katika Kupata Huduma za Tiba**

| Matatizo Makuu katika Kupata Huduma za Tiba | Wanaume % | Wanawake % | Wote % |
|---|---|---|---|
| Kuombwa kulipia gharama | 40 | 36 | 38 |
| Upatikanaji wa madawa na vifaa vya tiba | 30 | 28 | 29 |
| Umbali / muda wa kwenda huko | 25 | 25 | 25 |
| Kusubiri kuonana na wahudumu / kupata matibabu | 14 | 15 | 14 |
| Nidhamu ya wahudumu wa afya | 11 | 10 | 11 |

Katika maeneo mengi ambayo utafiti ulifanywa, wazee wanajua kuwa wana haki ya kupata bure huduma za tiba, lakini wakati mwingine sera hiyo hupuuzwa na watekelezaji. Hali hii ilionekana kuwepo kote: mijini na vijijini. Kisanduku Namba 7 kinaonyesha baadhi ya maoni kuhusu ugumu wanaokumbana nao wazee katika kupata huduma za bure za afya.

**SANDUKU 7**: **MATATIZO YA WAZEE KATIKA KUPATA MATIBABU YA BURE**

*"Kwenye redio wanasema akina mama, wazee, na watoto wadogo wanapewa huduma bure, lakini kwa eneo hili ni kitendawili na haijawahi kutokea."*
• Kikundi Maalumu cha Wanawake, Korogwe

*"Msamaha wa matibabu wa wazee huku ni kama haupo, ukienda na barua utaambiwa hakuna dawa. Maduka ya dawa tunayoagiziwa ni ya madaktari wenyewe."*
• Kikundi Maalumu cha Wazee, Tanga

*"Kuhusu matibabu ya bure kwa wazee bila kunyanyaswa… tunaambiwa tu, lakini inatakiwa pesa; mfano, unaweza ukaambiwa nenda huko walikotangaza matibabu bure… Umesikia wapi matibabu bure?'*
• Kikundi Maalumu cha Wazee, Dar es Salaam

*"Alienda kupata huduma akaulizia sera hiyo akakataliwa huduma mpaka atoe pesa. Jibu la wauguzi wanasema hawajui... Vikongwe wanahudumiwa na pesa."*
• Kikundi Maalumu, Lindi

### 11.5 Huduma Zinazotolewa na Wazee

Kulea wajukuu ni jambo la kawaida kabisa kwa wazee wengi wa umri mkubwa. Karibu 40% ya wazee waliosailiwa waliarifu kuwa walikuwa wakilea wajukuu wao, mara nyingi kwa sababu ya kufariki au kuugua kwa wazazi wa watoto hao. Katika kuwalea wajukuu wao, karibu robo tatu walisema kuwa walikuwa wanasaidiwa na ndugu zao wa karibu.

### 11.6 Wasiwasi wa Wazee kuhusu Mustakabali Wao

Wazee waliulizwa pia kuhusu hofu walizonazo kwa siku zijazo. Usalama wao katika umri mkubwa ni suala linaloleta hofu kubwa miongoni mwa wazee, huku 75% ya wazee waliosailiwa wakiwa na hofu ya kupoteza nguvu za kufanya kazi kwa kadri wanavyozidi kuzeeka, na 66% wakihofia kukumbwa na njaa na umaskini, na kupoteza uhuru wao kutokana na maradhi. Hofu hizi zinafanana miongoni mwa wazee wa kike na wa kiume. Jedwali 11.5 linaonyesha vilevile masuala mengine nyeti yahusuyo haki za binadamu kama vile hofu ya kutuhumiwa kujihusisha na mambo ya kichawi ambayo ilitajwa na 25% ya wanaume na 32% ya wanawake walioshiriki katika utafiti huu. Utafiti wa Tathmini ya Umaskini kwa Mbinu ya Ushiriki Tanzania pia ulibaini kuwa tuhuma za uchawi ni moja ya matatizo wanayokabiliana nayo wazee (Tz-PPA ESRF, 2004).

| **Jedwali 11.5** Wasiwasi wa Wazee kuhusu Mustakabali Wao | | | |
|---|---|---|---|
| **Wasiwasi wa Wazee kuhusu Mustakabali wao** | **Wanaume %** | **Wanawake %** | **Wote %** |
| Kutoweza kufanya kazi | 76 | 74 | 75 |
| Kupoteza uhuru kutokana na maradhi | 67 | 64 | 67 |
| Njaa, umaskini | 69 | 66 | 66 |
| Kupoteza hadhi, majukumu katika jamii | 53 | 47 | 50 |
| Kutoheshimiwa katika jamii | 48 | 43 | 46 |
| Kuwa mpweke, kutengwa au kupuuzwa | 47 | 40 | 45 |
| Kushambuliwa, kuporwa | 43 | 36 | 40 |
| Kulea yatima | 38 | 40 | 39 |
| Migogoro ya kifamilia | 33 | 31 | 33 |
| Kutuhumiwa kwa uchawi | 25 | 32 | 28 |
| Kunyang'anywa mali pindi mwenzi anapofariki | 27 | 21 | 25 |
| Kudhuriwa na wachawi | 27 | 24 | 25 |

Kutoheshimiwa na kupoteza hadhi katika jamii ni mambo yanayowapa mashaka karibu nusu ya wazee waliosailiwa. Hata hivyo, hii haimaanishi kuwa vijana hawawaheshimu tena wazee. Kimsingi, wazee wengi zaidi, 60%, waliosailiwa wanaamini kuwa vijana huwaheshimu ikilinganishwa na wale wanaoamini kuwa hawawaheshimu. Katika jamii nyingine, mathalani katika Kata ya Mwamanoni (Shinyanga), kuna ushirikiano kati ya vijana na wazee ambao kwa jadi unaitwa *'Ukombakomba'.*

Hatimaye, maswali mawili yaliyowataka wazee kutoa maoni yao yaliulizwa ili kupata mtazamo wao kuhusu raha na taabu wanazozipata kutokana na uzee. Zaidi ya theluthi moja, 36%, ya wazee hao hawakuona raha ya kuzeeka, huku 28% waliona kuna raha ya asili kwa mtu kuzeeka. Kuheshimiwa na kuwa na hekima hayakuwa mambo muhimu sana yaliyowaletea wazee furaha ikilinganishwa na kitendo cha kuishi na wajukuu wao. Ingawa 20% ya wazee hawakuwa na jambo la kulalamikia linatokana na kuzeeka kwao, 33% walilalamikia kupoteza nguvu zao na kwa sababu hiyo kupoteza pia uwezo wao wa kufanya kazi. Maradhi ya mara kwa mara ni suala lililowapa hofu wazee wengine wapatao 22%. Wazee wengi wa kiume walikuwa na hofu ya kupoteza nguvu na uwezo wao wa kufanya kazi huku wazee wengi wa kike wakihofia maradhi.

| **Jedwali 11.6** Karaha ya Kuzeeka | | | |
|---|---|---|---|
| **Madhara Makubwa ya Kuzeeka** | **Wanaume %** | **Wanawake %** | **Jumla %** |
| Kupoteza nguvu, uwezo wa kufanya kazi | 37 | 26 | 33 |
| Maradhi ya mara kwa mara | 19 | 25 | 22 |
| Hakuna | 18 | 20 | 20 |
| Hakuna jibu lililotolewa / mengineyo | 12 | 15 | 12 |
| Kutukanwa, kutoheshimiwa | 5 | 7 | 6 |
| Kupoteza kumbukumbu | 1 | 1 | 1 |
| Kuwa tegemezi | 6 | 4 | 5 |
| Kutuhumiwa kwa uchawi | 1 | 2 | 1 |

# KULINGANISHA NA MATOKEO MENGINE YA UTAFITI MWAKA 2003 NA 2007 KUHUSU UTOAJI HUDUMA

Kulinganisha matokeo ya utafiti huu na yale ya Utafiti wa Sera na Utoshelevu wa Huduma (2003) na ya *Afrobarometer* [5] kuhusu kiwango cha ubora wa maisha na ustawi wa jamii unaonyesha kufanana kwa baadhi ya mambo (Jedwali 12.1). Kama ilivyo katika utafiti wa 'Maoni ya Watu', tafiti hizi za siku za nyuma zinaonyesha jinsi wananchi wengi wanavyounga mkono juhudi za serikali za kuboresha elimu. Utafiti huu wa sasa unathibitisha jinsi wananchi wanavyounga mkono uwekezaji unaofanywa na serikali katika miundombinu ya elimu, lakini vilevile unaibua suala la upungufu wa vitabu vya kiada unaoendelea kuwepo kwenye shule za msingi na sekondari.

Kwa miaka kadhaa iliyopita, serikali imekuwa ikitenga bajeti kubwa zaidi kila mwaka kwa ajili ya huduma za msingi, lakini kuna ushahidi wa kutatanisha iwapo ongezeko la bajeti linaongeza na kuboresha huduma zinazotolewa. Walipoulizwa iwapo utoaji wa huduma za msingi ulikuwa ukiimarika au ukizidi kuwa duni, wananchi wengi zaidi waliosailiwa walisema kuwa ulikuwa ukiimrika, 44%, kuliko wale waliosema ulikuwa ukizidi kuwa duni, 9%. Hata hivyo, gharama kubwa za tiba ziliripotiwa kuwa tatizo kubwa na zaidi ya nusu ya wananchi waliosailiwa katika Utafiti wa Sera na Utoshelevu wa Huduma (2003), na kutajwa pia na 62% ya wananchi waliosailiwa katika utafiti wa Maoni ya Watu (2007). Hali kadhalika, kuna malalamiko mengi kutoka kwa wananchi waliosailiwa katika utafiti wa Maoni ya Watu (2007) kuhusu kupanda kwa gharama za madawa, 44%, ikilinganishwa na yale yaliyotolewa na wananchi waliosailiwa katika Utafiti wa Sera na Utoshelevu wa Huduma (2003), 35%, miaka minne iliyopita. Wananchi wengi wazee huwawia vigumu kupata huduma za afya bure. Huduma ya maji majumbani bado inaendelea kuwa tatizo sugu mijini na vijijini, huku kwa ujumla wananchi wengi wakiona kushuka kwa kiwango cha upatikanaji na usafi wa maji. Kwa wakazi wa mijini waliosailiwa, kupanda kwa gharama ya maji ni miongoni mwa matatizo waliyoyataja.

**Jedwali 12.1 Matatizo Makuu katika Huduma za Jamii Mwaka 2003 na 2007**

| Dar es Salaam | | Maeneo ya Vijijini | | Kote | |
|---|---|---|---|---|---|
| **2003** | **2007** | **2003** | **2007** | **2003** | **2007** |
| Madawa | Maji majumbani | Maji majumbani | Maji majumbani | Madawa | Maji majumbani |
| Maji majumbani | Tiba | Madawa | Tiba | Maji majumbani | Tiba |
| Elimu | Elimu | Elimu | Madawa | - | Madawa |
| - | Madawa | - | - | - | - |

**Angalizo:** 'Tiba' humaanisha kupanda kwa gharama za tiba
'Madawa' humaanisha ugumu wa kupatikana na pia kupanda kwa gharama za ununuzi wa madawa
Utafiti wa Sera na Utoshelevu wa Huduma (2003) ulisaili wakuu wa kaya; utafiti wa Maoni ya Watu (2007) uliwasaili watu wazima na vijana.

**5** Tafiti mbali mbali, rejea tovuti: www.afrobarometer.org

# SEHEMU YA TATU:

## MKUKUTA KUNDI LA III

UTAWALA BORA NA UWAJIBIKAJI

# UTAWALA BORA NA UWAJIBIKAJI

Kwa maana pana zaidi, utawala huhusiana na taratibu za uendeshaji wa masuala ya umma katika kusimamia rasilimali, kutoa huduma muhimu, na kulinda haki na ustawi wa Watanzania wote.

Matokeo mengi ya utafiti wa Maoni ya Watu yanatoa takwimu zenye manufaa kuhusu hatua zinazopigwa katika kufikia malengo ya MKUKUTA ya kuleta utawala bora na kuongeza uwajibikaji, ikiwa ni pamoja na ushiriki wa wananchi katika masuala ya umma, maoni kuhusu juhudi za kuongeza uwajibikaji wa viongozi wa serikali, kupata taarifa kutoka kwa watendaji wa serikali na katika vyombo vya habari, ufahamu na maoni ya wananchi kuhusu siasa na sera, maoni kuhusu suala la rushwa, na imani walizo nazo wananchi kuhusu uaminifu, ushirikiano na usalama katika jamii ya Watanzania.

### 13.1 Ushiriki wa Wananchi katika Masuala ya Umma

Ushiriki wa wananchi katika masuala ya umma ulipimwa kwa kutumia vigezo viwili: ushiriki katika masuala ya kidini na kijamii, na uanachama katika asasi mbalimbali. Karibu watu wote wazima waliosailiwa walionyesha kuvutiwa na masuala ya dini, 93%, na 66% walionyesha kuvutiwa na masuala ya siasa na vilevile kujisomea na michezo, 60%.

Washiriki waliulizwa iwapo ni wanachama au walipata kuwa wanachama wa asasi mbalimbali rasmi na zisizo rasmi (Jedwali 13.1). Nusu ya wananchi waliosailiwa walisema kuwa walikuwa au walipata kuwa wanachama wa vyama vya siasa. Kuwepo kwa idadi kubwa ya wanachama wa vyama vya siasa kunaonyesha jinsi watu wanavyovutiwa mno na mambo ya siasa kama ilivyoelezwa hapo juu. Karibu moja ya tano ya watu waliosailiwa, 19%, walisema kuwa walikuwa wanachama wa vyama vya kuzikana au walikuwa walinzi wa jadi, *sungusungu.* Takriban moja ya kumi, 13%, walidai kuwa au kupata kuwa wanakwaya au washiriki wa vikundi vya dansi au vya kitamaduni, au wanachama wa vikundi visivyo rasmi vya michezo ya upatu.

Chini ya 10% walipata kuwa wajumbe wa kamati ya shule au ya usimamizi wa maji, asasi ya kijamii, chama cha ushirika, chama cha wakulima au kikundi cha kujiendeleza kiuchumi, au walipata kufanya kazi kama wenyeviti wa vijiji, madiwani au wajumbe wa baraza la kata au wilaya. Ukiacha uanachama wa vikundi visivyo rasmi vya michezo ya upatu au vyama vya kukopeshana, washiriki wa vijijini walielekea zaidi kuwa wanachama wa vyama mbalimbali kuliko wenzao wa mijini.

**Jedwali 13.1** Uanachama katika Vyama vya Eneo Husika

| Uanachama katika Vyama (zamani na / au sasa) | Dar es Salaam % | Miji Mingine % | Maeneo ya Vijijini % | Kote % |
|---|---|---|---|---|
| Chama cha siasa | 44 | 57 | 50 | 49 |
| Chama cha kuzikana | 17 | 22 | 19 | 19 |
| Mlinzi wa jadi *(sungusungu)* | 12 | 20 | 21 | 18 |
| Kikundi kisicho rasmi cha upatu | 15 | 15 | 11 | 13 |
| Kikundi cha kwaya, dansi au kitamaduni | 11 | 15 | 14 | 13 |
| Kamati ya shule ya msingi | 5 | 9 | 10 | 9 |
| Asasi ya kijamii | 7 | 10 | 7 | 8 |
| Chama cha ushirika / wakulima / kikundi cha kujiendeleza kiuchumi | 2 | 4 | 7 | 5 |
| Kamati ya Usimamizi wa Maji | 2 | 5 | 6 | 5 |
| Mwenyekiti wa kijiji, diwani / mjumbe wa baraza la kata / wilaya | 2 | 3 | 5 | 4 |

Katika muktadha wa ushiriki, washiriki waliulizwa iwapo waliwahi kushiriki katika shughuli mbalimbali za kiraia kama zilivyoorodheshwa katika Jedwali 13.2. Kwa ujumla, kiwango cha ushiriki wa wananchi katika masuala ya umma kiko chini. Zaidi kidogo tu ya thuluthi moja, 22% ya washiriki wa vijijini ndio waliosema kuwa wamepata kushiriki katika zoezi la kubuni mipango ya maendeleo katika maeneo yao, na takriban 16% walipata kufanya kazi kwenye miradi ya umma, hususan ujenzi na ukarabati wa barabara. Washiriki wachache zaidi wa mijini ndio walioripoti kuwa wamepata kushiriki katika shughuli za kiraia za aina hiyo.

**Jedwali 13.2** Aina za Ushiriki katika Masuala ya Umma

| Aina ya Ushiriki katika Masuala ya Umma | Dar es Salaam % | Miji Mingine % | Maeneo ya Vijijini % | Kote % |
|---|---|---|---|---|
| Kushiriki katika kubuni mpango wa maendeleo wa kijiji / kata | 7 | 18 | 22 | 18 |
| Kufanya kazi katika mradi wa umma | 6 | 13 | 16 | 13 |
| Kuhudhuria mafunzo ya elimu ya uraia | 10 | 11 | 12 | 11 |
| Kuhudhuria mkutano mkuu wa baraza la eneo ninaloishi | 9 | 10 | 9 | 9 |

Washiriki waliulizwa pia iwapo katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita waliomba kupatiwa taarifa zozote zinazohusiana na huduma zinazotolewa na serikali katika ngazi ya wilaya, kata, kijiji au mtaa na iwapo kwa kufanya hivyo walipatiwa taarifa zozote. Washiriki walio wengi hawakuomba kupatiwa taarifa kutoka kwa viongozi wa umma katika ngazi hizi. Jedwali 13.3 pia linaonyesha kuwa wakazi wa vijijini wanaelekea zaidi kuomba kupatiwa taarifa, ambapo 20% ya wananchi waliosailiwa waliomba kupatiwa taarifa katika ngazi ya kijiji / mtaa. 14% ya wananchi wa vijijini waliosailiwa walipewa taarifa walizoziomba, wakati 6% waliomba kupewa taarifa, lakini hawakupewa.

**Jedwali 13.3** Maombi ya Kupewa Taarifa za Umma

| Taarifa Ziliombwa Kutoka: | Dar es Salaam % | | Miji Mingine % | | Maeneo ya Vijijini % | | Kote % | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Ndiyo | Hapana | Ndiyo | Hapana | Ndiyo | Hapana | Ndiyo | Hapana | Jumla ya Ndio |
| Wilaya | 4 | 3 | 4 | 4 | 4 | 3 | 4 | 3 | 7 |
| Kata | 8 | 6 | 8 | 6 | 8 | 5 | 8 | 5 | 13 |
| Kijiji / Mtaa | 6 | 4 | 8 | 5 | 14 | 6 | 10 | 5 | 15 |

**Ufunguo:** 'Ndiyo'= Taarifa zilizoombwa na kutolewa. 'Hapana' = Taarifa zilizoombwa lakini hazikutolewa.

Wananchi waliosailiwa waliulizwa maswali kadhaa kuhusu ushiriki wao katika kufanya maamuzi kwenye maeneo wanayoishi, jambo linalohimizwa na serikali katika sera yake rasmi. Jedwali 13.4 linaonyesha hisia walizo nazo wananchi kuhusu kushiriki katika masuala yahusuyo sera na maendeleo. Katika maeneo yote ambako utafiti ulifanywa, idadi kubwa kidogo ya wananchi waliosailiwa walikuwa na maoni kwamba wananchi wanaoeleza maoni yao mbele za watu huleta mabadiliko na 39% walikuwa na maoni kuwa viongozi wa serikali hawasikilizi yale wanayoyasema wananchi.

**Jedwali 13.4** Maoni Iwapo Ushirikishwaji wa Watu Huleta Mabadiliko

| Maoni kuhusu Iwapo Kuna Manufaa kwa Wananchi Kuhudhuria Mikutano Inayojadili Masuala ya Maendeleo ya Maeneo Yao | Dar es Salaam % | Miji Mingine % | Maeneo ya Vijijini % | Kote % |
|---|---|---|---|---|
| A. Watu kama mimi huleta mabadiliko kwa kueleza maoni yetu mbele za watu kuhusu mambo yanayotuathiri katika maeneo yetu | 52 | 54 | 53 | 53 |
| B. Hata kama mtu kama mimi akieleza maoni yake kwa masuala kama hayo, viongozi wa serikali hawasikilizi yale tunayoyasema | 39 | 38 | 39 | 39 |
| Sijui / Hakuna jibu lililotolewa | 9 | 8 | 9 | 9 |

**Angalizo:** Wananchi waliosailiwa waliombwa kuchagua kati ya A au B.

Swali linalohusiana na hilo liliulizwa ili kudadisi hisia za washiriki kuhusu kiwango ambacho wananchi hawana budi kushirikishwa katika masuala ya umma (Jedwali 13.5). Wengi wa wananchi waliosailiwa,

65%, walisema kuwa watu wa kawaida hawana budi kushirikishwa zaidi katika kufanya maamuzi yanayohusu masuala ya msingi ya uchumi na maendeleo ya jamii yanayoathiri maisha yao. Wakati huohuo, zaidi kidogo ya robo, 27%, walikuwa na maoni kuwa licha ya kuwashirikisha wananchi, serikali ndiyo yenye jukumu la kutoa huduma nzuri kwa wananchi na kwamba wananchi wa kawaida hawana uwezo mkubwa wa kuifanya serikali iboreshe utendaji kazi wake.

**Jedwali 13.5 Maoni kuhusu Iwapo Wananchi Hawana Budi Kushirikishwa Zaidi katika Kufanya Maamuzi kwenye Masuala ya Umma**

| Maoni kuhusu Iwapo Wananchi Hawana Budi Kushiriki katika Masuala ya Umma | Dar es Salaam % | Miji Mingine % | Maeneo ya Vijijini % | Kote % |
|---|---|---|---|---|
| A. Wananchi wa kawaida hawana budi kushirikishwa zaidi katika kufanya maamuzi yahusuyo masuala ya msingi ya uchumi na maendeleo ya jamii yanayoathiri maisha yao | 65 | 64 | 66 | 65 |
| B. Ni wajibu wa serikali kuwapa wananchi huduma nzuri: wananchi wa kawaida hawana uwezo mkubwa wa kuifanya serikali iboreshe utendaji kazi wake | 27 | 30 | 27 | 27 |
| Sijui / Hakuna jibu lililotolewa | 9 | 7 | 7 | 8 |

Hivyo basi, katika maeneo yote kulikofanywa utafiti huu, Watanzania wenye umri wa utu uzima walielekea zaidi kuunga mkono msukumo wa wananchi kuliko kuwaacha tu viongozi 'kuendelea na kazi zao'. Watanzania walio wengi wanaona kuwa ushiriki wa wananchi katika kufanya maamuzi ni wajibu wao wa kiraia, lakini wana mashaka kama kweli viongozi wa serikali wanayo nia ya kuwasikiliza.

### 13.2 Habari na Mawasiliano

Kama ilivyokwisha kuonyeshwa hapo juu, Watanzania wengi wenye umri wa utu uzima wanapendelea masuala ya siasa na ya umma, huku wengi wao wakiamini kuwa sauti ya watu huleta mabadiliko katika utendaji kazi wa serikali na katika utoaji huduma, na hata walio wengi zaidi wanaona kuwa wananchi wa kawaida hawana budi kushirikishwa katika kusimamia utendaji kazi wa watendaji wa serikali. Uchunguzi wa kina kuhusu namna watu wazima wanavyopata habari ili waweze kushiriki kikamilifu umeonyeshwa katika sehemu hii.

Watu wazima waliokuwa katika sampuli ya utafiti huu waliulizwa kuhusu vyanzo vyao vikuu vya kupatia habari zinazohusu masuala ya umma (Jedwali 13.6). Matangazo ya redio yalikuwa chanzo muhimu zaidi cha habari nchini kote kwa 60%, tena umuhimu wake ukiwa juu kidogo katika maeneo ya mijini kuliko ya vijijini. Magazeti na televisheni ni vyanzo muhimu mno vya habari jijini Dar es Salaam kuliko sehemu nyingine za nchi. 'Habari za kuambiwa' ni chanzo muhimu cha habari kwa 21% ya Watanzania waishio mijini na vijijini. Kwa ujumla, wananchi wa Dar es Salaam hupata habari kwa kiwango kikubwa mno kuliko wananchi wengine.

**Jedwali 13.6 Vyanzo vya Habari kwa Maeneo Mbalimbali**

| Chanzo Muhimu cha Habari za Siasa, Michezo na Masuala ya Kimataifa | Dar es Salaam % | Miji Mingine % | Maeneo ya Vijijini % | Kote % |
|---|---|---|---|---|
| Redio | 67 | 63 | 56 | 60 |
| Habari za kuambiwa | 19 | 22 | 22 | 21 |
| Magazeti | 44 | 24 | 7 | 20 |
| Televisheni | 43 | 20 | 5 | 18 |
| Mikutano ya wananchi | 7 | 13 | 15 | 12 |
| Kanisa / msikiti | 8 | 11 | 5 | 7 |
| Asasi za kijamii / zisizo za kiserikali | 3 | 3 | 2 | 2 |

Watu wazima waliulizwa pia kuwa ni kwa kiasi gani hupata habari kutoka kwenye vyombo vikuu vya habari. Jedwali 13.7 linaonyesha kuwa Watanzania wengi wenye umri wa utu uzima husikiliza redio mara kwa mara. Jijini Dar es Salaam ambako magazeti na televisheni hupatikana kwa urahisi zaidi kuliko sehemu nyingine, 43% ya watu waliosailiwa walisema pia kuwa huangalia televisheni mara kwa mara na

44% walisema husoma magazeti mara kwa mara. Kuongezeka kwa umuhimu wa simu za mkononi kama njia ya mawasiliano na chanzo cha habari unajidhihirisha, ambapo 35% ya watu wazima waliosailiwa walimiliki simu za mkononi: kati yao 65% kwa Dar es Salaam na 16% kwa maeneo ya vijijini.

**Jedwali 13.7** **Kupata Habari Mara kwa Mara**

| Kupata Habari Mara kwa Mara kutoka Vyombo vya Habari | Dar es Salaam % | Miji Mingine % | Maeneo ya Vijijini % | Kote % |
|---|---|---|---|---|
| Kusikiliza redio | 61 | 58 | 52 | 56 |
| Kuangalia televisheni | 40 | 17 | 5 | 17 |
| Kusoma gazeti | 36 | 21 | 6 | 17 |

Majibu haya ya watu wazima yanamaanisha kuwa kuna habari muhimu za kuupasha umma. Utafiti uliofanywa kwa watoto wa shule ya msingi ulibainisha kipengele kingine muhimu katika upashanaji habari - nacho ni cha kusikiliza. Kwa kutumia utafiti uliofanywa kwa watoto wadogo wa shule ya msingi, ni dhahiri kwamba 'mfumo' wa kusikiliza maoni ya watoto ni duni. Fikra kuu walizo nazo walimu katika utoaji elimu ni zile zinazojali zaidi upande wa mwalimu, si upande wa mwanafunzi - kazi yao ni kueleza tu kwa ufasaha ili jambo fulani lieleweke kwa wanafunzi badala ya kuchokoza fikra za ndani za wanafunzi na kuwawezesha kujifunza kwa uhuru zaidi katika kuuelewa ulimwengu wanaoishi.

Shule moja tu ya msingi kati ya shule kumi zilizo kwenye sampuli ya utafiti ndiyo iliyokuwa na baraza hai la shule. Katika shule chache sana ambazo wanafunzi walipata fursa ya kuwakilishwa katika kamati za shule, picha waliyoipata wanafunzi ni kwamba hawasikilizwi kwa makini. Katika shule ambazo hawawakilishwi moja kwa moja, wanafunzi walionyesha kutofahamu vikao vilifanyika lini na nini kilichojadiliwa.

### 13.3 Ufahamu na Maoni kuhusu Sera

Maoni kuhusu masuala teule ya sera yalitafutwa ili kuchunguza kiwango cha ufahamu wa wananchi kuhusu mijadala ya siku za karibuni inayohusu sera na iwapo hufuatilia mambo haya.

#### Ufahamu wa Wananchi kuhusu MKUKUTA

Kitaifa, karibu watu wawili tu kati ya watano waliosailiwa, 38%, ndiyo waliosema kuwa wamewahi kusikia habari za MKUKUTA, na kwa vijijini, 34% ndiyo waliosema hivyo. Wengi wa wale waliosema kuwa wamewahi kusikia habari za MKUKUTA walidhani kuwa mkakati huo ulikuwa ukishughulika na suala pekee la kutengeneza ajira na kukuza uchumi, na pungufu ya 10% waliweza kubainisha makundi matatu ya MKUKUTA katika swali walilotakiwa kuchagua jibu sahihi kutoka katika orodha iliyokuwa na majibu mengi.

**Jedwali 13.8** **Ufahamu wa Wananchi kuhusu MKUKUTA**

| Je, umepata kusikia habari za MKUKUTA? | Dar es Salaam % | Miji Mingine % | Maeneo ya Vijijini % | Kote % |
|---|---|---|---|---|
| Ndiyo | 40 | 44 | 34 | 38 |
| Hapana | 60 | 56 | 66 | 62 |

Kabla ya kukaribisha maoni ya wananchi kuhusu masuala mahususi yahusuyo sera, hojaji iliuliza iwapo walikuwa na maoni yoyote kuhusu sera na utendaji kazi wa serikali. Zaidi ya theluthi mbili walisema walikuwa nayo, na karibu 34% (theluthi moja) walitoa majibu yenye mtazamo hasi, wengi wao wakiwa wanawake kuliko wanaume.

#### Mada Muhimu kwa Sasa

Washiriki waliulizwa maswali kuhusu mada mbalimbali kama iwapo makampuni ya uchimbaji madini yalikuwa yakilipa kodi ya kutosha au hapana, jambo lililosababisha tatizo kubwa la ukosefu wa umeme mwaka 2006, faida na hasara za kuwahamisha *wamachinga* (wafanyabiashara wa mitaani) kutoka

maeneo ya katikati ya miji na kuhusu misaada kutoka nchi za nje. Karibu nusu ya watu wazima waliosailiwa hawakuwa na maoni yoyote kuhusu mada hizi. Kwa wale waliotoa maoni yao, karibu wote (96%) waliamini kuwa makampuni ya uchimbaji madini hayana budi kulipa kodi kubwa zaidi. Kulikuwa na maoni yanayotofautiana kuhusu suala la *wamachinga* - 58% waliunga mkono hatua hiyo, wakati 34% waliikosoa hatua hiyo ya serikali. Karibu robo tatu (74%) wanaamini kuwa tatizo kubwa la umeme lilisababishwa na ukame. Watu wanne kati ya watano waliosailiwa, 81%, wanaamini kuwa 'misaada ya kigeni hunufaisha zaidi viongozi wa serikali,' na karibu theluthi mbili, 64%, ya watu waliotoa maoni yao wanakubaliana mno na wazo hilo.

### 13.4 Maoni kuhusu Viongozi wa Serikali na Vyama vya Siasa

#### Utendaji wa Viongozi wa Serikali

Maswali kadhaa yaliulizwa pia ili kutathmini maoni waliyo nayo wananchi kuhusu utendaji wa viongozi wa serikali na wa vyama vya siasa kwa miaka kadhaa iliyopita. Wengi wa watu wazima waliosailiwa walitoa maoni yaliyoonyesha kufurahishwa na utendaji kazi wa viongozi wengi wa ngazi za juu za serikali na wabunge. Zaidi ya 40% ya wananchi waliosailiwa waliona pia kuimarika kwa utendaji wa viongozi wa serikali za mitaa, madiwani, viongozi wa serikali za vijiji na askari polisi.

#### Mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa

Hatimaye, utafiti huu uliwauliza wananchi kuwa wanauonaje mfumo wa siasa za ushindani ulioanzishwa mwaka 1992. Idadi ya wananchi waliotoa maoni yao imegawanyika karibu sawa kati ya wale wanaopendelea mfumo wa chama kimoja cha siasa na wale wanaopendelea mfumo wa vyama vingi.

**Jedwali 13.9** Maoni ya Watu kuhusu Kuwa na Mfumo wa Chama Kimoja au Vyama Vingi vya Siasa

| Maoni kuhusu Mfumo wa Siasa | Dar es Salaam % | Miji Mingine % | Maeneo ya Vijijini % | Kote % |
|---|---|---|---|---|
| Ninayo furaha Tanzania kufuata mfumo wa vyama vingi | 46 | 47 | 44 | 45 |
| Heri Tanzania ingeendelea na mfumo wa chama kimoja | 37 | 40 | 42 | 41 |
| Mfumo wa chama kimoja / vyama vingi hauna tofauti yoyote ya maana | 8 | 7 | 6 | 7 |
| Hakuna maoni yaliyotolewa / Hawajafikia uamuzi | 9 | 7 | 7 | 7 |

### 13.5 Uwajibikaji

Utafiti huu ulichunguza pia ili kujua kama Watanzania waliona kuwa kuna mabadiliko katika juhudi za kuwafanya viongozi wa serikali kuwajibika zaidi. Kwa kuanzia, watu wazima waliombwa kutafakari iwapo kulikuwa na jambo lolote lililofanywa katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita likiwahusisha viongozi wa serikali kuu au serkali za mitaa ambalo kwao liliashiria kuwa utoaji wa huduma na uwajibikaji wa viongozi wa serikali ulikuwa unaimarika. Karibu 34% ya wananchi waliosailiwa walikiri kuwepo kwa hali hiyo, huku kukiwa na tofauti ndogo tu kati ya wananchi wa mijini na wale wa vijijini. Katika kudadisi zaidi, lilifuata swali lililowataka wananchi kueleza kinagaubaga kuhusu mabadiliko hayo waliyoyasema.

Kwa kiwango kikubwa, mabadiliko yaliyotajwa na wananchi walio wengi, 56%, yalikuwa katika elimu - kuboreshwa kwa shule, nyumba za walimu, na vyumba vya madarasa.

Maswali yaliulizwa kuhusu uwajibikaji wa viongozi. Karibu 32% ya washiriki walisema kulikuwa na mifano ya viongozi kutuhumiwa kwa kufuja fedha za umma na viongozi kufukuzwa kazi kwa rushwa na uzembe kazini. Washiriki wengine 24% walitaja mifano ya uboreshaji wa hali ya barabara kutokana na malalamiko ya wananchi.

| **Jedwali 13.10** Ushahidi wa Uwajibikaji | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Ushahidi wa Uwajibikaji** | **Dar es Salaam %** | **Miji Mingine %** | **Maeneo ya Vijijini %** | **Kote %** |
| Wananchi waliwatuhumu viongozi kwa kufuja rasilimali zilizokusudiwa kwa shughuli za maendeleo au huduma za jamii | 30 | 35 | 33 | 32 |
| Kiongozi wa serikali alifukuzwa kwa rushwa au uzembe kazini | 32 | 34 | 31 | 32 |
| Malalamiko kuhusu hali ya ubovu wa barabara yalisababisha ukarabati wa haraka | 25 | 28 | 22 | 24 |
| Mchanganuo wa matumizi ya fedha za umma uliotolewa na viongozi wa serikali ulikosolewa katika mkutano wa hadhara | 19 | 27 | 30 | 26 |
| Mwananchi mmojawapo alizungumzia kwenye mkutano wa hadhara taarifa zilizobandikwa katika ofisi ya serikali au kituo cha huduma kilichopo katika eneo husika | 11 | 12 | 13 | 12 |

Utafiti huu uliwauliza pia watu wazima maswali kadhaa kuhusu mabadiliko waliyoyaona siku za karibuni katika uwajibikaji wa viongozi wa umma na njia zilizotumiwa ili kuongeza uwajibikaji. Katika tathmini yao, washiriki walikiri kuwepo kwa hali ya mabadiliko katika siku za karibuni, hususan kuhusu mwitikio wa serikali kwenye masuala ya amani, utulivu na usalama na ubora wa huduma zinazotolewa kwa umma, huku wengi zaidi wakitaja kuongezeka badala ya kupungua kwa ubora katika maeneo hayo. Wakati huohuo, 44% ya watu wazima hawakutoa maoni yoyote kuhusu maswali haya.

| **Jedwali 13.11 Mwelekeo wa Uwajibikaji** | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwelekeo wa Uwajibikaji** | **Dar es Salaam %** | | **Miji Mingine %** | | **Maeneo ya Vijijini %** | | **Kote %** | |
| | ▲ | ▼ | ▲ | ▼ | ▲ | ▼ | ▲ | ▼ |
| Amani, utulivu na usalama kwa umma | 53 | 4 | 57 | 4 | 54 | 5 | 55 | 4 |
| Ubora wa huduma za msingi | 46 | 4 | 48 | 9 | 42 | 12 | 44 | 9 |
| Serikali kuheshimu sheria zilizopo | 36 | 6 | 43 | 5 | 41 | 6 | 40 | 6 |
| Kusimamia uchumi ipasavyo | 32 | 5 | 40 | 6 | 37 | 8 | 36 | 7 |
| Uvumilivu wa serikali inapokosolewa | 37 | 7 | 39 | 11 | 34 | 10 | 35 | 9 |
| Magazeti kuchunguza masuala ya rushwa | 35 | 6 | 31 | 10 | 20 | 11 | 25 | 9 |
| Kuwajibishwa kwa viongozi waandamizi wa kisiasa na kiserikali | 33 | 6 | 36 | 8 | 30 | 8 | 32 | 8 |
| Utendaji wa Taasisi ya Kuzuia [na Kupambana na] Rushwa | 32 | 7 | 35 | 9 | 30 | 9 | 31 | 8 |
| Mchango wa vyama vya upinzani bungeni | 31 | 10 | 27 | 18 | 24 | 19 | 27 | 16 |
| Haki / usawa katika ulipaji kodi | 16 | 6 | 18 | 10 | 18 | 10 | 17 | 8 |

**Ufunguo:** ▲ = Kuongezeka kwa uwajibikaji ▼ = Kupungua kwa uwajibikaji

## 13.6 Rushwa

Mara nyingi rushwa huchukuliwa kuwa kikwazo kikubwa katika kuleta utawala bora. Mtazamo kwamba rushwa imeenea miongoni mwa viongozi hushusha imani ya wananchi kwa vyombo vya serikali na watoa huduma. Kipengele hiki kinaangalia maoni waliyo nayo Watanzania kuhusu namna rushwa ilivyoenea kote katika jamii.

### Kuenea kwa Rushwa

Karibu 40% ya watu wazima waliosailiwa hawakuwa na maoni yoyote kuhusu kiwango cha rushwa kilichopo katika jamii. Kwa wale waliotoa maoni yao, idadi iliyo karibu sawa na hiyo wanaona kuwa rushwa ndogondogo ni jambo la ‘kawaida sana’ au ni la ‘kawaida kabisa’ - hayo yalisemwa na 44% ya watu wazima waliotoa maoni yao, sawa na 24% ya watu wazima waliokuwa katika sampuli ya utafiti huu. Rushwa kubwakubwa ilichukuliwa kuwa ya 'kawaida sana' au ya 'kawaida kabisa' na karibu 41% ya wale

waliotoa maoni yao, sawa na 25% ya watu wazima wote waliosailiwa katika utafiti. Matokeo sawa na hayo yameripotiwa kuhusu rushwa ya kisiasa, ambapo 40% ya wale waliotoa maoni yao walibainisha kuwepo kwa hali hiyo, hao wakiwa sawa na 26% ya watu wazima wote waliosailiwa katika utafiti. Watu wenye hali nzuri kimaisha, wakazi wa mijini kwa kiasi fulani wanaelekea zaidi kuona rushwa kama jambo la kawaida kuliko watu maskini na wakazi wa vijijini.

**Jedwali 13.12** Maoni kuhusu Kuenea kwa Rushwa

| Rushwa ni Jambo la Kawaida Sana na/au ni la Kawaida Kabisa | Dar es Salaam % | Miji Mingine % | Maeneo ya Vijijini % | Kote % |
|---|---|---|---|---|
| Rushwa ndogondogo | | | | |
| - Wale waliotoa maoni, 60% ya waliosailiwa | 46 | 46 | 41 | 44 |
| - Idadi yao kwa washiriki wote | 22 | 29 | 24 | 24 |
| Rushwa kubwakubwa | | | | |
| - Wale waliotoa maoni, 60% ya waliosailiwa | 43 | 44 | 38 | 41 |
| - Idadi yao kwa washiriki wote | 24 | 30 | 24 | 25 |
| Rushwa ya kisiasa | | | | |
| - Wale waliotoa maoni, 60% ya waliosailiwa | 40 | 40 | 39 | 40 |
| - Idadi yao kwa washiriki wote | 23 | 27 | 26 | 26 |

Washiriki waliulizwa zaidi kuhusu kiwango ambacho wanaona kuwa rushwa huathiri maisha yao na ya familia zao, biashara na siasa nchini Tanzania. Karibu 45% ya watu waliosailiwa waliona kuwa rushwa ilikuwa ikiathiri maisha yao, 42% maisha ya biashara, na 39% maisha ya kisiasa. Watu wachache tu, 8%, ndiyo walioamini kuwa rushwa haiathiri nyanja hizi tatu za maisha. Kwa mara nyingine tena, idadi kubwa ya watu waliosailiwa hawakutoa maoni yoyote katika maeneo haya matatu (idadi yao ikiwa kati ya 38% na 43%).

Maoni ya watu yalikusanywa pia kuhusu kiwango cha rushwa kilichopo katika sekta mbalimbali za utoaji huduma (Jedwali 13.13). Jeshi la Polisi na mfumo wa mahakama zinaonekana machoni mwa wananchi kama taasisi zilizokubuhu mno kwa rushwa, huku zaidi ya 40% wakiripoti kuwa taasisi hizi zimeathiriwa 'sana' kwa rushwa. Kwa ujumla, wakazi wa mijini wanaona kuwepo kwa hali mbaya zaidi ya rushwa katika sekta za umma kuliko wale wa vijijini, ingawa kwa ujumla tofauti hizo za maoni siyo kubwa sana.

**Jedwali 13.13** Maoni kuhusu Kiwango cha Rushwa katika Sekta Mbalimbali

| Sekta Zinazoonekana Kuathiriwa 'Sana' kwa Rushwa | Dar es Salaam % | Miji Mingine % | Maeneo ya Vijijini % | Kote % |
|---|---|---|---|---|
| Jeshi la Polisi | 48 | 51 | 44 | 46 |
| Mfumo wa mahakama | 43 | 50 | 42 | 44 |
| Huduma za afya | 32 | 40 | 31 | 33 |
| Usajili na vibali | 26 | 30 | 21 | 24 |
| Sekta ya elimu | 21 | 26 | 19 | 21 |
| Kodi ya mapato | 21 | 24 | 17 | 19 |
| Matumizi ya nyumbani | 19 | 20 | 13 | 16 |

### Utoaji Rushwa

Washiriki waliulizwa iwapo wao wenyewe au mtu mwingine katika kaya alienda kutafuta huduma mbalimbali katika kipindi cha mwaka mmoja kabla ya kufanywa kwa utafiti huu, na iwapo rushwa ilitolewa. Katika Jedwali 13.14, safu 'C' inawakilisha uwiano wa kaya zilizofanya safari za kukutana na watu mbalimbali wanaotoa huduma, na safu 'B' ni uwiano wa idadi ya safari za kukutana na watoa huduma ambazo rushwa ilitolewa.

**Jedwali 13.14 Kukutana na Watoa Huduma na Utoaji wa Rushwa**

| Mtoa Huduma | Dar es Salaam % | | Miji Mingine % | | Maeneo ya Vijijini % | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | C | B | C | B | C | B |
| Jeshi la Polisi | 20 | 55 | 9 | 33 | 9 | 33 |
| Mfumo wa mahakama | 14 | 43 | 9 | 22 | 9 | 22 |
| Usajili na vibali | 14 | 29 | 6 | 17 | 6 | 17 |
| Sekta ya kodi | 7 | 14 | 4 | 0 | 4 | 0 |
| Sekta ya elimu | 27 | 15 | 31 | 10 | 32 | 3 |
| Matumizi ya nyumbani | 12 | 17 | 5 | 0 | 5 | 0 |
| Sekta ya afya | 42 | 24 | 43 | 9 | 43 | 9 |

**Angalizo: C =** ni uwiano wa kaya zinazowatafuta watoa huduma **B =** ni uwiano wa wanaotoa rushwa

Kwa mara nyingine, taasisi za utoaji huduma zilizotajwa ambazo kulikuwa na matukio mengi zaidi ya utoaji rushwa ni polisi na mfumo wa mahakama. Jijini Dar es Salaam, 55% ya safari za wananchi kutafuta huduma za polisi zilihusisha utoaji rushwa, na 43% kwa mfumo wa mahakama. Karibu 42% ya wananchi waliosailiwa walionyesha kuwa wao wenyewe au watu wengine katika kaya walitumia huduma za afya katika kipindi cha mwaka mmoja uliotangulia. Jijini Dar es Salaam, karibu robo ya safari za kuonana na watoa huduma (24%) zilihusisha utoaji rushwa, na kwa wakazi wengine wa mijini na vijijini, 9% waliarifu kuwa walilazimika kutoa rushwa. Kwa wale waliosema kuwa walitoa rushwa, maswali yaliulizwa kuhusu kiwango walichokitoa. Hata hivyo, idadi ya majibu yaliyotolewa ilikuwa ndogo sana, na tofauti ya viwango vya pesa vilivyodaiwa kutolewa ilikuwa kubwa, hivyo kufanya uchambuzi wa majibu haya kuwa mgumu.

Hapa chini kuna mifano ya maoni ya baadhi ya watu waliyoyatoa kwenye majadiliano ya vikundi maalumu yanayoonyesha kwamba watu hutoa rushwa ili kukwepa kushikiliwa na polisi, kwamba kutoa taarifa za rushwa kunachukuliwa kuwa jambo la hatari na lisilozaa matunda yoyote, na kwamba haki za watu huuzwa na kununuliwa katika mfumo wa mahakama.

**SANDUKU 8**: RUSHWA

*"Kama mtu una malalamikio ya rushwa huwa unanyamaza tu. PCB (yaani Taasisi ya Kuzuia [na Kupambana na] Rushwa) walikuja na kutuachia vipeperushi. Wezi tunaowakamata huwa tunawapeleka polisi, ila baada ya siku mbili huwa wanarudi vijijini hivyo rushwa ipo wilayani na mijini sehemu nyingine hasa polisi na mahakamani."*
• Majadiliano ya Kikundi Maalumu cha Wanaume

*"Hakuna jinsi, serikali si ile ile tu? Afadhali unyamaze, maana ukiripoti ni hatari zaidi unawezahata kuuawa."*
• Majadiliano ya Kikundi Maalumu cha Wanawake

*'Mzee William na kaka yake wote wanafanya kazi ya ulinzi jijini Dar es Salaam. Siku moja usiku mnamo Julai 2007, wezi walivunja na kuingia kwenye jengo lililokuwa linalindwa na kaka yake Mzee William na kuiba mabati kadhaa. Kaka yake Mzee William alikamatwa kwa tuhuma za kuwasaidia wezi kuiba ingawa yeye anasisitiza kuwa alikuwa amelala. Alifunguliwa mashtaka kwa wizi wa mabati na mbao vyenye thamani ya shilingi 700,000/- za Kitanzania na kuwekwa rumande. Yeye anadai kuwa vifaa vilivyoibwa havina thamani hata chembe ya kiasi hicho. Mzee William alitoa shilingi 40,000/- ili kaka yake aachiwe kutoka rumande. Mzee William ambaye hupata ujira wa shilingi 110,000/- kwa mwezi ana wasiwasi kuwa hataweza kupata kiasi cha pesa kinachohitajika ili kaka yake 'asipatikane na hatia' kesi itakaposikilizwa.'*
• Uchunguzi wa simulizi za maisha ya watu, Mikocheni, Dar es Salaam

Waliosailiwa waliombwa kutathmini juhudi za serikali ya sasa katika kupambana na rushwa, na matokeo yake yameonyeshwa katika Jedwali 13.15. Karibu 40% ya wananchi waliosailiwa hawakutoa maoni yoyote. Kwa wale waliotoa maoni yao, wengi zaidi walikuwa na maoni kuwa serikali inafanya jambo jema katika kupambana na rushwa ikilinganishwa na wale walioona kuwa hakuna kinachofanyika. Chini ya mtu mmoja kati ya kila watu watano waliosailiwa walikuwa na maoni kuwa juhudi za serikali hazina nguvu.

**Jedwali 13.15 Maoni kuhusu Juhudi za Serikali ya Sasa katika Kupambana na Rushwa**

| Juhudi za Serikali Dhidi ya Rushwa | Dar es Salaam % | Miji Mingine % | Maeneo ya Vijijini % | Kote % |
|---|---|---|---|---|
| Zina nguvu | 41 | 48 | 45 | 45 |
| Hazina nguvu | 18 | 17 | 18 | 17 |
| Sijui / Hakuna jibu lililotolewa | 41 | 35 | 38 | 38 |

# UAMINIFU, USHIRIKIANO NA USALAMA

Utafiti huu ulichunguza mitazamo na hisia za Watanzania kuhusu masuala mbalimbali nyeti katika jamii. Uaminifu ni gundi inayounganisha jamii mbalimbali pamoja: watu wanaoaminiana wana uwezekano mkubwa zaidi wa kushirikiana kuliko watu ambao mara kwa mara hushuku nia za wengine. Watu wenye kuwaamini wale wanaotoa huduma serikalini na kuaminiana wao kwa wao wana uwezekano mkubwa zaidi wa kufanya kazi pamoja katika kufanikisha malengo waliyojiwekea pamoja kuliko watu wasioaminiana. Malengo ya pamoja yanajumuisha utunzaji wa rasilimali za wote na kuwalinda wanajamii walio katika hatari kubwa zaidi ya kudhuriwa na majanga ya asili kama vile ukame na baa la njaa, na masuala yanayoshtua katika jamii kama vile maradhi, ukosefu wa ajira na umaskini wa kupindukia. Malengo ya aina hiyo ni sehemu ya majukumu ya MKUKUTA na sera mbalimbali za kisekta. Kuwalinda watoto wadogo na wazee ni majukumu muhimu sana ambayo hushirikisha familia, jamii, na serikali. Hivyo basi, utafiti huu ulilenga kuchunguza kiwango cha uaminifu kilichoko katika jamii ya kisasa ya Watanzania.

## 14.1 Uaminifu

Watu wazima waliosailiwa waliulizwa, “Je, kwa ujumla, unaweza kusema kwamba siku hizi watu wengi wanaaminika, au kwamba watu wengi hawaaminiki?” Jedwali 14.1 linaonyesha kuwepo kwa viwango vya chini mno vya uaminifu. Idadi ndogo tu ya watu wazima waliosailiwa (22%) wanaamini kuwa, kwa ujumla, watu wengi ni waaminifu, huku 78% wakiamini kuwa watu wengi si waaminifu. Kiwango cha watu kutoaminiana kiko juu zaidi jijini Dar es Salaam (85%) kuliko vijijini (75%).

**Jedwali 14.1 Kiwango cha Uaminifu katika Jamii**

| Kiwango cha Jumla cha Uaminifu katika Jamii | Dar es Salaam % | Miji Mingine % | Maeneo ya Vijijini % | Kote % |
|---|---|---|---|---|
| Watu wanaaminika | 15 | 25 | 25 | 22 |
| Watu hawaaminiki | 85 | 75 | 75 | 78 |

Baada ya swali hili la juujuu, utafiti huu ulidadisi zaidi kwa kuuliza kuhusu kiwango cha kuaminiwa cha baadhi ya makundi mahususi katika jamii (Jedwali 14.2). Katika hali isiyoshangaza, watu waliosailiwa walielekea zaidi kuwaamini watu wa familia zao na ndugu zao wa ukoo kuliko watu wa makundi mengi katika jamii wanayohusiana nayo kwa mbali, lakini hata hapa pia, viwango vikubwa vya kutoaminiana vinaonekana dhahiri. 5% tu ya watu waliosailiwa ndiyo waliowachukulia ‘wageni’ wasio Watanzania' kuwa watu wenye kuaminika sana na 9%-10% waliwachukulia hivyohivyo vijana wa kike na wa kiume.

Watu wazima waliosailiwa - 40% waliwachukulia wageni Watanzania kuwa si waaminifu, na idadi karibu sawa na hiyo walisema hivyohivyo kwa vijana wa kiume. Zaidi ya nusu, 60% waliwachukulia wageni wasio Watanzania kuwa si waaminifu.

**Jedwali 14.2** Makundi Yanayoaminika katika Jamii

| Makundi Yanayoaminika Sana | Dar es Salaam % | Miji Mingine % | Maeneo ya Vijijini % | Kote % |
|---|---|---|---|---|
| Wanafamilia | 60 | 65 | 68 | 66 |
| Viongozi wa dini | 37 | 39 | 48 | 43 |
| Ndugu wa ukoo | 36 | 37 | 41 | 39 |
| Walimu | 20 | 24 | 33 | 28 |
| Watu wa kabila moja | 16 | 23 | 29 | 25 |
| Wazee wa kike | 21 | 24 | 32 | 27 |
| Wazee wa kiume | 18 | 22 | 30 | 26 |
| Mwenyekiti wa kijiji / kata | 12 | 24 | 28 | 23 |
| Madaktari na wauguzi | 17 | 21 | 27 | 23 |
| Viongozi wa serikali za mitaa | 12 | 22 | 25 | 21 |
| Wanasiasa | 7 | 15 | 18 | 14 |
| Wafanyabiashara | 7 | 12 | 15 | 12 |
| Viongozi wa asasi zisizo za kiserikali | 6 | 11 | 15 | 12 |
| Polisi | 8 | 12 | 14 | 12 |
| Wageni Watanzania | 6 | 8 | 13 | 10 |
| Vijana wa kike | 5 | 9 | 13 | 10 |
| Vijana wa kiume | 4 | 8 | 11 | 9 |
| Wageni wasio Watanzania | 3 | 8 | 13 | 5 |

### 14.2 Uhalifu na Ulevi

Tahadhari inayochukuliwa na watu katika kuwaamini wenzao inajionyesha kwenye maoni yanayohusu usalama wa watu binafsi na vilevile kwenye maoni yao kuhusu kiwango cha uhalifu, vurugu na matatizo mengine ya kijamii. Kwa ujumla, watu wana wasiwasi kuhusu kuwepo kwa uhalifu, vurugu na kutokuwepo kwa usalama, lakini mara nyingi kuna tofauti ya maoni kuhusu kiwango ambacho hali ni mbaya na iwapo hali inaimarika au inazidi kuwa mbaya. Utafiti huu ulichunguza maoni ya wananchi kuhusu athari na mwelekeo wa matatizo haya na matatizo mengine ya kijamii (Jedwali 14.3).

Kwa ujumla, ulevi (kwa kuuhusisha na uhalifu) ulichukuliwa kuwa tatizo kubwa na 63% ya watu wazima wote waliosailiwa, huku mtazamo huo ukionekana kuenea zaidi miongoni mwa wakazi wa vijijini. Kwa wastani, athari za ulevi zinadhaniwa kuwa zinazidi kuongezeka, huku athari ya matatizo mengine ya kijamii - kama vile migogoro ya mirathi na umiliki wa ardhi, matumizi ya mihadarati, tuhuma za uchawi na vurugu majumbani - zinachukuliwa kuwa zinapungua, mara nyingi kwa kiwango kikubwa. Hata hivyo, zaidi ya nusu ya washiriki wanauchukulia wizi wa mali za watu kuwa tatizo kubwa, huku washiriki wengi zaidi wa jijini Dar es Salaam wakilitaja tatizo hili. Matumizi ya mihadarati na kujichukulia sheria mkononi pia yanachukuliwa kuwa matatizo makubwa jijini Dar es Salaam kuliko sehemu nyingine.

Mbali ya ulevi na wizi, watu wachache tu waliosailiwa ndio waliochukulia aina nyingine za vurugu na hali ya kutokuwepo kwa usalama kuwa nayo ni matatizo makubwa. Ingawa haichukuliwi kuwa matatizo makubwa, migogoro ya umiliki wa ardhi, urithi (bila shaka wa mashamba pia), uchawi na vurugu majumbani inaonekana kuenea zaidi vijijini kuliko mijini. Kisanduku Namba 9 kinaonyesha baadhi ya maoni ya watu kuhusu suala la ulevi.

| **Jedwali 14.3** Maoni kuhusu Uhalifu, Vurugu na Kukosekana kwa Usalama | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Matatizo Makuu ya Uhalifu na Vurugu katika Jamii** | **Dar es Salaam %** | **Miji Mingine %** | **Maeneo ya Vijijini %** | **Kote %** | **Tatizo Linazidi %** | **Tatizo Linapungua %** |
| Ulevi | 54 | 59 | 64 | 63 | 33 | 24 |
| Wizi wa mali | 56 | 49 | 50 | 52 | 25 | 43 |
| Migogoro ya kumiliki ardhi | 20 | 33 | 47 | 37 | 18 | 28 |
| Tuhuma za uchawi | 23 | 33 | 44 | 36 | 18 | 25 |
| Migogoro ya matumizi ya ardhi | 18 | 28 | 43 | 34 | 18 | 26 |
| Matumizi ya mihadarati | 43 | 31 | 28 | 33 | 19 | 22 |
| Vurugu majumbani | 24 | 27 | 32 | 29 | 11 | 36 |
| Migogoro ya mirathi | 15 | 23 | 32 | 25 | 13 | 26 |
| Kujichukulia sheria mkononi | 36 | 18 | 15 | 21 | 12 | 31 |
| Udhalilishaji wa watoto | 18 | 17 | 21 | 20 | 9 | 31 |
| Ubakaji | 17 | 14 | 17 | 16 | 9 | 29 |
| Mauaji ya watuhumiwa wa uchawi | 6 | 7 | 12 | 10 | 5 | 21 |

**SANDUKU 9**: **HALI YA ULEVI NCHINI TANZANIA**

*"Ulevi upo. Wengi hufanya ulevi kama njia ya kujiliwaza kutokana na umasikini."*
• Kikundi Maalumu cha Wanawake

*"Ulevi ni tatizo kubwa hata kwetu wanawake. Sasa kama baba na mama wote mnalewa, unafikiri kuna maelewano tena hapo?"*
• Kikundi Maalumu cha Wanawake

*"Ulevi ni tatizo kubwa sana. Tunavumilia, tunashindwa; lakini, hata wanawake walevi wapo."*
• Kikundi Maalumu cha Wanawake

*"Ulevi ni tatizo kubwa. Kila mtu baada ya kazi utamkuta na chupa ya pombe hadi saa nane za usiku, wengine wanaanza asubuhi."*
• Kikundi Maalumu cha Wanaume

*"Ulevi hapa kwa ujumla ni tatizo ambalo hupelekea matatizo mengi kama mifarakano na maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi."*
• Kikundi Maalumu cha Wanaume

*"Ulevi upo lakini siyo tatizo. Hapa watu wako busy na shughuli za kuingiza vipato."*
• Kikundi Maalumu cha Wanaume

Washiriki waliombwa kutoa maoni yao kuhusu suala la watu kujichukulia sheria mkononi. Karibu mbili ya tano ya washiriki, 38%, walikuwa wamepata kusikia kuwepo kwa matukio ya watu kujichukulia sheria mkononi kwenye wilaya zao katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita, na nusu ya waliosailiwa Dar es Salaam, lakini karibu robo tatu ya wasailiwa wote, 71% walisema hakuna sababu inayoweza kuhalalisha mauaji ya watu wanaotuhumiwa kwa wizi; huku wale waliosema hivyo jijini Dar es Salaam walikuwa 61%.

Wakati Watanzania wanaonyesha kwa kiwango kikubwa kutowaamini watu wasiokuwa ndugu zao wa karibu, kwa ujumla maoni yao yanaonyesha kuwa wana matumaini makubwa sana na mwelekeo ambao umekuwepo kwa siku za karibuni wa kupungua kwa maradhi na matatizo ya kijamii, isipokuwa tatizo la ulevi, ambalo linatajwa kuwa linaongezeka na kuzidi kuenea, hususan vijijini.

### 14.3 Mshikamano na Ushirikiano katika Jamii

Taarifa zilitafutwa pia kuhusu mshikamano na ushirikiano wa jamii katika kufanya shughuli mbalimbali za kijamii - Jedwali 14.4. Washiriki wengi zaidi waliona kuwa jamii imepunguza badala ya kuongeza utoaji wa matunzo kwa watu maskini, wagonjwa na wazee, kuwalinda watoto dhidi ya ukatili na udhalilishaji na juhudi za kuwafunza watoto tabia nzuri. Ushirikiano wa wanajamii katika kukarabati barabara na madaraja, na tabia ya kushirikiana kuandaa mashamba kwa ajili ya kilimo na kuvuna mazao inaonekana kupungua pia. Kwa ujumla, kulikuwa na tofauti ndogondogo tu za maoni kati ya wakazi wa mijini na wale wa vijijini. Hata hivyo, karibu nusu ya washiriki wa vijijini waliona kuwa utunzaji wa misitu unaofanywa na jamii ulikuwa unaongezeka, idadi ambayo ni maradufu ya wale wanaoona kushuka kwa hali hiyo.

**Jedwali 14.4** Mwelekeo wa Mshikamano na Ushirikiano katika Jamii

| Mshikamano na Ushirikiano katika Jamii | Dar es Salaam % | | Miji Mingine % | | Maeneo ya Vijijini % | | Kote % | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | ↑ | ↓ | ↑ | ↓ | ↑ | ↓ | ↑ | ↓ |
| Kusaidia maskini, wagonjwa, wazee | 21 | 44 | 19 | 55 | 21 | 56 | 20 | 52 |
| Kuwafunza watoto tabia nzuri | 26 | 42 | 29 | 45 | 30 | 43 | 29 | 43 |
| Kuwalinda watoto dhidi ya ukatili / udhalilishaji | 26 | 32 | 28 | 38 | 32 | 33 | 29 | 34 |
| Kushirikiana kuandaa mashamba na kuvuna | - | - | 12 | 42 | 24 | 46 | 16 | 34 |
| Kukarabati barabara na madaraja ya eneo husika | 26 | 24 | 25 | 34 | 26 | 37 | 26 | 33 |
| Kulinda misitu isikatwe ovyo | - | - | 30 | 25 | 48 | 24 | 34 | 19 |

**Ufunguo:** ↑ = Kuongezeka ↓ = Kupungua

SURA YA
15

# HITIMISHO NA MAMBO YA KUFANYA KISERA

**Umaskini na Kukuza Uchumi**

Kwa kutumia matokeo ya utafiti, watu wengi zaidi wanaonekana kuwa na hali duni zaidi sasa kuliko walivyokuwa miaka mitatu iliyopita. Kwa watu wa madaraja yote ya vipato, ikiwa ni pamoja na wale wenye nafuu kimaisha, wengi wao wanaona kuna kushuka badala ya kupanda kwa hali ya maisha, na Watanzania wengi wenye umri wa utu uzima wanaona kupanda kwa gharama za maisha kuwa tatizo kubwa (hasa gharama za chakula). Wakulima, wafugaji, na wavuvi walio wengi waliripoti kwamba kwa kweli hawapati msaada wowote kutoka serikalini, na wangependa serikali itoe msaada mkubwa zaidi katika kuboresha upatikanaji wa nyenzo za uzalishaji mali na mikopo.

Hali ya ubovu wa barabara kuu za vijijini ilijitokeza kama kikwazo kikubwa cha shughuli za kiuchumi na juhudi za kupunguza umaskini vijijini, ingawa kwa hakika wakazi wa mijini walikiri kuwepo kwa mabadiliko kadhaa. Hivyo basi, uboreshaji wa hali ya barabara hauna budi kwenda sambamba na ongezeko la shughuli za uwekezaji ili kupunguza vikwazo katika utekelezaji na kuongeza uzalishaji katika sekta ya kilimo, na wananchi wanaomba bayana serikali ichukue hatua za dhati za kuboresha hali ya uchumi vijijini. Wakati huohuo, serikali imedhamiria kukuza uchumi katika sekta binafsi. Hivyo basi, matokeo haya ya utafiti yanatoa wigo mpana zaidi wa kutafakari maamuzi kuhusu majukumu ya serikali na yale ya sekta binafsi.

**Utoaji Huduma**

Serikali imekuwa ikitenga fedha zaidi katika bajeti yake kwa ajili ya utoaji wa huduma za jamii kwa miaka kadhaa sasa, na utafiti wa Maoni ya Watu (2007) unaonyesha jinsi wananchi wanavyounga mkono uwekezaji unaofanywa na serikali katika sekta ya elimu. Katika sekta ya afya, gharama kubwa za tiba na ununuzi wa madawa, na upungufu wa madawa vilitajwa kuwa vikwazo vikuu katika kupata huduma za afya, na pia ugumu uliopo kwa wananchi wengi wazee kupata huduma za bure za afya. Usambazaji wa maji kwa matumizi ya nyumbani, kwa mijini na vijijini, pia unaendelea kuwa tatizo sugu kama ulivyopimwa kwa kutumia taarifa zilizotolewa kuhusu kuwepo kwa uhaba wa maji safi na salama, na gharama kubwa sana za kupata maji. Ni dhahiri kuwa bado serikali inatakiwa kutenga fedha zaidi kwa ajili ya huduma za msingi katika jamii, na rasilimali zinazopatikana zitumiwe ipasavyo na kwa ufanisi.

**Utawala Bora**

Ukuaji endelevu kiuchumi, kupunguza umaskini na utoaji wa huduma bora, yote hutegemea mwongozo kutoka serikali kuu na serikali za mitaa. Utafiti wa Maoni ya Watu (2007) unaonyesha hofu waliyo nayo wananchi kuhusu madhara na kuenea kwa rushwa, lakini vilevile unaonyesha kuwa zaidi ya 40% ya wananchi waliosailiwa walikuwa na maoni kuwa serikali inafanya kazi nzuri katika kupambana na rushwa.

Kwa namna iletayo matumaini makubwa sana, utafiti huu unaonyesha kuwa wananchi wanaimani kubwa sana na uwezo wa serikali iliyopo madarakani katika kutunga na kutekeleza sera mbalimbali kwa manufaa ya umma. Kwa hakika, hii ni rasilimali muhimu sana ambayo haiwezi kudumu milele iwapo hakutakuwa na utoaji wa huduma bora na pia uwajibikaji mkubwa zaidi.

Huku ikikabiliwa na kushuka kwa kiwango cha mshikamano na ushirikiano kama ilivyoripotiwa na wananchi wa maeneo mbalimbali, kwa hakika kubuni njia za kuboresha shughuli za utawala ambapo wadau wote - serikali, wananchi, sekta binafsi na asasi za kiraia, watu wazima na watoto vilevile - watafanya kazi pamoja ili kufikia malengo ya pamoja kitaifa, kutaendelea kuwa mojawapo ya changamoto kubwa zaidi zinazoikabili Tanzania kwa miaka mingi ijayo.

# MAREJEO


ESRF (2004). "Tanzania Participatory Poverty Assessment"

REPOA, (2003). "Policy and Services Satisfactory Survey (PSSS)." Dar es Salaam: REPOA.

United Republic of Tanzania (URT). (2002). "Household Budget Survey 2000/01". Dar es Salaam: National Bureau of Statistics.

URT. (2004). "Vulnerability and Resilience to Poverty in Tanzania: Causes, Consequences and Policy Implications." TzPPA Main Report. Dar es Salaam: Vice President's Office.

URT. (2005). "National Strategy for Growth and Reduction of Poverty (NSGRP)". Dar es Salaam: Vice President's Office.